

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Kumi – Tarehe 16 Desemba, 2013

(Mkutano ulianza saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Zungu Azzan) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Spika, imetolewa chini ya Kanuni ya 33 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Katika Mkutano wake wa Kumi na Mbili Bunge lilipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali miwili iitwazo:-

*The National Irrigation Bill, 2013; na
The Cooperative Societies Bill, 2013.*

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba Miswada hiyo imeshapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria za nchi ziiwazo:-

The National Irrigation Act 2013 No. 4 ya Mwaka 2013; na

The Cooperative Societies Act 2013 No. 5 ya Mwaka 2013.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana.
(Makofi)

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Kamati hiyo kwa Mwaka 2013.

MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu yake kwa Mwaka 2013.

MASWALI NA MAJIBU:

Na. 105

Muda Unaotumika Kupata Mkopo wa Benki

MHE. HAMAD R. MOHAMED aliuliza:-

Je, kwa kawaida kama taratibu zote zimekamilika, mwombaji wa mkopo kwenye Benki za Biashara hutakiwa kupata mkopo wake baada ya muda gani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM)

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa wateja kupata mikopo baada ya taratibu zote kukamilika unatofautiana kati ya benki moja na benki nyingine kutegemeana na sera na taratibu za utoaji mikopo za benki husika.

Mfano kwa mkopo wa biashara sera ya *CRDB* inatamka siku 21, Benki *M (T) LTD.* siku 7, *NBC* siku 30, *NMB* siku 14, *Bank of Africa* siku 30. Aidha upande wa mkopo binafsi mara nyingi kutokana na sera za benki hizo hutolewa ndani ya siku 7.

Mfano mzuri ni *NMB* ambao hukamilisha mkopo binafsi ndani ya saa 24. Hata hivyo muda uliowekwa kisera kwa kila benki unaweza kupungua au kuongezeka kulingana na mazingira yaliyopo kati ya mwombaji na benki husika, aina ya biashara pamoja na uthibitisho wa nyaraka zinazohitajika kama dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tunatarajia kuona kwamba msukumo wa nguvu ya soko utayasukuma mabanki kuimarisha sera na taratibu zao za kutoa mikopo na hivyo kuwawezesha wateja wao kupata mikopo kwa wakati.

Pia Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kusimamia ubora, uimara na usalama wa uendeshaji wa shughuli za kibenki Taasisi za fedha na maduka ya kuuza na kununua fedha ili wananchi waweze kupata huduma zilizo bora na kwa wakati. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. RUKIA K. AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado nina masuala mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Mabenki yanayokopesha kwa mfano Wabunge, hawa watu ambao wana uhakika wa kulipa kila mwezi na pesa zazo zina uhakika ikawa riba iko vile vile hawapunguziwi.

Ni kwa nini Serikali hiingilii kati mabenki haya haya yamewakopesha Wabunge *Graduity* na wakati huo huo wanawakata riba

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu masuala mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rukia kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tukichukulia kikawaida ni wateja wa mabenki haya na riba ipo juu si tu kwa sababu ya uhakika wa kulipa lakini riba iko juu kwa sababu gharama za kutafuta zile fedha kwa ma benki zinakuwa ziko juu. Siyo tu Wabunge wana uhakika wa kulipa. Lakini vile vile Mbunge mmoja na Mbunge na Mbunge mwingine wanatofautiana kutokana na *income*.

Labda wengine wanakuwa wana dhamana nyingine zaidi kuliko mishahara yao. Wengine wana biashara mbalimbali. Kwa hiyo, gharama inakuwa iko juu hiyo ni kwa wote siyo kwamba ni Wabunge tu, lakini kikubwa ni kwa sababu fedha ambazo mabenki inazitafuta, inazitafuta katika riba kubwa *high coss of borrowing* na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti jingine ni *risk* gharama hii inatokana na *risk* ambayo inakuwa *associated* na mteja mwenyewe kwa sababu sasa hivi mfumo uliopo kwamba kupata taarifa za mteja inakuwa ni vigumu isipokuwa tu kuanzia mwaka jana tayari benki kuu imetoa ile *credit of reference bureau* ambayo itamwezesha sasa benki ikitaka kumkopesha mteja inaweza kujua taarifa zake, wapi anakaa,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

biashara gani anafanya, ana dhamana gani na kwa hiyo sasa hivi kutokana na hilo hata hizo riba zimeweza kuwa negotiable yaani benki moja inaweza ku-*negotiate* na mteja.

Kwa hivyo Mbunge kama mteja mwingine anahitaji vile vile kuwa na vile vielelezo ambayo vitahakikisha ile *risk* ya kumkopesha inakuwa ndogo zaidi, hilo tumelitekeleza through *Bank of Tanzania* ambayo sasa hivi tuna *create reference bureau* ambayo taarifa za mteja yoyote ukitaka kukopa zinapatikana *either* kama utakuwa labda una mkopo sehemu nyingine, umechukua mkopo wa kufanyia jambo jingine. Kwa hiyo, inahakikisha kwamba ile riba ambayo amekupa kwamba inahakikisha kwamba inarejesha fedha yake kwa wakati.

Lakini kuhusu Serikali iingilie kati, sasa hivi biashara ya benki imekuwa riberalised yaani inatokana na nguvu ya soko kwa hiyo Serikali hatuna mkono mkubwa sana wa kuingilia hilo, isipokuwa sisi tunaweka tu Sera zetu na taratibu kupitia Benki Kuu ya Tanzania tuhakikishe kwamba *at the end of the day* kwamba hii riba yote inakuwa inapungua siyo tu kwa Wabunge, lakini kwa kila Mtanzania hapa nchini.

MWENYEKITI: Tunaendelea swali la Mheshimiwa Concheste Leonce Rwamlaza.

Na. 106

Hasara Za Kutumia Mfumo wa Manunuzi Kwa Quotation

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA (K.n.y. MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA) aliuliza:-

Serikali hufanya manunuzi yake kupitia mfumo wa *quotations* ambao bei zake huwa ni za juu kuliko bei halisi.

Je Serikali haioni kuwa inapata hasara kutumia mfumo huo?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM)

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya ununuzi wa umma Sura ya 410 imeainisha njia mbalimbali za ununuzi. Lengo la kutumika kwa taratibu hizo ni kuhakikisha kunakuwa na uwazi na kupata thamani halisi ya fedha. Kati ya taratibu zilizoainishwa ni pamoja na nukuu ya bei (*quotations*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 163 (1) (a) na (b) cha sheria hiyo kimeainisha mazingira ambayo nukuu ya bei inaweza kutumika. Taratibu hizi hutumika kwa kuwashindanisha wazabuni wasio pungua watatu kwa ununuzi wenye thamani ndogo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Saba la kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ununuzi kwa kutumia 'nukuu ya bei kwa sehemu kubwa umesaidia kuongeza ufanisi kwa kupunguza gharama, kupunguza urefu wa mchakato wa ununuzi na kurahisisha upatikanaji wa bidhaa, huduma na kazi za ujenzi.

Aidha, changamoto kubwa tuliyonayo kama Taifa ni uadilifu miongoni mwa watendaji wa Serikali na wazabuni katika utekelezaji wa sheria mbalimbali. Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wa ununuzi wa Umma juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuchukua fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma zimeanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali la tarehe 13 Desemba, 2013. Hivyo ni rai yangu kuwa wadau wa ununuzi wa Umma watazifuata na vile vile kuzitekeleza ipasavyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Nilipenda kujua katika majibu yako ya msingi umesema ununuzi kwa kutumia nukuu ya bei kwa sehemu kubwa umesaidia kuongeza ufanisi na kupunguza gharama . Majibu haya umeyatoa kwa kuzingatia ushauri wa *CAG*?

Katika michango yao Wabunge karibu wote katika Bunge hili tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameonyesha kabisa kutokuridhishwana utaratibu huu wa ununuzi ambao unalingizia Taifa gharama kubwa za manunuzi.

Je, Wizara yako au Serikali haioni ni wakati muafaka sasa wa kuleta sheria mbadala ili kuokoa upotevu wa pesa nyingi zinazotokana na sheria hii ya manunuzi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Msigwa kama ifuatavyo.

Jibu langu limezingatia hata ushauri wa *CAG*. Ninachokuelezea mimi ni juu ya sheria inavyoitaka, sheria inavyoeleza na sisi kama Serikali hii sheria tumeiweka. *Target* yetu kubwa ni kupunguza gharama. Mheshimiwa Msigwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote.

Tatizo kubwa lililokuwepo hapa ni uadilifu wa wafanyakazi, lakini uadilifu wa wale ambao wanatoa tenda yaani wazabuni. Kwa hiyo kisheria kabisa hili tumelieleza katika sheria lakini uwekaji wa sheria ni kitu kimoja lakini utekelezaji na wanaofuata ile sheria ni jambo jingine.

Kwa hiyo, pamoja na majibu yangu nimefuata sheria ambavyo inavyosema lakini vile vile majibu yangu yote yamechukua ushauri vile vile wa *CAG*. Kwa hiyo, hapa tunajibu kutokana na suala ambalo limeulizwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM)]

Lakini kuleta sheria, Mheshimwa Mbunge sheria ambayo nairudia hapa ni sheria ya mwaka 2011 ambazo kanuni zake zimeshatangazwa katika gazeti la Serikali tarehe 13 Desemba, 2013. Sasa ukiniambia nilete sheria nyingine ipi wakati hii iliyokuwepo hatujaitekeleza?

Nadhani naona kama hilo sio la msingi sana. Kwa hivyo umuhimu kwamba sheria tumeshaweka acha tuitekeleze tukiona kuna mapungufu zaidi ya yale yaliyotoka sisi tuko tayari kuleta sheria nyingine au kulfanyia marekebisho (*amendments*). Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali sasa Wizara ya Maji Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu.

Na. 107

Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi Wilayani Moshi Vijijini

MHE. BETTY E. MACHANGU aliuliza:-

Mradi wa maji wa Benki ya Dunia wa vijiji kumi kwa kila Wilaya ulioanza takribani miaka tisa (9) iliyopita bado unasuasua katika Wilaya ya Moshi Vijijini ambapo mpaka sasa ni vijiji viwili tu vya kori Juu na Kori Chini ndio vimepatiwa maji, vijiji vingine vitatu vya Kirima Juu na Kirima Kati boro Serikali inasema imeingia mkataba na Mhandisi Mshauri wakati vijiji vitano vya Tela, Mande, Mawangeni, Matala na Kilimo Makuyuni haviko kabisa kwenye ratiba ya Serikali kupatiwa maji.

(a) Je, kuna sababu gani ya Serikali kutopanga vijiji hivyo katika mradi mpya wa Matokeo Makubwa (*BRN*)?

(b) Je, ni lini vijiji hivyo vitano ambavyo haviko kwenye ratiba ya Serikali vitapatiwa maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na(b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya maji iliyoanza kutekelezwa 2007, ikihusisha mradi wa vijiji kumi (10) katika Halmashauri zote nchini. Utekelezaji wa mradi huo umechukuwa muda mrefu kutokana na taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia kuwa ngeni ambazo zilihusisha Halmashauri kupata vibali mbalimbali kabla ya kuanza ujenzi yaani '*No Objection*'. Kwa sasa Serikali imeondoa taratibu hizo na Halmashauri zimeishajengewa uwezo wa kutosha. Miradi ya maji ya vijiji (10) imeingizwa na inatekelezwa kupitia Mpango wa Tekeleza sasa kwa Matokeo Makubwa yaani (*BRN*).

Serikali imepanga kukamilisha miradi ya maji kwenye vijiji(10) vya kipaumbele kwa kila Halmashauri ikiwemo Halmashauri ya Moshi ifikapo Juni, 2014. Katika Halmashauri ya Wilaya ya moshi vijijini, Serikali inatekeleza miradi ya maji vijiji 10 katika vijiji vya Korini Juu, Korini chini, Kirima juu, Kirima Kati na Boro ambapo ujenzi wa miundombinu ya maji upo katika hatua mbalimbali. Katika vijiji vya Tella, Mande Makami Juu, Makami Chini, Matala, Mwanjeni na Kilimo Mkuyuni ujenzi wa miradi utanza mapema mwezi January, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyote alivyotaja Mheshimiwa Mbunge vya Tela, Mande, Mwanjeni, Matala na Kilimo Makuyuni vipo katika utekelezaji na ifikapo mwezi Juni, 2014 vitakuwa vimekamilika. Halmashauri inashauriwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mikataba ili kufikia miradi kwa kuwasimamia wataalamu Washauri na Wakandarasi kwa mujibu wa mikataba ilikufikia lengo hilo na wananchi wapate huduma ya maji inayotarajiwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machangu:

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya kutekeleza miradi ya vijiji 12 ni takribani bilioni 8, lakini kwa mwaka 2012/2013 mpaka sasa hivi zimepelekwa million 600 tu na katika mkutano uliokuwa umefanyika Morogoro miezi iliyopita Wataalam hao walielekezwa na Wizara kwamba waongeze hivyo Vijiji vifike 20.

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti naomba Serikali ituambie kwa miaka 10 vijiji 10 havikuweza kutekeleza sasa wameongeza vijiji 20, Serikali ituambie wana kauli gani ya fedha za kutekeleza miradi hiyo katika Wilaya ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za maji kwenye maeneo zilipo *either* vijijini au mijini zimeonyesha ufanisi mkubwa katika kusimamia maji ya maeneo walipo na pia kusimamia vyanzo vya maji.

Je, Serikali ni lini itawapa mafunzo wajumbe wa Kamati hizi ili waweze kusimamia maji vizuri zaidi kuliko wanavyofanya sasa hivi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Betty Machangu kama ifuatavyo:-

Naomba nitoe maelezo yafuatayo yanayowathibitisha kwamba miradi hii ya vijiji 10 inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa hvi baada ya kuingiza miradi hii kwenye vijiji kumi ya mpango wa mradi wa Tekeleza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

sasa kwa matokeo makubwa yaani (*BRN*) tayari katika nchi nzima vijiji 193 vinapata maji kwa takwimu za mwezi wa 10 na vijiji 854 miradi yake inajengwa ambayo itakamilika kati ya mwezi wa 2 mpaka mwezi wa 6. Vijiji 491 miradi yake imetangwazwa na itaanza ujenzi mwezi Januari kwa hiyo tuna uhakika kwamba vijiji hivi 10 vitakamilika kabla ya mwezi wa 6 mwaka kesho 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fedha kwamba tumepeleka Milioni 600 tu. Fedha hizi Mheshimiwa Mwenyekiti zinapelekwa kulingana na kazi zilizofanywa. Kama Mkandarasi ametekeleza kazi aina fulani anawasilisha *Certificate*.

Wakati tunapanga Bajeti tunahakikisha kwamba wale ambao kazi zinafanyika ndio wanapewa zile fedha. Kwa masikitiko yangu nataka kueleza kwamba Halmashauri ya Moshi Vijijini ni moja ya halmashauri ambazo hazijafanya kazi yake vizuri. Hivi ninavyoongea ni mradi mmoja tu wa *Collin juu* ambao uko katika asilimia 85. Miradi mingine bado utekelezaji wake unasusua.

Kwa hiyo niwaombe tu kwamba waongeze kasi ya utekelezaji, fedha zipo na watapewa. Katika mwezi huu wa 10 robo ya kwanza tumewapelekea halmashauri hii Milioni 121. Wachukue hizo fedha wazitumie ili waweze kuharakisha miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili Kamati za Maji zinafanya kazi vizuri, zinahitaji mafunzo. Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunatekeleza miradi hii ya Vijiji 10. Mradi kabla hawajakabidhiwa wananchi huwa lazima uwe umeundiwa jumuiya ya watumia maji (*KOUSO*). *KOUSO* hii wakati mradi unatekelezwa wanapewa mafunzo. Kwa hiyo ni kuhimiza tu kwamba miradi yote inapokuwa imekamilika ikabidhiwe kwa *KOUSO* ambazo zimeshapata mafunzo. Lakini kama ni mafunzo ya ziada, Wizara inalichukua italifanyia kazi kuona namna gani tuweze kuwaongezea mafunzo. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwulize Naibu Waziri wa Maji maelezo yake ni mazuri na ikifika hiyo Januari huenda mambo yetu yakawa mazuri.

Lakini kuna ule mradi wa Himo pale Mjini ambao nimehangaika sana na Mtukufu Rais katoa Shilingi Milioni 100 kaja kutoa tena Milioni 50 watu wakaanza kunywa maji. Lakini kuna kitu mmeleta kinaitwa MUWASA kinavuruga wale wananchi, wananchi hawapati maji tena.

Sasa Waziri anaweza kutuhakikishia vipi upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Himo Mjini?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mrema, kama ifuatavyo:-

Nimefanya ziara Mkoa wa Kilimanjaro na moja ya eneo ambalo nilipita ilikuwa ni pale Himo. Pale kuna mradi wa maji ambao tatizo lake kubwa ilikuwa ni usimamizi haukuwa mzuri na hivyo ulikuwa unashindwa kujiendesha. Tulifanya maamuzi kwamba MUWASA ambao ni Mamlaka ya Maji ya Moshi isimamie ili kuona namna gani wale wananchi wanapata maji wakati wote. Mamlaka imeshaanza kusimamia na taarifa nilizonazo wananchi wameshaanza kupata maji na wanalipa vizuri.

Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge Mrema, tushirikiane kuwahamasisha wananchi wa Himo waiunge MUWASA mkono. Niseme tu kwao wananchi wa kwa Himo wana bahati kwa sababu Mamlaka hizi za Maji za Mikoa zinajitegemea na zina uwezo wa kukopa kwenye mabenki. Kwa hiyo hawatashindwa kuendesha huo mradi wa Himo. *(Makofi)*

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii. Vijiji vya Majalilla na Igagala ni miongoni mwa vijiji vilivyopewa nafasi ya kupewa miradi ya maji. Je, ni kwanini mpaka sasa miradi ya vijiji hivi haijapata fedha ni lini Serikali itapeleka fedha hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo:-

Kwanza nimshukuru kwa swali zuri. Naomba nitoe taarifa kwamba mgao wa kwanza, robo ya kwanza ya mwezi wa 7, wa 8 wa 9 umegawiwa mwezi wa 10, na kila halmashauri imeshatumiwa fedha tunaomba Wabunge wafuatilie na tutatoa orodha ya mgao huo ninayo hapa ili kila Mbunge aweze kujua ni kiasi gani kimekwenda kwenye halmashauri yake. Fedha hizi zinahusisha fedha za ndani na fedha za nje. Tumepeleka fedha za ndani Bilioni 86 na fedha za nje Bilioni 75. Jumla Bilioni 161 zimegawiwa kwenye halmashauri kwa miradi ya maji mbalimbali.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mradi wa Kigoma unavyoendelea nilitaka kujua kwa Mheshimiwa Waziri, Mradi wa Maji wa *Lake Tanganyika* ulikuwa unahusisha Vijiji vya Mwandiga pamoja na vijiji vyote vya jirani. Nataka kujua imefikia wapi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kumjibu Mheshimiwa Serukamba kwa swali lake zuri kama ifuatavyo:-

Ni kweli Serikali inatekeleza Mradi wa Maji pale Kigoma Mjini ambao ni miongoni mwa miradi mingine kama wa Lindi, Sumbawanga, Musoma na Bukoba. Hivi ninavyoongea Mkandarasi yupo kazini na Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Kigoma aliutembelea huu mradi na aliona kazi imeshaanza kufanyika. Nina hakika na vijiji alivyovitaja vitanufaika kwenye mradi huu wa maji.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Mwambiti Kata ya Mwamishali Halmashauri ya Meatu ni miongoni mwa vijiji vilivyochangia fedha kwa ajili ya mradi wa maji. Kijiji cha Mwambiti kila kaya ilichangia 23,500/= ili kurahisisha au ku-*facilitate* zile gharama za mwanzo za mradi wa maji.

Je, kwakuwa sasa katika kijiji hiki hakuna uwezekano kabisa wa kupata maji haya, Serikali iko tayari sasa kurudisha fedha za wananchi ambazo walichanga kwa ajili ya mradi huu wa maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Opolukwa Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie majibu yangu kama Mheshimiwa amenielewa vizuri, ni kwamba tunatekeleza miradi ya vijiji 10 ambayo tayari utekelezaji wake sasa hivi unafanyika vikiwemo vijiji vyake vya kule Meatu. Tumesema kwamba sasa hivi kuna miradi 854 maana yake vijiji 854 miradi yake inajengwa, ambayo itakamilika kabla ya mwezi wa sita. Nina hakika na kijiji hiki kipo.

Sasa suala la michango ya wananchi ile michango haikuwa kwa maana ya kuchangia ujenzi, ile michango ni kama baada ya mradi ukikamilika itumike kwa ajili ya kuendesha ule mradi.

Kwa hiyo tuwaombe wananchi wavute subira mradi ukikamilika fedha zao zitunzwe ili zivasaidie mradi baada ya kukamilika waweze kuendesha ule mradi.

Na. 108

Utekelezaji wa Miradi ya Maji Kibaha Mjini

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU (K.n.y. MHE. SILVESTRY F. KOKA) aliuliza:-

Wananchi wa Kibaha walichangia miradi mbalimbali ya maji ya Vijiji kumi chini ya Mpango wa Benki ya Dunia lakini mpaka leo miradi hiyo haijatekelezwa:-

Je Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa mradi huu au mbadala wake unatekelezwa ili wananchi wa Kibaha waweze kupata majisafi na salama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha Mradi wa Vijiji kumi (10) katika Halmashauri zote ikiwemo Halmashauri ya Kibaha Mjini unatekelezwa kwa kasi na kuwapatia wananchi maji, Serikali imeondoa taratibu za upatikanaji wa vibali vya ujenzi wa miradi ya maji vijiji kumi (10) yaani *“No Objection”* na Halmashauri zimekwishajengewa uwezo wa kutosha, hivyo kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Katika Halmashauri ya Kibaha Mjini, ujenzi wa miradi ya maji umekamilika katika Vijiji vya Mwanalughali, Saeni, Zogowale na Jonugha. Kwa vijiji vya Vikawe Shule, Vikawe bondeni na Galagaza ujenzi unaendelea. Vijiji vya Mikongeni, Uyaoni, Misugusugu, Hatua, Visiga, Sagale Sofu, Kidenge na Viziwaziwa vipo katika hatua za kusaini mikataba na Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa upanuzi wa mtambo wa Ruvuma Juu ili kuongeza uwezo wake kutoka uzalishaji wa lita Milioni 82 kwa siku za sasa hadi lita Milioni 196 kwa siku. Upanuzi huo utahusisha ujenzi wa Kitekeo cha maji (*intake*) na ulazaji wa bomba jipya kutoka Mlandizi hadi Dar es Salaam.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa Kibaha iko karibu sana na Mtambo wa Ruvu juu kwanini Serikali isichangamkie sana mradi huu wa kutengeneza maji au kupeleka maji katika vijiji hivi vya Ruvu, vya Kibaha badala ya kufikiria mradi mwingine?

Swali la pili; ni lini Serikali italeta mkakati maalum wa kushughulikia maji kwenye vijiji vyetu vyote hivi nchi nzima vikiwepo vijiji vya kule Wilaya ya Igunga, Kilwa, Dar es Salaam badala ya kutegemea *World Bank* ambao hata fedha zenyewe zinasumbua?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kafumu, Mbunge wa Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mbunge wa Igunga na wananchi wa Dar es Salaam kwamba mradi mkubwa unaojengwa sasa wa kutoa maji Ruvu juu na kuongeza kutoka lita Milioni 82 kwenda 196 vijiji vyote vinavyopitiwa na Bomba hili ikiwemo vijiji vya Kibaha, Mlandizi watapata maji. Kwa hiyo tusebiri tu mradi ukikamilika wananchi wote watapata maji kwenye mradi huo.

Kwamba mkakati maalum wa kushughulikia tatizo hili Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati tayari upo. Tumesema kwamba sasa hivi zipo sekta 6 ikiwemo sekta ya maji ambazo zimeingizwa kwenye *big result now*, na mkakati huu umegawa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

katika miaka mitatu. Ambapo tumesema kwamba mwaka wa kwanza utatoa maji kwa watu Milioni 7,100,000 na mwaka wa pili 7,100,000 tena na mwaka wa tatu Milioni 1,300,000 na hivyo kuongeza upatikanaji wa maji kufikia asilimia 74.

Tumesema kwamba kufikia mwaka kesho mwezi wa 6 baada ya kukamilisha vijiji hivi 10 kila halmashauri ilete mapendekezo ya vijiji 20 mpaka 30 ili tuweze kuanza utekelezaji wake na kuwapatia wananchi maji.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kuona umuhimu wa ujenzi wa mradi wa maji kutoka Njombe kwenda Mbarali kwa maana ya huduma ya Kata ya Ipwani na Mawindi. Ningetaka kujua ni lini utekelezaji wa mradi huu utaanza.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilufi kama ifuatavyo;-

Lakini kwanza nimshukuru sana kwa sababu amekuwa akifuatilia sana mradi huu, lakini kwa mara ya kwanza awamu hii ya nne imeuingiza mradi mkubwa wa kutoa maji toka Njombe na kupeleka Mbarali upo kwenye bajeti ya mwaka huu 2013/2014 na hivi ninavyoongea umeshapewa fedha ili utekelezaji wake uanze.

Tumesema kwamba Wilaya ya Mbarali ndio watangaze kwa sababu wao ndio wana michoro na *design* zote ili utekelezaji uanze mara moja. Naamini Mkurugenzi ananisikia hapa atangaze mara moja, wasaini mkataba ili utekelezaji wake uweze kuanza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali ni nzuri sana lakini naomba Mheshimiwa Naibu Waziri akubali kwamba mradi huu wa kupeleka maji vijiji 10 kwa kila Halmashauri bado una tatizo, kwa sababu kila siku ndani ya Bunge haikosi maswali mawili, swali moja, maswali matatu linalohusu mradi wa vijiji 10 vya maji.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuchukua tatizo hili alirudishe Wizarani wakae watafakari, waangalie usimamizi, ufuatiliaji na upelekaji wa hela ukoje ili maswali haya yapungue hata kwangu kule Iramba Mashariki kero hii ipo. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Ni kweli mradi huu umechukua muda mrefu kama nilivyosema kwenye jibu la msingi la swali ambalo limepita muda sio mrefu. Tumeeleza sababu kwamba ni kwanini ilichukua muda mrefu. Sababu mojawapo kubwa ni kwamba miradi hii ilikuwa inachangiwa na wafadhili mbalimbali ikiwemo Serikali yetu, Ufaransa, Ujerumani na nchi zingine na Benki ya Dunia.

Kwa hiyo, ili kutekeleza miradi hii iliamriwa kwamba taratibu za manunuzi zitumike za Benki ya Dunia. Taratibu hizi zilikuwa zinachukua muda mrefu na zilikuwa na mlolongo ambao wataalam wetu wa halmashauri walikuwa hawana ujuzi wa kuzitekeleza.

Tumesema kwamba zile taratibu sasa hivi kwanza halmashauri zimeshakuwa na uwezo wa kutosha na tumeziona hizo *No objection*. Ndiyo maana sasa hivi unaweza ukaona matokeo kwamba tayari kuna vijiji 193 vimeshakamilika na vijiji 854 vinajengwa na 491

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

vimetangazwa. Nina hakika baada ya vijiji hivi kukamilika mwezi wa 6 kero hii itapungua kwa kiasi kikubwa.

Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli yapo matatizo ya usimamizi ambayo naomba tushirikiane. Nimekwenda pale Singida, nimeona matatizo haya kwenye usimamizi sehemu mbalimbali. Kwa kweli lazima tushirikiane kusimamia ili miradi iweze kutekelezwa.

MHE. MOZA A. SAIDY: Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti naomba swali langu namba 109 lipatiwe majibu.

Na. 109

Mafunzo Maalum ya Polisi Kufanyikia Porini na Kutengewa Fedha Za Posho

MHE. MOZA A. SAID aliuliza:-

Jeshi la polisi limeanzisha mafunzo ya Kisayansi ya Polisi kwa ngazi za Cheti, Diploma na Shahada:-

(a) Je, Kwanini washiriki wa mafunzo haya hawaendi kujifunza stadi za porini ili kujifunza mbinu za kivita na kupambana na majambazi?

(b) Je, kwa nini Serikali haiwapi washiriki fedha za mafunzo wanapokuwa mazoezini ili kuongeza utendaji kazi na kumudu gharama mbalimbali?

(c) Je, ni lini Askari hawa watapewa vyeti vyao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Said, Mbunge wa viti Maalum, lenye sehemu a, b, na c, kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo kwa vitendo au mbinu za medani ni sehemu ya Mitaala ya kozi mbalimbali ikiwemo Sayansi ya Polisi ngazi ya Cheti na Stashahada. Mafunzo haya hufanyika ndani na nje ya mipaka ya Chuo husika kwa muda wa wastani wa wiki mbili hadi nne.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanafunzi wanaohudhuria mafunzo niliyoyaeleza hapo juu hupatiwa huduma zote muhimu ikiwemo malazi, chakula na matibabu wanapokuwa mazoezini. Pia askari hawa huendelea kulipwa mishahara na posho zao kama kawaida. Kwa kuzingatia utaratibu huu Jeshi la Polisi halioni umuhimu wa kutoa posho au malipo ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utaratibu wa kutoa Vyeti kwa wahitimu wa mafunzo mbalimbali ndani ya Jeshi la polisi hutegemea aina ya mafunzo. Kwa wanafunzi wa Sayansi ya Polisi, vyeti hutolewa mara tu baada ya kumaliza mitihani na matokeo yao kuridhiwa na Bodi ya Mafunzo ya Jeshi la Polisi. Mpaka sasa wahitimu wote waliokamilisha taratibu hizo wameshapatiwa vyeti vyao.

MHE. MOZA A. SAIDY: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuuliza tu Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya ziada.

(a) Kwa kuwa mafunzo haya yanafanyika kwa muda mfupi sana huoni haipelekei askari hawa kujua mbinu hizo?

(b) Mafunzo yoyote ni lazima yawe na motisha, mbali na malazi, chakula, matibabu na hali kadhalika ulivyosema. Mheshimiwa Waziri hauoni umuhimu sasa kuwapatia motisha ya fedha askari hawa ili na wengine wawe na moyo wa kuweza kujifunza mafunzo hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

La kwanza anasema kipindi hiki ni kifupi. Ukweli ni kwamba mafunzo haya yanakuwa na mambo mengi lakini wiki nne ndani ya *field* kwa maana ya medani tunahisi kwamba inatosha. Hata hivyo kama kuna wengi wanaofikiri ni muda mfupi tunaweza kuzingatia, tukatafakari na tukaona kama kuna umuhimu wa kuongeza hilo halina tatizo.

Kuhusu motisha ya fedha: Kozi hii askari wanakuwa wanaomba ili waongeze ujuzi wao, lakini ni kozi hii hii ambayo baada ya kumaliza wanaongezewa mshahara. Lakini pia kozi hii inawafanya wawe wana-*qualify* katika sehemu nyingine za kazi wanazofanya.

Kwa hiyo kwa vyovyote kozi hii ni motisha ya kutosha ikiwemo motisha ya kazi kawaida, lakini pia na kuongeza mshahara ambayo ni motisha ya kifedha kama alivyopendekeza.

MHE. DAVID E. SILINDE: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miongoni mwa motisha ambazo sisi kama Bunge Tukufu tulipitisha ni ongezeko la *ration* ambayo ni kutoka shilingi 150,000/= mpaka 225,000/= kwa Polisi wote nchini. Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kufahamu Serikali mpaka sasa utekelezaji wake umefikia wapi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kuna baadhi ya Majeshi yetu yanapata posho ambayo ilitakiwa, na hata wakati mwingine kuna wanafunzi nafikiri kwa siku wanapata elfu 7,500/= Serikali kwa kuona hilo ilipendekeza kwamba na posho ili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

ration allowance iongezeke kwa askari wote. Tatizo lilikuja kwamba wakati tunapanga Bajeti hili halikuwezekana na tukakata *appeal* kwenye Kamati ya Bajeti ya Bunge.

Kwa hiyo Serikali ina nia hiyo na maombi haya yapo Bunge lako likikubali Mwenyekiti basi mwaka ujao wa fedha pengine tunaweza kuona umuhimu wa kuinua na ikatumika kama inavyopendekezwa. *(Makofi)*

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijana waliomaliza JKT wanakuwa wamepata mafunzo ya kijeshi:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwachukua vijana hawa wotee wajunge na Jeshi la Polisi na Magereza ili wajepushe kutumia ujuzi wao katika vitendo vya kihalifu? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la nyondeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Nia ya Serikali ni kwamba wanafunzi wanapomaliza masomo yao hasa ya *High School*, waende JKT. Kwa vyovyote vile miaka inayokuja tutakuwa na idadi kubwa kuliko tuliyo nayo leo. Kwa hiyo, siyo *practical*. Haitawezekana wote wanaomaliza JKT waingie kwenye Taasisi za Polisi. Kama juzi Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi alivyosema, pia haitawezekana kuingia wote jeshini.

Tunachofanya ni kuhakikisha kwamba tunaowachukua katika majeshi haya watokane na waliopata mafunzo ya JKT. Lakini la pili, mafunzo ya JKT tuyaboreshe ili kuwafanya wajajiri wanapotoka kabla hawajapata nafasi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mafunzo ya kisayansi ya Polisi kwa ngazi ya Cheti na Diploma, yanasaidia askari wengi kupanda nyadhifa na vyeo. Lakini vile vile kigezo cha ukatili, unyanyasaji na uuaji; kimekuwa ni kigezo muhimu kinachotumika ndani ya Jeshi la Polisi kupandisha Polisi vyeo:-

Je, ni kwa nini kigezo hicho sasa kinatumika?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taratibu ninazozijua mimi, kigezo cha ukatili hatukitumii katika kupandisha vyeo. Inawezekana ikawa ni ujasiri na ukakamavu, lakini siyo ukatili.

Na. 110

Wizi wa Watoto Wachanga

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni, kumejitokeza uhalifu wa Wizi wa Watoto Wachanga katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati mbalimbali hapa nchini:-

(a) Je, ni sababu gani zinazosababisha kuongezeka kwa tatizo hilo katika miaka ya hivi karibuni?

(b) Je, ni watoto wangapi wameripotiwa kuibiwa kwa utaratibu huu tangu mwaka 2011 hadi Septemba, 2013?

(c) Je, ni Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za Mikoa gani zilizoongoza kwa uhalifu huu na Serikali imechukua hatua gani kukomesha atatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwea Kidawa Hamid Salehe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, matukizo ya Wizi wa Watoto Wachanga yamejitokeza katika maeneo mbalimbali hapa nchini yakiwemo Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali na hata Majumbani. Ziko sababu nyingi zinazosababisha kushamiri kwa matukio haya, zikiwemo athari za kisaikolojia kwa baadhi ya watu wake kwa waume wanaojihisi kuwa na matatizo ya uzazi pamoja imani za kishirikina.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2011 hadi Septemba, 2013 kulikuwa na jumla ya matukio 310 ya Wizi wa Watoto katika nchi nzima kati yao wa kike walioibiwa ni 128 na wa kiume 182. Jumla ya watoto 177 kati ya 310 walioibiwa waliweza kupatikana baadhi yao wakiwa hai na wengine wakiwa wamefariki na watoto 133 hawakuweza kupatikana hadi leo. Aidha, jumla ya watuhumiwa 174 wakiwemo wanaume 101 na wanawake 73 walikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza hapo juu, matukio ya Wizi wa Watoto yanajitokeza sehemu nyingi za nchi yetu. Hata hivyo, takwimu zilizopo kuanzia kipindi cha Januari, 2011 hadi Septemba, 2013 zinaonyesha kuwa Mkoa iliyoongoza ni Dar es Salaam kwa kuwa na jumla matukio 73, ikifuatiwa na Mkoa wa Mara wenye matukio 38 na Mkoa wa Mbeya wenye matukio 23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linachukua hatua mbalimbali kukabiliana na vitendo hivi vya kinyama, kupitia miradi ya Polisi Jamii kama vile ulinzi shirikishi, familia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

yetu haina uhalifu na usalama wa familia. Aidha, Jeshi la Polisi limeanzisha dawati la Jinsia na Watoto kwa lengo la kupambana na ukatili dhidi ya watoto yakiwemo matukio ya Wizi wa Watoto.

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa moja ya sababu zinazowasukuma wanawake kuiba watoto ni kunyanyaswa na kudhalilishwa na kudharauliwa na waume zao kwa kutoweza kuwapatia watoto. Wanaume wao wakijiona ni safi, hawana tatio lolote:-

Je, Serikali iko tayari kutoa elimu kwa wanaume kuwafahamisha kuwa na wao yawezekana kuwa ni chanzo cha kutowapa ujauzito wake zao kwa maana yoyote ile ya kisaikolojia au ya kimaumbile?

Pili, kwa kuwa katika jibu la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna baadhi ya watoto wamepatikana tayari wameshafariki. Je, ni nini hukumu au ni hukumu gani imetolewa kwa hawa wahalifu waliopatikana na watoto wameshakufa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la kwanza katika maswali mawili ya Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe kuhusu kutoa elimu kwa akina baba kuonyesha mapungufu yaliyopo katika uwezekano wa kupata watoto.

Elimu ya uzazi inatolewa katika Vituo vyetu vya Tiba, lakini vile vile kwa kutumia Vyombo vya Habari, elimu hiyo inatolewa. Katika Mpango wa Uzazi Salama na katika Elimu ya Mpango wa Uzazi, tunatoa maelezo kwamba kasoro zinazopelekea mama kutopata mtoto ni zote kwa pamoja, ni kati ya baba na mama kwa pamoja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA AFYA]

Kuna matatizo ambayo yanatokea kwa baba na kuna matatizo ambayo yanatokea kwa mama. Sasa kwa kutumia njia hii, tunaendelea kutoa elimu kwamba kasoro ya kutopata mtoto siyo kasoro ya mama peke yake.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hospitali mbalimbali zimeshachukua hatua za msingi kupambana na uhalifu, wametenga bajeti kwa ajili ya kujenga *fence* katika hospitali zao. Mfano, Hospitali ya Mrara iliyoko Wilaya ya Babati, tumetenga kiasi cha milioni 150 kwa ajili ya kujenga *fence* kupambana na uhalifu.

Napenda kufahamu, Serikali iko tayari kupeleka fedha hizo mapema ili kuzuia uhalifu katika Hospitali yetu ya Mrara?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pauline Gekul kama ilfuatavyo:-

Kama fedha alizosema zimetengwa na zimo kwenye bajeti ya mwaka huu, basi Serikali lengo lake ni kutimiza mahitaji yote ya Bajeti kama ilivyotengwa katika sehemu tofauti. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kusema kwamba hizi pengine zisitoke. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itahakikisha kwamba na hizi na nyingine zitatoka kwa ajili ya utekelezaji.

Na. 111

**Watanzania Waishio Nje ya Nchi Kuunganishwa
na Wawekezaji**

MHE. LETICIA MAGENI NYERERE aliuliza:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LETICIA MAGENI NYERERE]

Baadhi ya wawekezaji wa nje wameshindwa kuelewa utamaduni na mila za nchi yetu na kurudi kwao bila kuwekeza, japokuwa kuna Watanzania wengi waishio nje wangeweza kuwaelimisha wawekezaji hao kabla hawajaingia nchini:-

(a) Je, Serikali huwahusishaje Watanania walioko nje ili waingie ubia na wawekezaji?

(b) Je, ni Watanzania wangapi kutoka Diaspora waliounganishwa na Balozi zetu na mpaka sasa wapo kwenye ubia na wawekezaji nchini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Leticia kwa kujipambanua kama Msemaji, Mtetezi na Balozi mahiri wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi. Baada ya pongezi hizo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kumjibu Mheshimiwa Leticia swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Balozi zake imekuwa ikifanya jitihada za kuwaweka Watanzania waliopo nje ya nchi karibu, kwa kuwahimiza kuunda vikundi au jumuiya. Kwa kupitia umoja huo wa jumuiya hizo, Balozi zetu zimekuwa zikitoa taarifa za fursa za uwekezaji zilizopo nchini.

Aidha, Balozi zetu zimekuwa zikitumia fursa zinazojitokeza pale Viongozi wa Serikali wanaopotembelea nchi mbalimbali kuwakutanisha na Watanzania kwa ajili ya kutoa taarifa na kujadiliana masuala mbalimbali ya kitaifa, ikiwemo masuala ya uwekezaji. Lengo la jitihada zote hizi ni kuwashawishi na kuwahimiza Watanzania waliopo ughaibuni kutumia fursa zilizopo nchini kwa ajili ya kuwekeza wao binafsi au kwa kuingia ubia na wawekezaji kutoka nje.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE]

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu kujua idadi kamili ya Watanzania kutoka Diaspora ambao wameunganishwa na Balozi zetu na mpaka sasa wapo kwenye ubia na wawekezaji hapa nchini.

Serikali inaamini ikuwa kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa za kutoa taarifa za fursa za uwekezaaji zilizopo nchini kwa Watanzania hao, ipo idadi kubwa ya Watanania ambao wamehamasika na hivi sasa wanashirikiana na wawekezaji kutoka nje kuwekea hapa nchini kwa njia mbalimbali, ikiwemo kununua hisa kwenye makampuni ya kigeni yanayowekeza hapa nchini. Serikali itaendelea na jitihada za kutoa taarifa za fursa za uwekezaaji zilizopo nchini kwa Watanzania waliopo nje ya nchi na kuwahimiza Watanania hao kuwaelimisha na pia kushirikiana na wawekezaji kutoka nje katika kuwekeza hapa nchini.

MHE. LETICIA MAGENI NYERERE: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutambua uwezo wangu wa masuala ya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza, naomba niseme nukuu ifuatayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Leticia, muda wetu ni mdogo, tuna maswali zaidi ya 10 yaliyobakia. *Go to your question please.*

MHE. LETICIA MAGENI NYERERE: Nakuelewa Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima nijenge hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Leticia nitakukalisha, muda wetu ni mdogo. Uliza swali la nyongeza kama Kanuni inavyotaka. Haya mengine tutazungumza *canteen* huko.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LETICIA MAGENI NYERERE]

MHE. LETICIA MAGENI NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usemi unaosema kwamba *'in theory there is no difference between theory and practice, but in practice there there is'*. Maana yake ni kwamba, katika nadharia hakuna tofauti, lakini kwenye vitendo tofauti ipo. Swali:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuwashirikisha kwa vitendo Watanzania waishio nchi za nje katika masuala ya uwekezaji kwa ajili ya manufaa ya Taifa letu?

Swali la pili, kwa kuwa Watanzania waishio nje wana uwezo kitaaluma na vile vile wana uwezo kiuchumi. Kwa kuwa kuwanyima haki ya kuwekeza nchini wakati akielewa fika kwamba hawezi kulivaa hilo gauni.

Je, ni kwa namna gani sasa Serikali itatoa vivutio kwa wana *Diaspora* ili waje nchini wawekeze kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kumjibu Mheshimiwa Leticia maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza nikianza na kwamba kama tupo tayari kuwashirikisha kivitendo, tumekuwa tayari, tuko tayari, na tutaendelea kuwa tayari kuwashirikisha Watanzania hao. Zile jitihada ambazo nimesema ambazo za kuwa-*organize* wawe katika vikundi na pia kuwakutanisha na viongozi wakuu wanapotembelea katika nchi hizo. Yale siyo mambo ya kinadharia, ni mambo kivitendo. Katika mikutano hiyo pia tumekuwa tukiwaambia juu ya fursa zilizopo.

Lakini fursa hizo hasa kwa Watanzania walioko nje, zinapatikana katika mitandao ambayo inahusu uwekezaji, na inapambanua ni kwa kiasi gani wao wanaweza kunufaika na kutumia fursa hizo. Kwa hiyo, tuko tayari.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE]

Kuhusu suala la pili la kutumia Watanzania hao au kuwapa fursa hizo kwa sababu wao wana uwezo, wana wasomi. Tunatambua uwezo wao, tunatambua maarifa ambayo wanayapata wakiwa nje. Ndiyo maana karibu viongozi wetu wanapokutana nao, wamekuwa wakiwahimiza na kuwahamishia utaalum na uzoefu huo kuja nao nyumbani. Lakini wakati huo huo pia tunatambua kwamba na Watanzania waliopo nyumbani nao pia wana uwezo wa kutosha.

Na. 112

Mgomo wa Walimu Nchini

MHE. CECILIA DANIEL PARESSO aliuliza:-

Mnamo 2012 kulikuwa na mgomo wa Walimu uliotekelezwa na Walimu nchini wakidai stahili zao mbalimbali:-

Je, mpaka sasa Serikali imeyashughulikiaje matatizo hayo ya Walimu hapa nchini?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Dannel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Walimu Tanzania (CWT) waliitisha mgomo kuishinikiza Serikali kulipa nyongeza ya mishahara ya Walimu kwa asilimia 100%, posho ya kufundishia ya asilimia 55% kwa wanaofundisha masomo ya Sayansi na asilimia 50% kwa wanaofundisha masomo ya Sayansi Jamii, pamoja na posho ya mazingira magumu ya asilimia 30% kwa wanaofanya kazi maeneo yenye mazingira magumu. Kufuatia mgomo huo, mnamo tarehe 2 Agosti, 2012, Serikali ilifungua kesi katika Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi dhidi ya CWT ili kupinga mgomo huo. Baada ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

kusikilmiza kesi hiyo, Mahakama ilitoa hukumu kuwa CWT isitische mgomo huo na kuagiza Serikali na CWT zirudi kwenye meza ya majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na CWT wanaendelea na majadiliano kuhusiana na madai hauyo ya Walimu na tayari vikao vinane (8) vimefanyika. Katika vikao hivyo, Serikali iliahidi kutoa nyongeza ya wastani wa asilimia 14.62% ya vianzia vya mishahara ya Walimu wakati CWT walishuka kutoka asilimia 100% hadi asilimia 53% ya nyongeza waliyokuwa wanadai. Aidha, ahadi ya Serikali ya nyongeza ya vianzia vya mishahara imeanza kutekelezwa Julai, 2013. Pande zote mbili, yaani CWT na Serikali zinaendelea na majadiliano kwa juhudi na kwa nia njema.

Mheshimewa Mwenyekiti, Serikali pia inaendelea kulipa madeni mbalimbali ya Walimu na kuhakiki madai yaliyobaki. Aidha, Serikali imejiwekea mkakati wa kudhibiti uwepo wa madeni mapya ya Walimu na malimbikizo ya madeni kwa kuhakikisha waajiriwa wapya wanaingizwa kwenye orodha ya malipo ya mishahara mara wanapojiriwa, kurekebisha mishahara ya Walimu mara tu wanapopanda madaraja, kudhibiti uhamisho usio na tija pamoja na kutenga Bajeti kwa ajili ya malipo ya stahili mbalimbali za Walimu. *(Makofi)*

MHE. CECILIA DANIEL PARESSO: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Niseme kwamba nasikitika sana kwa majibu haya ya Serikali yasiyokuwa na matumaini kwa Walimu nchini:-

Swali langu la kwanza. Kwa kuwa Walimu waliopandishwa madaraja huendana na marekebisho ya mishahara na kwa kuwa kuna zaidi ya Walimu 30,000 waliopandishwa madaraja bila marekebisho ya mishahara, na hivyo kufanya madai ya shilingi bilioni 30 Serikalini. Je, ni lini Serikali italipa mapunjo haya ya Walimu?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CECILIA D. PARESSO]

Swali la pili, kwa kuwa katika vikao mbalimbali kati ya Serikali na CWT kuhusu nyongeza ya mishahara kwa Walimu nchini katika mwaka huu wa fedha ni kufikia asilimia 50%; Je, Serikali inapata kigugumizi gani kulipa nyongeza hii ya mishahara kwa Walimu nchini?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheahimiwa Paresso kama ifuatavyo:-

La kwanza, ni kuhusu madeni haya ambayo yako sasa hivi yatalipwa lini. Kwanza naomba niseme kwamba Serikali imejipanga kwa nia thabiti ya kuondokana kabisa na kadhia hii ya madeni. Haimfaidii Mwalimu wala haiifaidii Serikali wala haimfaidii mwananchi yeyote.

Kwa hivyo, kazi ambayo tunaifanya sasa hivi ni ya kuhakikisha kwamba madeni haya tunayaondosha, na zoezi linaloendelea hivi sasa ni uhakiki wa madeni hayo Serikalini, lakini kwa ushiriki kamilifu wa CWT. Ili madeni hayo, tunasema madeni yajulikane na Serikali, lakini yajulikane pia na Chama cha Walimu Tanzania. Niwashukuru sana, niushukuru uongozi wa CWT kwa kushiriki kikamilifu katika zoezi hili. Nina uhakika kwamba tutakapokuwa tumelikamilisha kulipa pesa ndani ya mwaka huu wa fedha, itakuwa ni kwa maridhiano ya pande zote mbili bila ya mgogoro wowote.

Waendeleo kufanya kazi hivyo, kama mnavyowaona Chama kimepanga vizuri kufanya kazi na Serikali bila malumbano na ndicho kitu ambacho tunakifanya hivi sasa.

Kwa swali la pili, la Mheshimiwa Paresso kwamba kwa nini CWT imeteremka katika madai yake mpaka asilimia 53, kwa nini Serikali basi isilipe tu hiyo asilimia 53 na kumaliza zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba madai ya walimu kwa kima ambacho CWT ilikihitaji ni madai makubwa sana yanazidi bajeti au *bill* ya mishahara ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

watumishi wote wa umma. Kwa hivyo, hakukuwa na namna ambavyo lingeweza kulipwa. Lakini madai yale pia yanakwenda kwenye trilioni 5 na kitu. Ni zaidi ya asilimia 50 ya mapato ya ndani ya Serikali, hakuna njia ambayo Serikali inaweza ikalipa, na ndiyo maana Serikali ilibidi ifanye majadiliano.

Lakini kilichowezezana tangu madai haya yametolewa, Serikali kila mwaka ilikuwa inaongeza mishahara ya walimu na kwa sasa tunatathmini kwamba nyongeza ambayo mpaka hivi sasa imehafanyika ni karibu asilimia 30.9 ya mishahara. Lakini kipengele majadiliano kinasema kwamba kama hakumaliza majadiliano katika mwaka husika basi mnaanza upya.

Kwa hiyo, yale yaliyopita haya hesabiwi, yana hesabiwa mwaka huu tunatoa kiwango gani? Kwa hiyo, kama tukifuata mpaka sasa Serikali imetoa kiasi gani sehemu iliyobaki katika madai ya walimu ya nyongeza ingekuwa ndogo sana. Lakini tunajitahidi kuongea kama nilivyosema mwanzo katika jibu langu la msingi kwamba tunazungumza kwa nia safi, kwa juhudi ili tuondokane na kadhia hii.

MWENYEKITI: Nakushukuru. Waheshimiwa Wabunge yamebakia maswali nane muda ni nusu tu. Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar

Na. 113

Vyuo vya Ufundi – VETA Nchini

MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y.MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR) aliuliza:-

Ili Taifa lolote lipate maendeleo ya haraka jamii husika lazima ipatiwe elimu kulingana na mazingira yake:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RICHARD M. NDASSA]

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Shule za Ufundi VETA ili vijana wengi wapate elimu ya kuwawezesha kujiajiri Jimboni Nyang'wale?

(b) Je, ni lini mazingira ya kufundishia walimu yataboreshwa?

(c) Je, Serikali imejipanga vipi kutatua matatizo yanayowakabili walimu kama vile makazi mazuri, maslahi bora?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'wale lenye sehemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nyang'wale ipo katika MKoa Mpya wa Geita na kwa kuwa Mkoa huo upo katika mpango wa kujengewa Chuo kipya cha Ufundi Stadi cha Mkoa kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015, namshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Nyang'wale wawe na subira wakati Chuo cha Mkoa kinaendelea kujengwa.

Aidha, kwa sasa nawashauri wananchi wa Wilaya ya Nyang'wale watumie Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa na Wilaya jirani kupata mafunzo ya ufundi stadi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ni suala endelevu. Kwa sasa Serikali kupitia Mipango ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (*MMEM*) na Sekondari, (*MMES*) inaendelea na uboreshaji shule mazingira na kujenga na kukarabati miundombinu ya shule pamoja na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya maabara, vyumba vya madarasa, vyo na miundombinu ya maji na umeme katika shule 1,200 za sekondari.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, kasi ya uboreshaji wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia inatarajiwa kuongezeka kupitia "Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa" uliozinduliwa mapema mwaka huu 2013.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Serikali ni kuboresha maslahi ya walimu mwaka hadi mwaka kwa kadri bajeti inavyoruhusu. Aidha, kuhusu makazi Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba za walimu kupitia Mipango ya Maendeleo ya *MMEM* na *MMES*. Kupitia Awamu ya Pili ya *MMEM* Serikali imejenga jumla ya nyumba za walimu 7,758 na kupitia *MMES* Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba 500 katika shule za sekondari.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimwuliza maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa sababu Vyuo vya *VETA* Waheshimiwa Wabunge ni vitu vya msingi sana. Ni lini sasa Mheshimiwa Waziri utaleta orodha ya Mpango kwa kila Wilaya maeneo ambayo hayana Vyuo vya *VETA* ili Waheshimiwa Wabunge wajue kwamba mwaka huu Chuo cha *VETA* kwangu kitajengwa ili kupunguza maswali?

Lakini la pili, kwa sababu ipo ahadi leo ni mwaka saba wa kujenga Chuo cha *VETA* pale Wilaya ya Kwimba. Ni lini sasa wananchi wa Kwimba wategeme ujenzi wa Chuo cha *VETA*?

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusu orodha ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi Nchini Wilaya kwa Wilaya kama Mpango wa Serikali ulivyoainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba nakubali ombi hili la kuwasilisha orodha hiyo Bungeni ili igawiwe kwa Wabunge kila Mheshimiwa Mbunge afahamu na nitajitahidi kufanya hivyo hata kabla ya Bunge hili kumalizika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

La pili, kuhusu Chuo cha Kwimba kwamba kitajengwa lini? Naomba radhi tu kwamba Chuo cha Kwimba sikukiangalia, ingekuwa swali la msingi ningeweza kukiangalia kipo katika awamu ya ngapi?

Lakini vile ambavyo sasa hivi tumevitengea fedha katika mwaka huu wa fedha vipo vitano, na kimoja ni kile cha Kilindi au Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga Ludewa kule Njombe, Chunya kule Mbeya na Namtumbo, Ruvuma na Ukerewe Mwanza, hivi tayari tumeishavitengea fedha na vipo katika mchakato na vingine tutavitafutia pesa kwa ajili ya kuweza kujengwa.

Hivi sasa pia tumeomba mkopo kutoka *African Development Bank* na tumepata mkopo wa jumla wa dollar za Kimarekani milioni 51.9 ama kwa shilingi za Kitanzania bilioni 83 hizo tutazitumia kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi vya Mikoa kwa Mikoa ile mipya minne nchini kwetu.

MWENYEKITI: Nakushukuru umejibu vizuri kuliko maswali mengine yote. Tunaendelea na swali la Wizara ya Afya na Stawi wa Jamii Mheshimiwa Al-Shymaa kwa niaba yake Mheshimiwa Martha Mlata.

Na. 114

Gharama Za Matibabu Kwa Watu Wenye Ulemavu

MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR) aliuliza:-

Familia nyingi zenye watoto wenye ulemavu ni zile zilizokuwa na hali duni kifedha hivyo kuwawia vigumu kulipia mahitaji muhimu kwa ukamilifu hususan elimu, matibabu, na kadhalika:-

Je, Serikali ina mikakati gani wa kuwasamehe kulipa gharama za matibabu watu wenye uelemavu pale inapobidi?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shyamaa John Kwegyir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Al-Shyamaa, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulemavu ni hali inayotokana na dosari mwilini auna akilini ambayo inasababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida angetegemewa kuyaweza na hivyo kumletea mtu huyo kizuizi katika utekelezaji wa majukumu yake katika jamii. Kizuizi katika utendaji unatokana pia na mfumo wa matizamo wa jamii dhidi ya mtu mwenye ulemavu.

Katika jamii yetu na kwingineko duniani, hali ya mtu kuwa na ulemavu inaambatana na unyanyapaa unaotokana na mila zilizopitwa na wakati. Kutokana na hali hii, Watu Wenye Ulemavu wanaonekana kuwa ni tegemezi, wasiojiweza na wanaostahili kusaidiwa na watu wasio na ulemavu katika kumudu maisha yao. Mtizamo huu sio sahihi na unakwenda kinyume na haki za kimsingi za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shyamaa John Kwegyir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua adha wanayoipata watu wasio kuwa na uwezo katika kulipia gharama za matibabu. Kwa kutambua hilo Wizara yangu imefanya juhudi za makusudi kwa kutoa mwongozo wa utoaji wa msamaha wa matibabu kwa watu wasiokuwa na uwezo, Wizara ilikwisha ziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwasilisha takwimu za watu wenye ulemavu na wazee wasiojiweza wanaopatiwa msamaha wa huduma za matibabu kupitia zahanati na hospitali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

Kwa kutambua mahitaji ya watu wenye ulemavu, katika mwaka huu wa fedha, Serikali inakusudikuanzisha Mfuko wa Taifa wa kushughulikia mahitaji ya kiuchumi, kielimu afya na mafunzo ya ufundi ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuundwa kwa Mfuko huo ni mwanzo mzuri utakaofungua milango kwa wadau wengine kuchangia. Aidha, mfuko huo utaanza kutengewa fedha katika Bajeti ya Serikali ili kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kupata fedha kwa ajili ya ujasirimali, kama ilivyo kwa Mfuko wa Wanawake na Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inafanya mapito ya mfumo wa ukusanyaji takwimu ujulikanao kama MTUHA, ili tuweze kuwa mana mfumo wa kieletroniki ambao utakuwa na uwezo mpana zaidi wa kukusanya takwimu na kuwezesha kutambua wanaopata misamaha na kuweka utaratibu wa kuwezesha vituo hivyo kuendelea kutoa huduma hizo kwa wanawake wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka 5, watu wenye ulemavu, wazee wale wasio na uwezo.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nipongeze tu kwamba Serikali inakusudia kuanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu kupata mafunzo pamoja na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu anisaidie kwamba kama alivyosema nchi zingine walemavu wamekuwa wakipewa kipaumbele sana. Sasa hapa Tanzania wanapofika kwenye huduma zetu za Vituo vya Afya.

Kwanza, hata ule binadamu wa kuona kwamba huyu mtu ni mlemavu apewe hata kipaumbele cha kumwona tu Daktari unakuta mtu ni mlemavu, lakini anawekwa kwenye foleni kuanzia mpaka muda ambapo wengine watamalizika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARTHA M. MLATA]

Je, yupo tayari kutoa agizo kwamba watu wenye ulemavu wapewe kipaumbele kwa ajili ya kuwaona Madaktari bila kukaa kwenye foleni? Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Lakini jambo la pili, sielewi atatusaidiaje sisi Wabunge kwa sababu unapofika kwenye hospitali au Zahanati zetu, unakuta ni kweli anaweza akamwona Daktari bure, lakini inapofika kwenye kuchukua dawa, dawa hakuna; na kwa kuwa *MSD* wanapopeleka dawa, dawa zinaibiwa, zinaonekana kwenye famasia zote na hivyo kuelekezwa wakanunue kule. Ni nini Serikali inatamka kuhusu huduma hiyo kwa watu wenye ulemavu? Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, *short and clear.*

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo lipo kwa kawaida tu na ni desturi ya Madaktari na watoa huduma wote wenye uadilifu mzuri kutoa kipaumbele kwa wale wenye hali mbaya katika ugonjwa au wale wazee au wajawazito au wale wenye ulemavu. Kutokana na hili naagiza tu utendaji katika vituo vyote vya tiba hapa nchini waweze kuzingatia maadili mazuri ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli dawa zinakuwa na matatizo ya kupatikana katika baadhi vituo vyetu, na katika hili ndiyo sababu tunahimiza kuweza kujiunga Mifuko ile ya Bima ili tuongeze mapato yetu katika vituo na fedha hizo ziweze kutumika katika kuviwezesha vituo vyetu kupata dawa.

Lakini katika suala la wizi kama tulivyotoa kwenye taarifa yetu ya awali kwamba hivi sasa *MSD* imeanza kuagiza dawa, vidonge vyenyewe vinachapisho la *GOT* kwenye vile vidonge. Kwa hiyo, tukivikuta vile vidonge katika maduka ya dawa binafsi itakuwa nyepesi zaidi kumkamata huyo mtu na kumzuia kufanya biashara ya kuuza ya dawa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge mtaniwia radhi muda wetu ni mdogo sana tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Hussein Mponda na kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Nkya.

Na. 116

Ujenzi wa Barabara ya Mikumi-Lupia-Kilosa Mpepo-Londo-Lumecha (T.16) kwa kiwango cha Lami

MHE. DKT. HAJI HUSSEIN MPONDA aliuliza:-

Serikali imeahidi kufungua Barabara ya Mikumi – Mahenge - Kilosa kwa Mpepo - Londo (*T16*) katika sehemu ya barabara yenye urefu wa kilomita 40 ambayo inaunganisha Mikoa ya Morogoro na Ruvuma:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa kipande hicho kilichobakia utakamilika ili barabara hiyo ianze kutumika kwa kuwaunganisha wakazi wa Mikoa hii miwili?

(b) Je, ni lini kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara hiyo (*T16*) kwa kiwango cha lami utaanza na kukamilika?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Haji Hussein Ponda, Mbunge wa Ulanga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianza utekelezaji wa kufungua barabara ya Mikumi –Mahenge - Kilosa kwa Mpepo -Londo – Lumecha (*T16*) kwa sehemu iliyokuwa hajafunguliwa ya Malinyi - Kilosa kwa Mpepo – Londo – Kitanda (km 238) katika mwaka wa fedha 2005/2006. Hadi sasa barabara imefunguliwa kwa urefu wa kilometa 184 kati ya kilomita 238 zinazotakiwa kufunguliwa. Serikali itakamilisha ufunguaji wa sehemu ya barabara

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

iliyobakia yenye urefu wa (km 54)katika mwaka wa fedha 2013/2014 kwa kutumia fedha zilizotengwa kwenye Bajeti ambazo ni shilingi milioni 250.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianza utaratibu wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kidatu – Lupiro – Kilosa kwa Mpepo – Londo Lumecha (km. 512) kwa kiwango cha lami kwa kutangaza zabuni tarehe 30 Januari, 2012. Hata hivyo, kukamilika kwa hatua ya kumpata Mhandisi Mshauri kumechelewa sana kwa sababu Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) ambayo ndio wanatusaidia kulipia gharama za usanifu imechelewa kutoa *no objection* ili Mkataba utiwe saini. Inategemewa kuwa *no objection* itapatikana mwezi huu wa Desemba, 2013 na kazi hiyo itaanza mara moja. Kazi hii inatarajiwa kukamilika katika muda wa miezi 24.

MHE. DKT. HAJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya yongeza.

La kwanza, Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza moja kwa moja swali lile (a) kwamba ni lini ujenzi wa kipande kile cha kilomita 54 utaanza. Katika Bajeti ya mwaka huu tumepitisha, tutenga milioni 400 kwa ajili ya kumaliza hicho kipande. Sasa zaidi ya miezi sita karibu inafika, lakini mpaka leo hakuna jibu la uhakika swali ambalo nimeliuliza. Kwa hiyo, nipo pale pale ni lini kazi hii itaanza kuunganisha kile kipande cha kilomita 54 ili tukutane na watani zetu wa Namtumbo?

La pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hadithi ya upembuzi yakinifu toka mwaka juzi tulianza nayo. Sasa Mheshimiwa Waziri anieleze tu, ni Kampuni gani ambayo waliipendekeza na wakapata hiyo *no objection*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba hicho kipande cha kilomita 54 kimewekewa fedha kwenye ya mwaka huu 2013/2014 na mwaka wa fedha unaanzia Julai, mpaka Juni.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi. Tumeishaahidi kipande hicho tutakifungua mwaka huu na fedha tumeziweka kwenye Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, hadithi ya upembuzi yakinifu ni kweli hadithi ya upembuzi yakinifu ni msingi ili kuweza kufanya tathmini ya barabara ambayo tunataka kujenga kwa kiwango lami.

Kama anavyofahamu Mbunge kwamba barabara hizi zinaigharimu Serikali fedha nyingi lazima tujue mahitaji ya barabara hizi, tujue mizigo ya aina gani ipita ili kusudi tufanye usanifu wa kina na kuweza kujua gharama za barabara hiyo.

Wafadhili wa barabara hii wa *African Development Bank* na kama unavyofahamu ni barabara ya kilomita 512 ni barabara ndefu. Kwa hiyo, kwa kweli ni lazima tufuate *procedure* wanayoitaka. Siwezi kusema jina la Kampuni ambayo ilipendekezwa, lakini Mheshimiwa Mbunge bado naweza nikapata hizo data zaidi kwamba ni kampuni ipi imependekezwa kamaitasaidia kwa kuweza kuwaeleza wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa tuendeleo na swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala kwa niaba Mheshimiwa Juma Nkamia.

Na. 115

Barabara ya Uhuru Jijini Dar es Salaam

MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU aliuliza:-

Barabara ya Uhuru mkoa wa Dar es salaam iko katika hali mbaya sana hivyo kusababisha msongamano mkubwa wa magari:

Je, kwa nini Serikali haitoi kipaumbele kwa barabara hii kwa kuitengea fedha ili iweze kutengenezwa?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, mbunge wa Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ilitumia jumla ya shilingi bilioni 1.325 za Mfuko wa Barabara kufanya matengenezo maalum katika barabara ya Uhuru. Aidha katika mwaka huu wa fedha 2013/2014 shilingi milioni mia tano (500) kutoka Mfuko wa Barabara na shilingi milioni mia nne na saba (407) fedha za maendeleo zimetengwa kwa ajili ya matenenezo maalum na za sehemu korofi. Zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi zimetangazwa upya tarehe 28 – 29 Oktoba, 2013 baada ya uchambuzi wa zabuni za awali kushindwa kutoa Mkandarasi anayefaa kwa kazi za matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kua, pamoja na matengenezo inayopata barabara hii kuwa njia nne umekamilika. Serikali kwa sasa inatafuata fedha kwa ajili ya kutekeleza maradi huu uanaolenga kupunguza msongamano wa magari katika Jijini la Dar es Salaam.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru nina maswali mawili tu madogo ya nyongeza.

(a) Fedha anazoitaja hapa Mheshimiwa Naibu Waziri ni nyingi sana na sote tunapita barabara hii labda yeye huwaapiti. Yupo tayari kuongozana na Mbunge wa Ilala akaonyeshe hizi fedha zilivyotumika kutengeneza barabara hii?

(b) barabara hii ina historia kubwa sana ya uhuru wa Taifa letu na kuitelekeza ni sawasawa na kupuuza siku ya uhuru wenyewe.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuwa makini kuhakikisha kwamba barabara hii inaendana sambamba na siku ya kumbukumbu ya uhuru wenyewe wa Taifa letu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu. Ile ya kwanza aliyotuletea alisema tutakwenda hata kesho.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nkamia kama ifuatavyo:-

(a) Sioni tatizokuongozana na Mheshimiwa Mbunge nikamuonyeshe kazi ambazo zimefanyika.

(b) Katika swali la pili, Mheshimiwa anasema tuwe makini na mimi nakubali kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni makini na ndiyo maana tumeshaamua barabara ile kuipanua na kuwa njia nne ili kuweza kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar-es-salaam. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea swali la Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila.

Na. 117

**Kutengeneza Barabara a Vijijini Ili Kuepusha
Vifo Vya Uzazi**

MHE. ROSWEETER FAUSTIN KASIKILA aliuliza:-

Ili kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi mikakati ya kutosha inahitajika ikiwa ni pamoja na kuwa wa barabara zinazopitia kirahisi huko vijijini.

Je, Serikali ina makakati gani endelevu wa kutengeneza barabara kutoka Sitalike kwenda Kilyamatundu na daraja la Momba ili wazazi wafike salama katika Vituo vya Afya?

WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Sitalike hadi Kilyamatundu ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa barabara (*TANROADS*) ikiunganisha mkoa ya Katavi na Rukwa. Barabara hii ina jumla ya urefu wa km 310.26 ambapo km 131.78 mkoa wa Katavi na km. 178. 48 ziko Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi milioni 2,080 zilitengwa na kutumika kwa matengenezo ya barabara hii. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya shilingi milioni 3,732 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetenga pia shilingi milioni 2, 290 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daaja la Momba. Usanifu wa awali kwa ujenzi wa daraja hilo umekamilika na sasa Mhandisi Mshauri anaendelea na usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za Zabuni. Mara baada ya usanifu wa kina kukamilika utaratibu wa kumpata makandarasi wa kujenga daraja hilo utaanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa matengenezo ya barabara hii ili kuhakikisha kwamba inapatikana vizuti majira yote.

MHE. ROSWEETER FAUSTIN KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nakushukuru kwasababu barabara hii ya Stahalike mpaka Nyamatundu inashughulikiwa lakini kasi yake ni ndogo sana. Kwa sababu kasi yake ni ndogo ni kwa vile mgao wa fedha wa Mfuko wa barabara *TANROAD* wanapewa asilimia sabini lakini Halmashauri zinapewa asilimia thelathini tu. Katika asilimia thelathini utakuta matengenezo ya kwa ajili ya barabara za vijijini ni chini ya asilimia kumi.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda muafaka kuziongezea Halmashauri mgao ili angalau kufikia asilimia arubaini ili barabara hizi za vijijini ziweze kutengenezwa kwa kasi zaidi ili wajawazito waweze kufikia zahanati na vituo vya afya, bila misukosuko na kwa haraka zaidi?

Je, Serikali haioni kwamba barabara za vijijini na hasa ile ya Kasanga, Samazi, Muzi mpaka Kipanga zikitengenezwa kwa haraka basi wakulima wanaweza kusafirisha mazao yao kwa wingi na kwa haraka ili wainue kipato chao?

Lakini bila kuwasahau wavuvi wa ziwa Tanganyika na ziwa Rukwa? Ahsante sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza tunazipokea shukurani zake na pia nampongeza na yeye kwa kufuatilia matengenezo ya barabara hii. Sasa katika swali la uwiano wa mgao wa fedha za Mfuko wa Barabara kwa asilimia thelathini na sabini. Nikukumbushe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili lipo kwenye Sheria.

Wakati ule tulijadili na tukaona kwamba umuhimu kwamba barabara hizi kuu, barabara za Mikoa na barabara kuu zinahitaji fedha nyingi zaidi kwa sababu ya ukubwa wa barabara zenyewe, na mizigo inayopita kwenye bara zile. Barabara za vijijini ni barabara ambazo ni ndogo na ni unategemea kwamba ni magari machache yanayopita katika barabara zile.

Lakini kama bado kuna haja ya kujadili tena uwiano suala hili tunaweza tukaendelea kulijadili na tukaona kama tutabadilisha Sheria ile.

(b) Katika swali lake la pili nakubaliana naye kwamba ni kweli barabara za vijijini ni muhimu kwasababu hata huo mzigo unaohitaji kupeleka kwenye barabara kuu na za Mikoa lazima utoke vijijini. Serikali itaendelea kuboresha na kujenga barabara za vijijini ili ziweze kupitika na kutoa mazao ya wananchi na wananchi kuweza kuongeza thamani ya mazao yao waweze kupata fedha zaidi kwa maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru tunaendelea swali sasa la Mheshimiwa Rose Kamil Sukum.

Na. 118.

Mpango Wa Umeme Vijijini

MHE. ROSE K. SUKUM aliuliza:-

Mpango wa umeme vijijini upo katika Mpango wa Serikali wa miaka mitano (5); maeneo ya Miji midogo kama vile Endasiwold, Gendabi na Masqaroda ambayo tayari yamewasilisha maombi yao kwa *TANESCO* bado hayajafikishiwa umeme licha ya nguzo kufikishwa kwenye Mji wa Masqarod:-

Je, ni lini Miji hiyo itafikishiwa umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum kama, ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *REA* na *TANESCO* inaendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika maeneo ya vijijini kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Serikali wa Maendeleo wa miaka mitano (5).

Hii imedhihirishwa kwa kukamilika kwa baadhi ya miradi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ikiwemo mradi wa kupeleka umeme katika Mji mdogo wa Masqaroda. Utekelezaji wa mradi huo ulianza mwisho wa mwaka 2012 na kukamilika rasmi manamo tarehe 16 Aprili, 2013. Mradi huu uliharimu kiasi cha Shilingi milioni 30.8.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilisha mradi huo mwezi Aprili, 2013 kasi ya maombi uya umeme kutoka kwa wateja hairidhishi. Napenda kutumia nafasi hii kumwomba mheshimiwa Mbuinge pamoja na wananchi wa maeneo ya mradi kutumia fursa iliyopo kuwasilisha maombi ya kufungiwa umeme kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI (MHE. G. B. SIMBACHAWENE)]

Mheshimiwa Spika, tathimini ya gharama ya mradi wa kupeleka umeme vijiji vya Endasiwold na Gendabi imeishafanyika, amabpo jumla ya Shilingi 227,038,043 zinahitajika kwa ajili ya:-

(i) Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 4;

(ii) Ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 4;

(iii) Ufungaji wa transfoma mbili (2) zenye uwezo wa KVA 50 na 100; na

(iv) Kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 135. Mradi huu upo katika orodha ya miradi itakayotekelezwa na *TANESCO*.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri nilikuomba naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Wenzetu wa *TANESCO* wanaleta urasimu mkubwa sana Wilaya ya Hanang kwa maana ya kwamba hawa ambao wamefungiwa au waliopeleka maombi yao wanawaaambia kwamba walipie nguzo.

(a) Je, huu utaratibu wa utekelezaji wa Miradi ya maendeleo kupitia *REA* na *TanESCO* wananchi vijijini wanalipia hizo nguzo?

(b) Je, kwa upande wa vijiji vingine vya Endashiog, Gendabi, Simbai, Hilbadau na Gehandu ni lini watapata huo umeme na fedha ni lini zitapelekwa kwa ajili ya utekelezaji huo?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rose Sukum, kama ifuatavyo:-

Nichukue nafasi hii kupitia swali la Mheshimiwa Mbunge kuwaagiza *TANESCO* kwamba lugha wanayoitumia kwamza haistahili na haipo hata katika misamiati ya kuhudumia Wateja. Wateja wanahudumia kupitia umbali uliopo kutoka kwenye nyumba ya Mteja na mahali ambapo umeme unaishia. Wala sio kwa idadi ya nguzo. Bei ya umeme kuingizwa kwenye nyumba ndani ya mita thelathini ni shilingi laki moja na elfu sabini na saba kwa vijijini.

Nichukue nafasi hii kuwaagiza *TANESCO* kwamba wahikikishe wanahudumia wateja wao vizuri na wasitumie lugha hiyo ya kuwataka wateja walipie nguzo, nguzo ni nini, mbona hatuzungumzii habari ya waya? mbona hatuzungumzii habari ya vikombe? Kwa hiyo nichukue nafasi hii nitumie swali lako kuagiza nchi nzima *TANESCO* wasitumie lugha hiyo.

La pili vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge kikiwepo cha Gilbada, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane tuone nini tatizo na kama kuna kitu cha kufanya tuone tutawezaje kuwahudumia Wateja wetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tuendeleo na swali la mwisho, la Mheshimiwa Stephen Ngonyani, kwa niaba ya Mheshimiwa Maige.

Na. 119

Wachimbaji Wadogo Kupatiwa Maeneo

MHE. EZEKIEL M. MAIGE (K.n.y. MHE. STEPHEN HILARY NGONYANI aliuliza:-

Wachimbaji wadogo wadogo wa madini katika Kata ya Mashewa sehemu ya Kalalani na Kigwasi wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa kwa kupigwa na kunyanyaswa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maeneo ya kudumu wachimbaji hao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapokonya maeneo ya kudumu wachimbaji wasioyaendeleza na kuwapatia wachimbaji wadogo?

(c) Je, Serikali ipo tayari kuwalipa fidia wale wachimbaji waliokuwa wananyanyaswa?

WAZIRI WA NISHARTI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, lenye sehemu (a) na (b) (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo ya uchimbaji mdogo hupatikana kwa:-

(i) kutenga maeneo yalioachwa na watafutaji wakuba wa madini (*relinquished areas*) wakati wa kuhuisha leseni kwa mujibu wa kifungu Na. 15 (2) cha Sheria ya Madini Mwaka 2010. Maeneo haya yakishapatikana huyafanyiwa tathimini na kutengwa kwa ajili wadogo; na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NISHARTI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)]

(ii) Kupata maeneo baada ya leseni ambazo hazitimizi masharti ya Sheia ya Madini ya Mwaka 2010 kufutwa. Ombi la Mhe. Mbunge la wachimbaji wadogo wa Kalalani na kigwasi kupata maeneo zaidi ya kuchimba madini linafanyiwa kazi kwa utaratibu huu nilioueleza.

Aidha, Wilaya ya Korogwe tayari ina leseni za wachimbaji wadogo zaidi ya 223 kwa ajili ya kuchimba madini mbalimbali ya vito, nyingi zikiwa katika maeneo ya kigwasi, Kalalani na Daluni.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imefuta leseni za utafutaji mkubwa zipatazo 293 hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2013 kutokana na kutotimiza masharti ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kama nilivyokwishaeleza hapo juu. Zoezi hili linaendelea ili eneo yasikaliwe bila kuendelezwa.

Aidha, zoezi hili si kwa watafutaji na wachimbaji wakubwa pekee, bali hata kwa wachimbaji wadogo ambao hawaendelezi maeneo yao.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria za nchi, hairuhusiwi mwananchi au mtu yeyote kumnyanyasa mwananchi mwingine au kuchukua sheria mkononi. Vitendo kama hivyo ambavyo wachimbaji wa Kalalani na Kigwasi wanafanyiwa havikubaliki hata kidogo. Inabidi sheria ichukwe mkondo wake. Si sahihi mwananchi yeyote kupigwa halafu apewe fidia na yule ambaye ana uwezo wa kumpatia fidia.

Wito wangu kwa wachimbaji wadogo wa Kalalani na Kigwasi nasehemu nyingine nchini ni kuhakikisha kuwa hawavunji sheria kwa kuendesha uchimbaji katika maeneo ambayo si yao kisheria. Sote tuajua kuwa kufanya hivyo ni kuvunja sheria.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo limekuwa ni tatizo kubwa kwasababu mengi yamechukuliwa na makampuni makubwa na mtuhumiwa namba moja kwenye eneo hili ni makampuni makubwa hasa *ABG* pamoja na *Geita Gold Mine*. Lakini kwa taarifa zao za karibuni wanasema kutokana na mdororo wa bei ya dhahabu kwasasa wameamua kupunguza *exploration works* zao na hivyo wameachia baadhi ya maeneo.

(i) Je, Waziri anaweza akatuambia maeneo ambayo sasa *ABG* imeachia ili Serikali iweze kuyagawa kwa wachimbaji wadogo wadogo?

(ii) Kwa kuwa yamekuwepo maombi Wizarani kwa muda mrefu ya kuiomba Serikali irasimamishe maeneo ya Mazimba, Nyangalata pamoja na Masabi katika Jimbo la Msalala ili yawe rasmi ya wachimbaji wadogo wadogo badala ya kuwa wanagombana na wachimbaji wakubwa.

Je, Serikali imefikia wapi na maombi hayo?

NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba maeneo mengi ya nchi yetu yameshikiliwa na leseni za uchimbaji mkubwa kwa maana ya utafiti na wachimbaji wadogo. Serikali inapata tabu kupata maeneo mapya ya kuchimba na kuyatenga kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NISHARTI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)]

Kazi kubwa tunayoifanya ni kuhakikisha kwamba maeneo haya yote ambayo yameshikiliwa na leseni ambazo hazifanyiwi kazi kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, tunayachukua na tunayafanyia tathimini ya kuyagawa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *ABG* na *GGM* kwa pamoja na Serikali tunaendesha Mradi wa pamoja wa kuhakikisha kwamba tunawasaidia wachimbaji wadogo kwa kutenga maeneo haya ya kuchimba pamoja na kuwapa mafunzo, kuwapa vifaa na teknolojia ya kuchimba vizuri.

Tumeteuwa maeneo mawili ikiwa eneo la Geita Mkoa wa Geita pamoja na Mkoa wa Mara kwa maana ya eneo la Tarime kama ni maeneo ya mfano kwa zoezi hilo la kuweza kuwasaidia wachimbaji wadogo na zoezi hilo litaanza Januari 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa eneo la Kahama kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge eneo la Nyangalata pamoja na Mwanzimba, maeneo haya yalikuwa yakishikiliwa na mgodi wa *ABG* kwa leseni ambazo zilikuwa ni za watu binafsi wengine ni Watanzania ambao wallingia mikataba na *AGB*.

Tumefanikiwa kukubaliana na wenye leseni zile baada ya *ABG* kuziachia maeneo yale yatengwe kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Hivi sasa tupo katika taratibu za mwisho kabisa kwa eneo la Nyangalata ili kuweza kutoa leseni kwa vikundi ambavyo vimeanzishwa na wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. Sasa natangaza wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wanne wa Mheshimiwa Nelson Makongoro Mahanga Mbunge Naibu Waziri wa Kazi na Ajira ambao ni wawekezaji katika kampuni ya FUTAD ya Gwanzulu China wanaotaka kuwekeza katika viwanda vya kutengeneza pikipiki, mafuta na masuala ya ufundi katika *IT*. Karibuni sana, *Wellcome to the Parliament of Tanzania*. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mbunge ambao ni Ndugu Victoria Mwanache na Mwalimu Paschal Kafubi, karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Wageni waliofika kwa ajili ya mafunzo, Wageni wa Kaimu Katibu wa Bunge, Ndugu John Joel, ambao ni Mrs. Ramlati Jumanne, Miss Ashura Jumanne na Mr. Hakimu Jumanne. Karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mohamed Amour Chomboh, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge kutoka Zanzibar anaomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa imetokea ajali mbaya jana Jumapili tarehe 15 Desemba 2013 iliyohusisha wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya *Zanzibar University* na *State University of Zanzibar* SUZA ambayo wanafunzi 20 wamelazwa katika hospitali ya Dodoma watatu kati ya hao wakiwa na hali mbaya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI]

Wabunge wameanza kuchangia fedha ili kukabiliana na baadhi ya mahitaji muhimu. Hivyo tunawaomba Wabunge wengine wenye nia ya kuchangia kumwona Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mbunge wa Chaani.

Tangazo la Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba kuwatangazia Wajumbe wote wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 16 Desemba, 2013 saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao katika Ukumbi Na. 231 ghorofa ya pili, jengo la Utawala.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo, kuwa leo kutakuwa na Kikao tarehe 16 Desemba, 2013 Saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa B.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 16 Desemba, 2013 saa 7.00 mchana kutakuwa na Kamati katika Ukumbi 219 ghorofa ya pili jengo la Utawala. Katibu tuendeleo.

HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati Ulinzi na Usalama na Kamati
ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa**

**MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI
YA ULINZI NA USALAMA):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Kamati kuanzia Machi, 2013 hadi Novemba 2013, kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati hii waliteuliwa kwa barua yako Mwezi Machi, 2013 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Na. 113, Toleo la 2007. Wajumbe hao ni:- Mheshimiwa Anna Margreth Abdallah, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ni Mheshimiwa Dkt. Muhamed Seif Khatib.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Brig. Gen (msf). Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Capt.(msf) John Zefania Chiligati, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Mallole, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Rachel Masishanga Robert, Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere na Mheshimiwa Omari Rashid Nundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo na majukumu ya Kamati. Kamati imepewa majukumu mahususi ya kushughulikia taarifa za hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi na usalama wa raia na mali zao kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 7(2) (b) Nyongeza ya 8 ya Kanuni ya Kudumu za Bunge.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Maazimio, Bajeti na Ziara za Kamati. Kama inavyofahamika, Kamati za Bunge hutekeleza shughuli zake kwa niaba ya Bunge lako Tukufu. Katika kufanya hivyo kwa kipindi kilichotajwa, Kamati ilitekeleza majukumu hayo kwa kufanya shughuli zifuatazo:

Uchambuzi wa Miswada ya Sheria, Maazimio ya Uchambuzi wa Bajeti za Wizara, kujadili Taarifa za Utekelezaji na Utendaji wa Wizara na Taasisi zake. Pamoja na kutekeleza shughuli hizo, pia Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kufanya ziara sehemu mbalimbali nchini ili kujionea hali halisi na kuzishauri Wizara husika kuhusu hatua muhimu za kuchukua kupitia Bunge lako Tukufu. Katika kipindi hiki, Kamati haikuwa na Muswada wowote uliotakiwa kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maazimio, Katika kipindi hiki, Kamati yangu ilishughulikia Maazimio yafuatayo:-

Azimio la Bunge kulaani Tukio la ulipuaji wa bomu katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi Parokia ya Olasiti jijini Arusha tarehe 5 Mei, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia hivi sasa imekabiliwa na tishio kubwa la ugaidi ulilosambaa sehemu mbalimbali duniani. Mojawapo kati ya matukio hayo ni matukio ambayo Tanzania imekumbana nayo likiwemo tukio la ulipuaji wa bomu katika Kanisa la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi lililotokea Arusha tarehe 5 Mei, 2013.

Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Bunge liliridhia Azimio hilo. Azimio la Kuridhia Ulinzi wa Pamoja wa Afrika Mashariki, '*The East African Protocol on Cooperation in Defence Affairs*'.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

Kutokana na uzito wa suala hili naomba nikiri kuwa, wadau waliisaidia sana Kamati kutoa maoni yaliyoboresha Azimio hilo kwa kuzingatia hali ya ulinzi na usalama wetu na mustakabali wa nchi yetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kutokana na uzito wa michango yao, Kamati iliamua kukaa kikao cha pamoja na Kamati ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kufuatia kikao hicho iliamuliwa kuwa upitishwaji wa Azimio hilo usitishwe kwa muda. Kwa hiyo hadi sasa Azimio hilo halijaletwa Bungeni kutokana na sababu mbalimbali za kiitifaki. *(Makofi)*

Kupitishwa kwa Mpango wa Serikali kupeleka Wanajeshi nchini *DRC*. Baada ya Serikali yetu kuombwa na Umoja wa Mataifa kupeleka wanajeshi wetu Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo (DRC)* ili kujiunga na vikosi vya *UN* vya kulinda amani nchini humo.

Serikali iliwasilisha ombi hilo kwa Kamati hii ili itoe uamuzi. Kamati ilikaa pamoja na Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kutafakari ombi hili. Baada ya uchambuzi wa kina Kamati hizi mbili kwa niaba ya Bunge zilitoa idhini kwa Serikali kupeleka Wanajeshi *DRC* kwa maslahi ya amani ya *DRC* na pia kwa maslahi ya utulivu wa nchi yetu. Kutokana na idhini hiyo, Askari wetu walipelekwa *DRC*, na wanaendelea kutekeleza majukumu yao kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio na mapato na matumizi. Kwa kuzingatia utaratibu mpya ulioanzishwa na Bunge wa kujadili Bajeti ya Serikali mwezi Aprili kila mwaka badala ya mwezi Juni/Julai, Kamati ilipitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara inazosisimamia mwezi Machi na April, 2013 Jijini Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

(a) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

(i) Wizara ya Ulinzi na JKT – Fungu 57;

(ii) Ngome – Fungu 38;

(iii) Jeshi la Kujenga Taifa- Fungu 39.

(b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani – Fungu 51;

(ii) Idara ya Uhamiaji – Fungu 93;

(iii) Jeshi la Polisi – Fungu 28;

(iv) Jeshi la Magereza - Fungu 29; na

(v) Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji – Fungu 14

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto, baada ya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo, Kamati iliweza kubaini changamoto mbalimbali zinazokabili Wizara hizi. Zifuatazo ni baadhi ya Changamoto hizo :-

Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji. Kamati ilibaini kuwepo kwa tatizo kubwa la ukosefu wa zana za Uokoaji, hasa: *Cranes* Maalumu za kufukua watu waliobanwa kwenye vifusi vya majengo yanapo poromoka, ngazi ndefu na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

maalumu za kuokoa watu walionasa kwenye maghorofa marefu, boti za uokoaji kutokana na ajali za majini na kadhalika. Ukosefu wa zana hizi unazorotesha utendaji wa vikosi hivi pale vinapokabiliana na matatizo ya uokoaji wa maisha ya wananchi.

Jeshi la Magereza. Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la madeni ya muda mrefu ya wazabuni kutokana na Bajeti ndogo ya chakula cha Wafungwa, kwa sasa Serikali inatoa Tshs. 500/= tu kwa ajili ya chakula cha mfungwa kwa siku badala ya Tshs. 3,500/= zilizokubaliwa na Serikali na pia kuna changamoto sugu ya msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani.

Jeshi la Polisi. Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo kubwa la mafuta ya magari kwa ajili ya kufanya kazi za kawaida na za dharura za Polisi. Tatizo hili linaathiri kwa kiwango kikubwa ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Jeshi la Polisi. Takwimu zinaonyesha kuwa bajeti ya mafuta kwa magari ya Polisi ni lita 5 tu kwa siku.

Idara ya Uhamiaji. Kamati imebaini changamoto kuhusu tatizo kubwa la wimbi la wahamiaji haramu linatokana na ulegevu wa viongozi wa Serikali wa ngazi za vitongoji, vijiji na kata, pia linatokana na bajeti ndogo ya Idara ya Uhamiaji isiyotosheleza kununua vifaa vya doria mipakani na kuajiri watendaji wa kutosha katika vituo vya mipakani.

Jeshi la Wananchi (JWTZ).Changamoto ya uhaba wa nyumba za askari, na kusababisha askari wengi kuishi uraiani, badala ya kuishi makambini (*barracks*) kama ulivyo utaratibu wa majeshi yote duniani. Vilevile ipo changamoto ya raia kuvamia na kujenga ndani ya maeneo ya Jeshi kwa kuwa baadhi ya maeneo hayo bado hayajapimwa na kutolewa hatimiliki kwa jeshi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

Mheshimiwa Mwdenyekiti, ziara. Kamati kama nilivyoeleza hapo awali, katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu, Kamati ilifanya ziara mbalimbali za kikazi na za mafunzo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Asasi na Taasisi zilizo chini ya usimamizi wake kama ifuatavyo:-

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (*Mradi wa Ujenzi wa nyumba 10,000 za askari*);

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi (*Kituo cha kutengeneza vitambulisho vya Uraia (NIDA)*);

Jeshi la Kujenga Taifa (*Itende JKT*);

Jeshi la Polisi (*kukagua mradi wa ujenzi wa nyumba za askari Kambi ya Kilwa Road*);

Jeshi la Wananchi wa Tanzania (*Komandi ya Infantria na Nyuki Brigedi- Zanzibar*);

Jeshi la Magereza (*Magereza ya Segerea, Ruanda na Songwe*);

Makao Makuu ya Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji;

Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji;

Ziara ya Darfur-Sudan;

Ziara ya Mkoa wa Mbeya; na

Ziara ya Visiwa vya Pemba na Unguja.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ziara hizo zilikuwa na mafanikio makubwa kwani Kamati imejifunza mambo mengi na ilitoa ushauri kwa Wizara husika. Aidha utaratibu huu uliwezesha Kamati kujionea mafanikio na changamoto zinazozikabili Wizara husika katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya Darfur, Kamati ilipata nafasi ya kuwatembelea askari wa kulinda amani walioko Darfur nchini Sudani. Katika ziara hiyo Kamati ilikutana na kuzungumza na askari. Kwa kifupi askari wetu walikutwa wana morali ya hali ya juu na wanatekeleza jukumu la kulinda amani kwa juhudi, nidhamu na weledi wa kiwango cha juu.

Aidha kwa niaba ya Bunge, kamati ilitoa salamu za pole kwa askari wetu kutokana na vifo vya askari wenzao saba vilivyotokea tarehe 13 Julai, 2013 kutokana na kuviziwa na kushambuliwa na vikosi vya waasi walipokuwa wanasindikiza msafara wa watoa huduma za jamii vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya Mkoa wa Mbeya, napenda nilijulishe Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 21-24 Oktoba, 2013, Kamati ilitembelea Mkoa wa Mbeya ambapo ilikagua mpaka wa Tanzania na Malawi eneo la Kasumulu, Mradi wa Songwe *River Basin Development Program*, Gereza la Mkoa la Ruanda, Gereza la Kilimo la Songwe, Kambi ya JWTZ-44KJ; na Kambi ya JKT Itende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo ya Mkoa wa Mbeya, Kamati ilibaini changamoto kadhaa zinazoukabili Mkoa huo ikiwa ni pamoja na kukithiri kwa matukio ya uhalifu yakiwemo matukio ya mauaji, mengi yakiwa yanatokana na imani za kishirikiana na wivu wa mapenzi, unyang'anyi wa kutumia silaha, ubakaji, uvunjaji wa nyumba na wizi wa mifugo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

Changamoto nyingine ni kuongezeka kwa biashara ya madawa ya kulevya na pombe haramu ya *viroba* kutoka Malawi, na wimbi la wahamiaji haramu. Vilevile ipo changamoto ya kuwepo kwa vivuko mpakani visivyoo rasmi (njia za panya) zinazotumika kupitishia bidhaa za magendo na wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya Mipaka ya Tanzania na Zambia, kwa upande mmoja, na Tanzania na Malawi kwa upande mwingine, kwa jumla hali ni shwari. Hata hivyo, katika mpaka na Malawi, kituo cha mpakani (*border post*) cha Kasumulu, kuna changamoto kadhaa zilizojitokeza. Changamoto hizo ni:

Ukosefu wa vitendea kazi kama vile magari, mafuta, radio za mawasiliano (*radio call*) kwa matumizi ya Polisi na Uhamiaji, pia ukosefu wa vifaa vya kisasa vya Idara ya Forodha kukagua mizigo inayotishwa mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapenda kuishauri Serikali ifuatilie kwa karibu changamoto hizi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mkoa huo unapata vitendea kazi vya uhakika na vya kisasa vitakavyoyawezesha majeshi yetu kukabili na biashara ya madawa ya kulevya. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kudhibiti njia zote za panya zinazotumika kwa vitendo vya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara ya Zanzibar, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi hiki pia Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Visiwa vya Unguja na Pemba. Katika ziara hiyo Kamati ilikutana na askari ambao waliieleza Kamati mafanikio na changamoto mbalimbali ikiwemo ya uhaba wa nyumba za kuishi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

Kamati imeshawasilisha changamoto hizo kwa Mawaziri husika ili zifanyiwe kazi. Aidha Kamati ilikagua ujenzi wa kituo cha Polisi cha kijiji cha Sokoni Mchanga Mdogo (Pemba) kilichojengwa kwa nguvu za wananchi wakishirikiana na Polisi. Kamati inawapongeza wananchi hao kwa kujenga kituo cha Polisi na ni mfano unaostahili kuigwa na Wananchi wengi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Makao Makuu ya Uhamiaji upande wa Zanzibar na kuelezwa kuwa moja ya changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni Mamlaka ya Vizazi na Vifo (*RITA*) kuendelea kutoa vyeti vya kuzaliwa (*Birth Certificates*) vyenye maelezo au (*Column*) ya Uraia, jambo ambalo linafanya na kuongeza udanganyifu kwa Wahamiaji haramu wengi kujiandikisha kama ni raia wa Tanzania kwenye vyeti hivyo vya kuzaliwa.

Kamati inatambua kwamba mwenye mamlaka ya kutambua uraia ni Idara ya Uhamiaji na siyo RITA, hivyo Kamati inaishauri Serikali iielekeze Mamlaka ya Vizazi na Vifo (*RITA*) kufuta kipengele cha uraia kwenye vyeti vya kuzaliwa kwani inaleta mkanganyiko miongoni mwa Idara hizo za Serikali. *(Makofi)*

Kupokea na kujadili Taarifa za Hali ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki pia Kamati ilipata fursa ya kupokea Taarifa ya Hali ya Ulinzi na Usalama zilizowasilishwa kila baada ya miezi mitatu na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Mambo ya Ndani na Idara ya Usalama wa Taifa chini ya Ofisi ya Rais-Utawala Bora. Kamati ilipokea taarifa hizo na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya Kamati, baada ya maelezo hayo, sasa naomba niwasilishe Maoni na Mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwekwa kwenye Vipaumbele Sekta ya Ulinzi na Usalama. hivi sasa katika mpango wa Serikali wenye maeneo sita ya kipaumbele, Sekta ya Ulinzi na Usalama haimo. Amani, Ulinzi na Usalama ni kipaumbele kwa kusemwa kwa maneno tu, lakini kibajeti havijapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Kamati inaishauri Serikali irekebishe dosari hii ili nadharia ya kuienzi amani, ijionyeshe kwenye mgawo wa bajeti. Matokeo ya sekta ya Ulinzi na Usalama kutokuwa ya kipaumbele ni kwamba vyombo vya Ulinzi na Usalama vinapewa bajeti finyu isiyoweza vyombo hivi kufanya kazi kwa ufanisi wa kudumisha amani na utulivu nchini. *(Makofi)*

Hali hii ya kutokuwekeza katika kugharimia amani, ulinzi na usalama ikiachwa iendele, itadhoofisha vyombo vya Ulinzi na Usalama kiasi kwamba vitashindwa kulinda amani na utulivu uliopo hivi sasa, na matokeo yake Serikali itatumia gharama kubwa kurejesha amani iwapo itavunjika. *(Makofi)*

Ili tudumishe amani yetu ambayo ndio msingi wa maendeleo yetu, Kamati inaishauri Serikali itoe kipaumbele kibajeti kwa lengo la kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama vifanye kazi zao kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi Kuongezewa Bajeti. Kamati inapenda kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi zao kwa weledi japo katika mazingira magumu kutokana na changamoto nyingi zinazowakabili.

Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na bajeti isiyokidhi mahitaji hususan katika matumizi mengineyo *(OC)*. Ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kumudu majukumu yake ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali iliwezeshe kifedha na vifaa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

kwa lengo la kuliongezea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Operesheni Tokomeza na Operesheni Kimbunga. Kamati inaishukuru Serikali kwa juhudi za makusudi za kuanzisha Operesheni Tokomeza Ujangili na Operesheni Kimbunga zilizolenga kutokomeza wahalifu na uhalifu nchini. Pamoja na dosari zilizojitokeza na ambazo tayari zinafanyiwa kazi na Serikali na Bunge, bado Kamati inaishauri Serikali iendelee operesheni hizo kwa lengo la kuwatokomeza majangili na kuwaondoa wageni wote walioingia nchini kinyume cha sheria. Kamati inaamini kwamba Operesheni hizo bado ni muhimu kuendelea kufanyika kinachohitajika ni kurekebisha dosari zilizojitokeza na kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vitendo vya uhalifu dhidi ya watu wasio na hatia. Kamati imesikitishwa na matukio na vitendo vya Wananchi wasio na hatia wakiwemo viongozi wa dini kumwagiwa tindikali, kuharibiwa kwa nyumba za ibada na ulipuaji wa mabomu. Aidha Kamati hairidhishwi na kasi ya upelelezi na usikilizaji wa kesi zinazohusu matukio haya, kwa sababu hadi sasa hakuna kesi iliyomalizika Mahakamani na wahusika kuhukumwiwa kwa mujibu wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maandamano yasiyo rasmi. Katika siku za karibuni umezuka mtindo wa vikundi vya watu, Vyama vya Kisiasa au Mashirika yasiyo ya Kiserikali kufanya maandamano bila utaratibu wa kueleweka, yaani kufanya maandamano siku yoyote, mahali popote, na wakati wowote na hivyo kusababisha usumbufu miongoni mwa jamii ikiwa ni pamoja na shughuli za kijamii kusimama.

Kamati inatambua haki ya kikatiba ya vikundi mbalimbali kujumuika bila ya kuvunja sheria. Hata hivyo ni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI)]

maoni ya Kamati kwamba Serikali ipitie upya sheria zake ili hatimaye iandae muswada wa sheria itakayoweka utaratibu mahususi wa watu kuandamana utakaozingatia siku, muda na mahali ili kumwezesha mwananchi atumie haki yake ya kuandamana bila ya kuingilia uhuru wa mtu mwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Teknolojia ya kisasa katika kuimarisha ulinzi wa Polisi. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha matumizi ya teknolojia ya kisasa kwa ajili ya ulinzi katika maeneo ya mikusanyiko mikubwa ya watu, na hasa matumizi ya kamera maalumu (CCTV) ili kunasa nyendo za wahalifu katika maeneo hayo.

Vilevile katika ukamataji wa madereva wanaokiuka sheria za barabarani, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inashauriwa ianzishe utaratibu wa kuweka kamera maalumu zitakazo wanasa madereva wote wanaovunja Sheria za *Traffic*. Hatua hii pia itapunguza rushwa miongoni mwa askari wa Traffic kwani kazi ya ukamataji makosa ya barabarani sasa itafanywa na kamera maalumu zitakazoonyesha mahali na saa ya tukio, badala ya Polisi wa *Traffic* ambao baadhi yao hutumia fursa hii kupokea rushwa.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mradi wa nyumba za Askari Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba 10,000 za askari. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali isimamie kwa karibu ujenzi wa nyumba hizo ili zikamilike katika muda uliopangwa kwa lengo la kupunguza tatizo la uhaba wa nyumba za askari na maofisa wa Jeshi la Wananchi na JKT.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI)]

Hatua hii itapunguza rushwa miongoni mwa askari wa trafiki kwani kazi ya ukamataji makosa barabarani sasa itafanywa na kamera maalumu zitakazoonesha mahali na saa ya tukio badala ya trafiki wa polisi ambao baadhi yao hutumia fursa kupokea rushwa.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa: Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba 10,000 za Askari. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali isimamie kwa karibu ujenzi wa nyumba hizo ili zikamilike katika muda uliopangwa kwa lengo la kupunguza tatizo la uhaba wa nyumba za Askari na Maofisa wa Jeshi la Wananchi na JKT.

Mweshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafunzo ya JKT; Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri wa Bunge kuhusu kurejesha mafunzo kwa mujibu wa Sheria kwa vijana wanaohitimu sekondari na vyuo. Kwa hali halisi ilivyo, Kamati inaona kuwa mafunzo ya miezi mitatu hayatoshi kumbadilisha kijana ili kumjengea moyo wa uzalendo kwa nchi yake, kumjenga kimaadili na kumuwezesha kuwa na stadi za kujitegemea; hivyo basi, Kamati inashauri Serikali iongeze muda wa mafunzo haya walau yawe ya muda wa miezi sita badala ya miezi mitatu ya sasa. Aidha, vijana ambao watakwepa kwenda JKT bila sababu za msingi wanakiuka Sheria; hivyo, Serikali iwachukulie hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inazidi kusisitiza kwamba, Serikali iwe na mkakati utakaowezesha vijana wote wanaojiriwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kama vile Jeshi la Wananchi, Polisi, Magereza, Zima Moto na Uokoaji, Uhamiaji na Usalama wa Taifa, watoke Jeshi la Kujenga Taifa. Hatua hii itaimarisha moyo wa kizalendo na utaifa katika Vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inashauri Serikali iliwezeshe Jeshi la Kujenga Taifa, liandae mafunzo kwa vikundi maalumu kama vile Viongozi katika Idara za Serikali, Mashirika ya Umma, Mashirika yasiyo ya Serikali na Wahariri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI)]
wa Vyombo vya Habari ili kujenga uzalendo kwa makundi
haya muhimu yenye ushawishi mkubwa kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea kwenye mipaka ilibaini kuendelea kuwepo kwa tatizo la kun'golewa kwa alama za mipaka (*beacons*) na kuvamia maeneo ambayo hayaruhusiwi kwa makazi kwa mujibu wa Sheria. Kamati inasikitika kuona kuwa tangu Bunge la Tisa, imekuwa ikizungumzia kuwepo kwa tatizo hili, lakini hadi sasa hakuna hatua zilizochukuliwa. Kwa kuwa suala hili ni mtambuka, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuzielekeza Wizara za Ardhi na Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Kimataifa, zishughulikie kurudisha alama hizo mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe suala la ujenzi na ukarabati wa barabara za usalama mipakani, linaweka mkakati maalumu wa Kitaifa. Moja ya mikakati hiyo iwe ni kuziweka barabara hizi chini ya *TONROADS* na *tender* za matengenezo zitolewe kwa Vitengo vya Uhandisi vya Jeshi na JKT kwa vile wana wataalam na zana za kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kulipa Jeshi la Kujenga Taifa jukumu la kutengeneza samani za Serikali kwani wanao uwezo mkubwa wa kufanya kazi hizo. Aidha, Serikali iweke mkakati wa kutumia Jeshi, JKT na Magereza kwa kuwapa zabuni za Miradi iliyo ndani ya uwezo wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwasiliana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iweze kutoa mapema iwezekanavyo, mapendekezo yatakayowezesha kukamilika kwa Sera ya Taifa na Ulinzi na hatimaye Sheria ya Usalama (*National Defence Act*). Mkakati wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Ulinzi ilianza tangu Bunge la Kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inashauri Serikali kuharakisha kuleta Bungeni Sheria Namba 16 ya 1964

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI)]

inayounda Jeshi la Kujenga Taifa ili ifanyiwe marekebisho kuendana na malengo na mazingira ya wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefuatilia na kubaini kwamba, kutotekelezwa kwa ukamilifu Sheria ya Msamaha (*Parole*), ni moja ya sababu inayosababisha msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani. Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni marekebisho ya Sheria hiyo ili kupanua wigo wa kuwahusisha wafungwa wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, Kamati ilibaini kwamba, Sheria inawataka waharifu wenye makosa madogo madodo kupewa adhabu ya vifungo vya nje ili watumikie jamii (*Communities Services Act*), nayo haitekelezwi kwa ukamilifu; hivyo, husababisha msongamano wa wafungwa Gerezani. Sheria hii tangu ilipopitishwa na Bunge mwaka 2002, inafanya kazi katika Mikoa 17 tu ya Tanzania Bara kutokana na uhaba wa fedha, Watendaji na vitendea kazi. Kamati inashauri Serikali iwezeshe Sheria hii ifanye kazi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara ili isaidie kupunguza tatizo la msongamano Magerezani kama ilivyokusudiwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza yetu kwa sasa yanakabiliwa na msongamano mkubwa wa wafungwa. Kati ya wafungwa hao, wengine ni wahamiaji haramu ambao hukaa Gerezani kwa muda mrefu bila kurudishwa makwao. Mfano, Kamati imefanya ziara Mkoani Mbeya, ilikuta kulikuwa na jumla ya wahamiaji haramu 262 kwenye Gereza la Ruanda. Kamati inashangazwa na Serikali kwamba, haina fedha ya kuwarudisha wahamiaji haramu makwao, wakati inatumia fedha nyingi kuwalisha na kuwatunza Magerezani. Hivyo basi, Kamati inahimiza Serikali iwarudishe makwao wahamiaji hao ili kupunguza mzingo wa walipa kodi ya Watanzania kuendeleza kuwatunza wahamiaji haramu wapatao 1,172 katika Magereza yote nchini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza yetu tuna wafungwa wengi kutoka nchi za nje waliofungwa kwa makosa mbalimbali ya jinai. Moja ya njia ya kupunguza idadi ya wafungwa wa aina hiyo ni kwa Serikali kuweka utaratibu wa Kisheria kurudishiana wafungwa na nchi zenye wafungwa wengi kwenye Magereza yetu hasa nchi za jirani za Burundi, Rwanda na Kenya ili wakatumikie adhabu ya vifungo kwenye Magereza ya nchini kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati imebaini kuwa, kuna msugurano wa mapato ya *Visa* kati ya Wizara ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwani hivi sasa Wizara ya Mambo ya Nje, wameweka utaratibu wa kutokuwa na Maofisa Wahamiaji kwenye balozi zetu nchi za nje na hivyo kusababisha shughuli za uhamiaji kufanywa na watu wasiokuwa na ujuzi huo, likiwemo suala la ukusanyaji wa mapato ya *Visa*. Jambo hili siyo tu linasababisha kupotea kwa mapato ya Serikali, bali pia ni hatari kwa Usalama wa Taifa. Kamati inaishauri Serikali ishughulikie tatizo hili ili Maofisa Uhamiaji wapelekwe kwenye Balozi zetu, hasa zile zenye wasafiri wengi wanaoomba *Visa* katika Balozi zetu nje. Aidha, Serikali inashauriwa isimamie kwa ukaribu utaratibu wa *Visa* kutolewa kwa mashine za stika katika Balozi zetu na ipige marufuku utoaji wa *Visa* kwa utaratibu wa kugonga muhuri kwenye *Passport* kwani unavujisha mapato ya Serikali yatokanayo na *Visa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishukuru Serikali kwa kuanzisha maeneo mapya ya utawala ili kusogesa huduma za Wananchi. Hata hivyo, inashauri Serikali ijitahidi kujenga Vituo vya Polisi, Magereza na Mahakama katika maeneo haya mapya hususani katika Wilaya na Mikoa mipya inayoanzishwa, kwani moja ya sababu kubwa ya msongamano wa mahabusu na wafungwa ni kukosekana kwa Vituo vya Polisi, Magereza na Mahakama, katika Wilaya hizo mpya na hivyo kulazimisha kusafirisha mahabusu kwenda Wilaya nyingine kufuata huduma hizo na hivyo kusababisha gharama kubwa kwa Serikali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi na Mbili lilitokea tukio la aibu ndani ya Bunge, ambapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walirushiana ngumi na mateke Bungeni na askari wanaolinda usalama wa Bunge, baada ya askari hao kutekeleza amri halali ya Kiti na hivyo kuhatarisha amani na usalama wa Bunge na Wabunge. Kamati ya Ulinzi na Usalama imetafakari kwa umakini suala hili na kuona siyo vyema kukaa kimya na tukio lile likapita bila kulishauri Bunge lako Tukufu kuhusu hatua mwafaka kukabiliana na hali hiyo. Kamati inashauri kwamba, Kanuni na Sheria zote zinazohusiana na haki na madaraka ya Bunge, zipitiwe upya ili kuweka Kanuni za Maadili ya Wabunge (*Code of Ethics*) kwa lengo la kukabiliana na vitendo vinavyolidhalilisha Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuitikia wito wa Mheshimiwa Rais kwamba, Jeshi la Magereza na JKT watoe mchango katika kutekeleza azma ya Mapinduzi ya Kilimo Nchini kwa kuzalisha mbegu bora, Jeshi la Magereza katika baadhi ya Magereza na pia Makambi ya JKT, msimu uliopita walizalisha mbegu bora za mahindi na kuziua kwenye makampuni yanayosambaza mbegu hizo. Hata hivyo, baadhi ya makampuni hayo bado hayajalipia mbegu na hivyo kupunguza uwezo wa Magereza na JKT kulima mbegu msimu ujao. Kamati inashauri Serikali iyabane makampuni yanayodaiwa na Magereza na JKT walipe haraka iwezekanavyo ili kuwezesha Magereza na JKT wajiandae kuzalisha mbegu zingine msimu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kufanikisha shughuli za Kamati yetu katika kipindi hiki chote. Aidha, napenda nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Job Ndugai - Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wote, ukiwemo wewe Mheshimiwa Zungu, Mwenyekiti wetu wa leo hapa Bungeni, kwa kutusaidia vizuri katika kufanikisha shughuli zetu za Bunge. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashillillah na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. KAWAWA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI)]

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama katika kipindi cha Machi hadi Desemba, 2013. Naomba pia Taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(*Makofi*)

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

MHE. JUMA S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati hiyo kuhusu shughuli zake kwa kipindi cha Machi, 2012 hadi Desemba, 2013 kwa mujibu wa Kanuni ya 117, Ibara ya 15 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati hii waliteuliwa mwezi Machi, 2013 kwa mujibu wa Kanuni ya 116 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Wakati wa uteuzi ulituteua jumla ya Wajumbe 15, lakini kwa sasa tupo Wajumbe 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa dhati kwa jinsi ulivyozingatia vigezo muhimu vilivyoainishwa katika Fasili ya Tano ya Kanuni ya 116 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili mwaka 2013. Kwa namna hiyo, Kamati imeweza kuwa na Wajumbe wenye taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu kwa utekelezaji wa majukumu yake. Tunaamini ulifanya hivyo pia kwa Kamati zingine zote.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati hii yameainishwa katika Fasili ya Nne ya Kifungu cha Sita pamoja na Fasili ya Kwanza ya Kifungu cha Saba, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Majukumu hayo ni kusimamia Wizara mbili ambazo ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu, Kamati pia ina majukumu mengine manne yaliyoainishwa kwenye Kifungu cha 2(a) cha Fasili ya Saba ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013. Majukumu hayo ni kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya Nchi nyingine, kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (c) kushughulikia Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika, kushughulikia Taarifa zote za Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 119 ya Kanuzi za Kudumu za Bunge, imetoa ruhusa kwa Kamati yoyote ikiwemo Kamati ya Kudumu za Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuwa na majukumu zaidi ya yale yaliyotajwa moja kwa moja kwenye Kanuni za Bunge. Namna mbili za majukumu ya nyongeza kwa mujibu wa Kanuni ya 119 ni Kamati kupendekeza ipewe jukumu la nyongeza, Kamati kupewa jukumu lingine lolote kadiri Spika atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizojitokeza; Wajumbe wa Kamati walifanya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu kwa mujibu wa Kanuni ya 116 na baadaye Mpango Kazi kwa kipindi cha Julai, 2013 – hadi Juni, 2014 ulioandaliwa kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
ikiwemo Kanuni ya 117 inayohusu taratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Kamati ilisimamia Wizara mbili zilizo chini yake pamoja na kufuatilia hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki. Mbali ya majukumu hayo, Kamati pia ilipokea na kujadili Taarifa za Wawakilishi wa Bunge kwenye Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika na Vyama vya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizofanyika katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati ni pamoja na kufuatilia mwendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki; kufuatilia utekelezaji wa Wizara zilizo chini ya Kamati; kufuatilia hali ya ujirani mwema nchi zinazopakana nazo; kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Ushirikiano wa Kimataifa; kushughulikia bajeti ya Wizara zilizoko chini ya Kamati hii; kushughulikia Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania kwenye Bunge la Afrika, Afrika Mashariki, SADC pamoja na Vyama vingine vya Kibunge ambako Bunge la Tanzania ni Mwanachama; na mwisho ni kuwasilisha Azimio Bungeni.

Maelezo na maoni ya kamati kutokana na shughuli hizo yanafanuliwa katika Taarifa hii. Jambo lingine muhimu lililojadiliwa linahusu mchakato wa kuridhia mikataba iliyosainiwa pamoja na namna ya kuainisha Sheria za Nchi na masharti ya mikataba hiyo. Katika semina hiyo ilibainika changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Nchi kutoainishwa na mikataba na itifaki. Ni ukweli ulio wazi kwamba, mara baada ya nchi kusaini na kuridhia Mikataba au Itifaki ya Kimataifa chini ya Sheria ya Kimataifa, nchi inakuwa na mujibu, haki, kwa mujibu wa Mkatoba au Itifaki husika. Kwa sababu hiyo, hali ya mikataba iliyoridhiwa kutoainishwa na Sheria za Nchi husababisha mkanganyiko kati ya Sheria ya Kimataifa (*International Law*) na mfumo wa Sheria za Nchi. Kwa mfano, licha ya Tanzania kusaini na kuridhia Itifaki ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
SADC Kuhusu Jinsia (The SADC Protocol of Gender), bado Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 haiendani na Itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa Tanzania imesaini Itifaki hiyo mwaka 2008 na Bunge lako Tukufu likaridhia mwaka 2010. Katika Itifaki hiyo, Ibara ya 8 inapingana na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971. Eneo lenye tofauti kati ya Mkataba na Sheria ni umri wa chini wa mwanamke kuolewa wakati Ibara ya 8 ya Itifaki ya *SADC* inataka umri wa kuoja kwa mwanamume na kuolewa kwa mwanamke uwe miaka 18, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inaruhusu mwanamke chini ya umri wa miaka 18 kuolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo jambo jema kwa nchi kusaini na kuridhia Mkataba wa Itifaki bila kutunga Sheria sambamba na mikataba hiyo; hivyo, Kamati inashauri dosari hii ifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugumu wa utekelezaji wa Mikataba; Mikataba ya Kimataifa itakuwa na mafanikio iwapo utekelezaji wake utawezekana. Mwendendo wa utekelezaji wa baadhi ya Mikataba na Itifaki zilizoridhiwa unaonesha ugumu wa kufikia lengo. Kamati inaona kuwa hakuna ugumu wa utekelezaji katika mikataba kwa kuwa utaratibu wa kuridhia mikataba hiyo unahusisha kujiridhisha. Iwapo Mkataba unaendana na Sera na Masharti ya Katiba ya Nchi, pia kwa kuzingatia faida zinazoweza kupatikana, Kamati imebaini kuwa, pamoja na utaratibu wa kuridhia kuwa mzuri, bado kuna ugumu wa utekelezaji wa baadhi ya mikataba na itifaki zilizoridhiwa. Kwa mfano, wakati Tanzania inasaini na kuridhia Itifaki ya *SADC* kuhusu jinsia, mchakato uliohusisha kuainisha masharti ya Itifaki na Katibu ya Nchi na Sera za Nchi yetu. Hata hivyo, kwa hali hiyo kisera siyo rahisi kufikia lengo linalohitajika kwa Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufafanuzi zaidi naomba kurejea Ibara ya 15 ya Itifaki ya *SADC* inayotaka nchi kuwa na uhusika sawa baina ya wanawake na wanaume katika utayarishaji na utekelezaji wa Sera za Uchumi hadi kufikia mwaka 2015. Kwa hali ilivyo sasa, lengo la Itifaki iliyosainiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
na kuridhiwa siyo rahisi kulifikia. Hali hii si jambo jema kwa Taifa na inahitaji kurekebishwa. Jambo muhimu kuhusu Itifaki na Mikataba ni kusaini na kuridhia baada ya kutafakali kuhusu uwezekano wa kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matayarisho hafifu kuhusu Mikataba ya Kimataifa kwa masilahi ya Taifa ya Sera, Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii. Kama wengi tunavyofahamu katika majadiliano na makubaliano kuhusu Mikataba ya Mataifa (*International Treaties*), matayarisho ni jambo la msingi ili masilahi ya Taifa, Kisera, Kisiasa na Kiuchumi na Kijamii, yazingatiwe ipasavyo. Wataalam wa kila nchi wanapaswa kujiandaa kwa majadiliano. Uzoefu unaonesha yapo malalamiko kuhusu matayarisho hafifu kwa upande wetu, ni vyema suala hili likafanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji wa hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki ni jukumu mojawapo la Kamati hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Katika kuteleza jukumu hilo, Kamati iliendelea kufuatilia hali ilivyo ili kujiridhisha kuhusu usimamizi wa masilahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 17 na 18 Oktoba na tarehe 8 Novemba, 2013, Kamati imefanya kikao cha pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ili kufahamu mambo makuu mawili; kwanza, uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na pili, hali na hatua ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya mtangamano wowote hutegemea uhusiano uliopo miongoni mwa Nchi Wanachama. Hali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inategemea kwa kiasi kikubwa, uhusiano miongoni mwa Rwanda, Uganda, Kenya, Burundi na Tanzania. Wakati wa kujadili taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Wajumbe walitaka kujua mambo mbalimbali kwa lengo la kujiridhisha kuhusu nafasi ya Tanzania katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa mambo yaliyogusiwa ni kuhusu mikutano ya tatu (*tripartite*). Kamati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
ilitaka kujua athali ya mikutano hiyo na kubaini mambo yafuatayo:-

Mikutano hiyo ya nchi tatu pamoja na mambo mengine, imeamua kuwa nchi hizo ziendeele kutekeleza himaya ya umoja wa forodha. Hali hiyo ni tofauti kabisa na makubaliano yaliyopo katika ngazi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini katika kutathmini Kamati imebaini kuwa, makubaliano ya nchi hizo huathiri kwa kiasi kikubwa majadiliano kuhusu himaya moja ya forodha katika ngazi ya Jumuiya. Licha ya kuwa na Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Nchini Tanzania, ambapo kuna jengo linaloweza kutumika kwa mikutano, Bunge la Afrika Mashariki liliamua kufanya vikao kwa mtindo wa mzunguko. Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kubaini kuwa Ibara ya 55(2) ya Mkataba inatamka kuwa, nanukuu: *“Subject to the provision of paragraph (1) of this Article, the Assembly shall meet at least once in every year at Arusha in the United Republic of Tanzania and at a time to be determined by the Assembly.”* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ingawa uamuzi wa Bunge la Afrika Mashariki kufanya vikao kwa mzunguko haukiuki Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna athari ya kiutawala na kibajeti kwa Sekretarieti ya Jumuiya hiyo. Ni dhahiri utekelezaji wa uamuzi huo, unahitaji bajeti kubwa zaidi kuliko kama mikutano hiyo ingefanyikia Arusha, Makao Makuu ya Jumuiya. Ili kufuatilia kwa kina, Kamati ilihoji kwa undani na kubaini kuwa takribani Dola za Kimarekani 50,000 za ziada huhitajika kufanya mikutano nje ya Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya Mikutano ya Utatu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki: Hakuna tatizo kwa Tanzania kutokuwa sehemu ya nchi tatu zinazoendelea na mikutano iwapo masharti ya Ibara ya 7(1)(e) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yatazingatiwa. Mkataba unaruhusu Nchi Wanachama kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
Jumuiya kwa kasi tofauti. Utaratibu huu unaitwa *The principle of variable geometry which allows for progression in co-operation among groups within the fields and at different speeds*. Hata hivyo, ni ukweli ulio wazi kuwa, baadhi ya mambo yanayojadiliwa katika Mikutano ya Utatu na kutolewa uamuzi bado yanaendelea kujadiliwa katika ngazi ya Jumuiya. Hali hiyo ni kinyume na ruhusa iliyotolewa kwenye Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Kibunge kuhusu kuisimamia Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni la msingi. Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, jukumu hilo lipo chini ya Kamati hii. Ili kutekeleza vyema jukumu la Kamati njia mbalimbali zilitumika. Njia hizo ni pamoja na kuhoji mambo mbalimbali yanayohusiana na majukumu ya Wizara hizo; kuzitaka Wizara kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa shughuli zake kwa namna Kamati itakavyoona inafaa; kutaka maelezo ya Wizara kuhusu jambo lolote mahususi linalohusu kazi za Wizara hizo kwa mujibu wa Hati ya Serikali ya uanzishwaji wa Wizara hizo; na mwisho ni kuchambua taarifa ya mwenendo wa utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa kila robo au nusu ya mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia njia hizo, Kamati imebaini mambo mbalimbali kama yanavyofafanuliwa katika Taarifa hii. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, miongoni mwa mambo hayo katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya kila Wizara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipofuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Malimbikizo ya madeni ya Watumishi na Wazabuni. Kumbukumbu zinaonesha kuwa hadi tarehe 14 Agosti, 2013 wakati Wizara ilipotoa taarifa yake kwa Kamati,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
ilikuwa inadaiwa Sh. 663,324,519 deni la tangu Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

(b) Kushindwa kufanikisha malengo ya kuwawezesha Watanzania kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mtangamano na hivyo kuwafanya Watanzania washindwe kuzitumia kikamilifu fursa zitokanazo na utangamano wa Afrika Mashariki.

(c) Ushiriki hafifu wa wadau ikiwa ni pamoja na Wizara za Kisekta kutotoa uzito stahiki kwa masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(d) Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutokuwa na kasi inayolingana na ile ya Jumuiya kukua haraka.

(e) Ukosefu wa Sera inayotoa mwongozo na kuainisha misimamo ni miongoni mwa mambo ya hatari yanayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 1999 Tanzania ilipojiunga na Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, haijawahi kuwa na Sera Maalum kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki. Kumbukumbu zinaonesha kuwa, Taarifa za Wizara hii tangu Bunge la Tisa zimeendelea kueleza kwamba, mchakato wa uandaaji wa Sera hiyo unaendelea. Siyo jambo jema kwa Sera muhimu kama hii kuendelea kuwa kwenye mchakato usiojulikana utakamilika lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatari kutekeleza jambo lisilokuwa na mwongozo bora wa Kiseru. Kasi ya kukabiliana na hatari hiyo siyo nzuri na inahitaji kuongezwa. Kwa mfano, tangu Tanzania imekuwa Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivi sasa ni takribani miaka kumi na minne. Baadaye Kamati inayohusisha Wadau kutoka Wizara za Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Viwanda na Biashara na Wadau wengine ndiyo kwanza wamekutana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
tarehe 14 - 16 Agosti, 2013 ili kupitia Rasimu ya Awali. Kasi
hiyo ni dhahiri inahitaji kurekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza jukumu la kuisimamia Wizara hii, kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 7(1) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(4)(a), Kamati ilirejea Hati ya Serikali ya Uanzishaji wa Wizara. Kwa mujibu wa Waraka huo, miongoni mwa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, kusimamia Mikataba ya Kimataifa, kuanzisha na kusimamia huduma za kikonseli na kulinda na kuendeleza masilahi ya kitaifa ya kiuchumi na mengineyo nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

Kwanza, ni kutofanyika kwa Mikutano ya Mabalози. Licha ya umuhimu mkubwa wa Mikutano ya Mwaka ya Mabalози kwa ajili ya kutathmini na kuboresha mambo ya msingi, ni miaka saba sasa Wizara haijaratibu Mikutano hiyo. Athari ya hali hiyo ni kukosekana kwa tathmini muhimu, jambo linaloweza kukwaza ufanisi wa Balози zetu na Wizara kwa ujumla.

Pili, majengo yanayomilikiwa na Serikali kutokarabatiwa. Kutokana na Majengo yanayomilikiwa na Serikali kutokarabatiwa na kwa hali halisi majengo mengi yanayomilikiwa na Balози zetu yanaaibisha kwa kuathiri hadhi na taswira ya nchi yetu. Matokeo yake si thamani ya majengo yaliyonunuliwa kwa fedha za Umma inateremka, bali pia inasababisha baadhi ya Watumishi kukata tamaa katika Balози hizo.

Tatu, Serikali imenunua viwanja katika nchi mbalimbali duniani kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na nyumba kwa matumizi ya shughuli za Kibalози, lakini hadi sasa hakuna hatua zilizochukuliwa kuvijenga. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Mheshimiwa Spika, hali hii inaweza kusababisha Serikali za nchi hizo kuvichukua viwanja hivyo kwa mujibu wa Sheria na taratibu za nchi zao kuhusu umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuwa na majengo ya Serikali kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi una faida nyingi. Mkakati wa kutekeleza uamuzi huo una manufaa ya kiuchumi, kisiasa, kiutawala na kidiplomasia. Kwa kuwa ni suala la kimkakati kuwa na majengo haya, ilitazamiwa kuwa, ushauri ambao umekuwa ukitolewa Bungeni mara kwa mara, kuhusu chombo cha kununua na kukarabati majengo ungetekelezwa lakini sivyo ilivyo. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati kwa kipindi chote cha Machi hadi Novemba, 2013, zinaonesha kukosekana kwa chombo maalum cha kushughulikia ununuzi na ukarabati wa majengo kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa chombo hicho maalum kwa ajili ya Majengo ya Serikali nje ya nchi, zinajitokeza dosari kadhaa za kimkakati. Kwa kuwa Wizara kwa sehemu kubwa zinahusika na uandaaji wa sera na kusimamia utekelezaji wake, siyo rahisi kufanikiwa katika usimamizi wa majengo. Matokeo ya kukosekana kwa chombo hiki ni kutofanya vizuri katika makusanyo ya mapato yatokanayo na majengo na kutotumia vyema hali ya soko la majengo mbalimbali ya nchi nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kununua majengo nje ya nchi kwa kuweka mali rehani (*Mortgage Financing*) ungeweza kusaidia na kuongeza mafanikio ya mkakati wa Serikali. Hata hivyo, katika kufuatilia Kamati ilielezwa kuwa, Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya Mwaka 1974 iliyorekebishwa mwaka 2004 (*The Government Loans, Guarantees and Grants Act*) ni changamoto kwa utekelezaji wa azma hiyo. Naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilishauri Sheria hii ifanyiwe marekebisho.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Ucheleweshaji wa fedha kwenda kwenye Balozi zetu ni jambo lingine linaloathiri ufanisi wa Balozi hizo. Licha ya ushauri uliotolewa Bungeni kuhusu utaratibu wa Hazina kupeleka moja kwa moja fedha za Ubalozi, bado mchakato wake ni wa taratibu mno kinyume na ushauri wa Bunge. *(Makofi)*

Kutokamilika kwa Sera ya Mtangamano wa Kikanda ni dosari inayoihusisha pia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kwa taarifa iliyotolewa kwenye Vikao baina ya Kamati na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, suala la Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki linachukuliwa kwa upana mkubwa ili kuwa na Sera ya Mtangamano wa Kikanda ikijumuisha Jumuiya ya SADC na nyinginezo ambazo Tanzania ni Mwanachama. Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki imekamilisha sehemu yake mapema kabla Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, haijakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Diplomasia ya Uchumi ni suala lenye mtazamo mpana na linalohusisha wataalam wa fani, Wizara na Idara tofauti tofauti, si jambo la kuachwa pasipo uratibu bora. Kwa muda mrefu sasa licha ya Kamati kushauri uanzishwaji wa Kitengo Maalumu cha Kuratibu Diplomasia ya Uchumi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa haijawa na Kitengo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Wizara hii kuhusu suala hilo ni kuwa na Wataalamu wa Fani mbalimbali za Siasa, Uchumi na Sheria. Aidha, Wizara inaeleza kuwa, pale inapohitajika Wataalamu huchukuliwa katika Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Maoni ya Kamati ni kuwa, uratibu wa Wataalamu hao na wale wa Taasisi nyingine unahitaji upekee wa kimkakati na utawala. Ni kwa msingi huo tunaona kuwa, kutokuwa na kitengo cha kuratibu masuala ya Diplomasia ya Uchumi si jambo la kuendelea nalo.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utekelezaji wa jukumu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
Kimataifa la kuratibu Masusala ya Uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine, Kamati ilitaka kujua hali ya ujirani mwema na nchi zinazopakana na Tanzania. Kutokana na taarifa zilizowasilishwa, Kamati ilibaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhusiano wa Malawi na Tanzania unaathiriwa na mgogoro wa mpaka. Taarifa zimeonesha kuwa, jitihada za pande mbili kuhusu suluhisho la mgogoro wa Mpaka wa Ziwa Nyasa zinaendelea. Juhudi za kusuluhisha mgogoro huo hadi sasa hazijafanikiwa. Mgogoro huo kwa sasa upo kwenye Jukwaa la Marais Wastaafu wa Nchi za SADC kwa ajili ya usuluhishi. Ili kugharamia usuluhishi, kila nchi iliombwa ichangie USD 761,016.96. Kamati imejulishwa kuwa, Tanzania imechangia kiasi cha USD 387,336.96, sawa na asilimia 50.9. Kwa upande wa pili, Malawi imechangia USD 50,000.00, sawa na asilimia 6.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa, Tanzania imechangia kiasi ambacho ni karibu mara nane ya kiasi cha mchango kilichotolewa na Malawi. Zaidi ya hivyo, nchi ya Malawi imeendelea kuonesha nia yake ya kutaka kuharakisha kuwasilisha suala hili katika Mahakama ya Kimataifa. Kamati ilijulishwa kuwa, msimamo wa Tanzania ni kutoa muda wa kutosha na fedha za kukamilisha kazi ya msuluhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge katika Kifungu cha 7, Fasili ya 1 (c), inaitaka Kamati hii kufuatilia utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Miongoni mwa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC). Aidha, Wizara hii vilevile inasimamia Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es Salaam na kusimamia Taasisi inayoshughulikia Mpango wa Afrika Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM). Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu mambo ambayo Kamati imebaini kwa kila Taasisi kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Mheshimiwa Spika, Historia ya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha (JNICC) inatokana na kusainiwa kwa Mkataba wa Ujenzi baina ya Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China, Tarehe 11 Aprili, 2008. Gharama za ujenzi zinatokana na asilimia 46.5 ambayo ni msaada (*Grant*) na kiasi kilichobaki ni mkopo nafuu usio na riba (*soft loan*).

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini yafuatayo katika Kituo hiki:-

(a) Wizara haina thamani halisi ya Jengo hili, jambo ambalo ni hatari, kwani haijulikani deni litakalolipwa ni kiasi gani.

(b) Hakuna *BoQ* za jengo, jambo linalotia wasiwasi.

(c) Uendeshaji wa Kituo hiki umeamuliwa kuwa chini ya Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Arusha (*AICC*). Kwa uamuzi huo, *JNICC* itaongozwa na Meneja atakayewajibika kwa Mkurugenzi wa Mikutano na Masoko wa *AICC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya diplomasia na utalii duniani inatambua Mikutano ya Kimataifa. Kwa sababu pia ni utaratibu wa kawaida kwa nchi nyingi kuwekeza kwenye vituo vya mikutano ya Kimataifa kwa ajili ya utalii wa mikutano. Tanzania kwa upande wetu, tunacho kituo kikubwa cha mikutano hiyo ambacho ni *Arusha International Conference Center (AICC)*. Kituo hicho kinamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 na kilianzishwa mwaka 1978 kwa kutumia majengo yaliyokuwa ya Jumuiya ya zamani ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utendaji wake, Kituo hicho kinapata fursa nzuri ya kibiashara kutokana na umaarufu wa Tanzania kwa kuenzi amani, usalama na utengamano, jambo ambalo ni mtaji na kivutio kikubwa kwa upande wa Sekta ya Utalii wa Mikutano. Hata hivyo, Kituo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto zilizobainika ni suala la ukosefu wa eneo la kutosha kwa ajili ya maonesho (*Convention and Exhibition Centre*). Aidha, licha ya kuwa rasilimali nyingi za Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (*AICC*) zipo katika maeneo nyeti ya Jiji la Arusha, hakuna juhudi za kutosha zilizofanyika kuendeleza rasilimali hizo ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuliwezesha Taifa kutumia hali yake ya usalama, amani na utengamano, *AICC* imependekeza na kukubaliwa wazo la kuwa na Kituo cha Kisasa cha Kimataifa cha Mikutano (*Mount Kilimanjaro International Covention Centre MK-ICC*), kitakachokuwa na eneo la kutosha kwa ajili ya maonesho. Kamati imeridhishwa na mapendekezo hayo na kwamba, yakitekelezwa ipasavyo, yataiwezesha nchi kutumia nafasi na umaarufu katika kukuza uchumi wa Taifa kupitia Utalii wa Mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Jijini Dar es Salaam kilianzishwa kwa pamoja na nchi mbili za Tanzania na Msumbiji mwaka 1978 kwa ajili ya kutoa mafunzo na kufanya utafiti katika Nyanja za Mahusiano ya Kimataifa, Diplomasia ya Uchumi, Itifaki na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Chuo hiki kinakabiliwa na changamoto kubwa ya Msumbiji kuacha kabisa ushiriki wa shughuli zote za uendeshaji na kutochangia chochote.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kubwa kwa mujibu wa Sheria za Mikataba ya Kimataifa, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kulifuatilia jambo hili ili kujua msimamo halisi wa Msumbiji kuhusu umiliki na uendeshaji wa Chuo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa ekari 1000 toka Kijiji cha Buma, Wilayani

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Bagamoyo ili kuepusha mgogoro unaoweza kutokea baina ya Serikali na waliokuwa wamiliki wa ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi inayosimamia Mpango wa Afrika Kujitathmini Kiutawala Bora – *APRM*: Tanzania ni miongoni mwa nchi 33 kati ya 54 za Umoja wa Afrika (*AU*) zilizojiunga na Mpango huu ambao unaipa dhima Serikali kusimamia majukumu ya nchi yetu katika kuratibu tathmini ya utawala bora hapa nchini, kwa mujibu wa mkataba na miongozo ya *AU/APRM* Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la *APRM* ni kusaidia Serikali za Afrika, Tanzania ikiwa mojawapo, kuhakikisha kuwa zinaimarisha Utawala Bora kwa kuwashirikisha Wananchi kubainisha changamoto za kufanyiwa kazi na mambo mazuri ya kuigwa na kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliarifiwa kuwa hivi sasa Ripoti ya Kwanza ya Hali ya Utawala Bora nchini imekamilika na maandalizi ya uzinduzi rasmi yapo katika hatua za mwisho ili utekelezaji wa mpango kazi wa miaka mitano wa kuondoa changamoto zilizobainishwa uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayoikabili Taasisi inayosimamia utekelezaji wa *APRM* ni ufinyu wa bajeti na kuchelewa kupatikana kwa fedha zilizotengwa kutoka Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha utaratibu wa kuipatia Taasisi hii Fungu lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu la Kamati la kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara zilizo chini yake, Kamati ilitekeleza Jukumu hili mwezi Aprili, 2013 kwa kuchambua Makadirio ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushiriano wa Kimataifa ina jukumu la kushughulikia Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Mabunge ya Afrika Mashariki, Afrika na SADC. Aidha, Kamati ina jukumu la kushughulikia taarifa za Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu hilo linazingatia na kuheshimu umuhimu mkubwa wa Diplomasia ya Kibunge. Utaratibu huu unatumiwa na Mabunge mengi duniani ikiwemo Bunge letu. Kwa Kanuni hizi ni rahisi kuona jinsi gani Bunge lako Tukufu ni miongoni mwa Mabunge mengi duniani yanayoheshimu na kuthamini nafasi yake katika kuwezesha ushawishi mzuri wa mambo ambayo ni ajenda ulimwenguni na kupendekeza hatua mbalimbali kuhusu masuala yanayojitokeza Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuthamini dhana hii, naomba kuwanukuu Spika wa Bunge la wawakilishi la Udachi, Mheshimiwa Frans W. Weiglas pamoja na Katibu Msaidizi wa Kamati ya Kudumu ya Ulinzi ya Bunge hilo, Bwana Gonnie de Boer waliosema kuwa : *“Alongside these development-orientated contacts, parliamentarians also meet quite regularly with colleagues from many different countries to discuss current affairs and their own institution’s working methods, for democracy is not a static condition - there is no real ‘end state’ that can be achieved. Parliamentary diplomacy, therefore, is also of great importance to provide periodically both developing as well as developed countries with a mirror to examine their own virtues and faults. Bilateral contacts can be used to discuss very concrete, urgent problems and perhaps to discover new ways of approaching them”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi maneno hayo yanaonesha kuwa, Katika Diplomasia ya Kibunge, Wabunge wanapokutana na Wabunge wa Mabunge mengine duniani husaidia kutoa fursa ya kujadiliana kuhusu mambo mbalimbali ya muhimu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Diplomasia hiyo imetumika pia kuboresha utendaji wa Mabunge mengi katika kusimamia Serikali zao, kuwawakilisha watu na Majimbo yao kwa ubora zaidi na kuongeza kukubalika kwa Taasisi za Ushirikiano miongoni mwa Serikali za nchi tofauti ndani ya nchi husika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linapaswa kuendelea na utaratibu wa ushirikiano na Diplomasia ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, katika kutekeleza jukumu linalohusiana na ushirikiano na Diplomasia ya Kibunge (*Parliamentary Diplomacy*), iliendelea kupokea na kujadili Taarifa za Wawakilishi wetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ACP – EU*: Bunge la pamoja kati ya Mabunge ya nchi za *ACP* na Wabunge wa nchi za Jumuiya ya Ulaya (*EU*) ni matokeo ya makubaliano ya ushirikiano wa Cotonue (*The Cotonue Partnership Agreement*), yaliyosainiwa mwaka 2000 kati ya nchi 78 za *ACP* na Bunge la Jumuiya ya Ulaya lenye nchi 27. Makubaliano hayo yalisainiwa Mjini Cotonue nchini Benin. Kati ya nchi 78 za *ACP*, 46 zinatoka Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, 17 kutoka Carribbean na 16 kutoka Visiwa vya Pasifiki. Wabunge hao kwa pamoja wanaunda Bunge linaloitwa *ACP/EU Joint Parliamentary Assembly*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipofuatilia uwakilishi katika *ACP/EU* ilibaini kuwa Ushiriki kwenye Bunge hili unapaswa kuendelezwa. Sababu kubwa ni umuhimu wake unaotokana na ukweli kuwa *ACP/EU* ni mahali ambapo sauti ya pamoja kwa nchi zinazoendelea inaweza kusikika. Vilevile ni katika chombo hiki, misimamo ya pamoja ya kuendeleza nchi za Afrika, Carribbean na Pasific inaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa hivi sasa nchi za Ulaya chini ya mwavuli wa Jumuiya ya Ulaya wanaendeleza mikakati ya kuzifanya nchi za *ACP* kuwa eneo la kupata malighafi kwa bei nafuu na kupata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)] soko kubwa kwa kupitia majadiliano ya EPA. Jukwaa la ACP linaweza kuzisaidia nchi hizi kuweka msimamo dhidi ya mbinu chafu kwa namna mbalimbali ikiwemo kuhimiza uhusiano wa kibiashara wa South-South na biashara kati yao (*Intra trade*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa Jukwaa Jukwaa la Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC – PF*) ni kupata sehemu ambayo Mabunge na Wabunge kwa ujumla wa Nchi Wanachama wanaweza kubadilishana uzoefu na mawazo ili kuimarisha mshikamano wa nchi husika kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Shabaha ya kuanzishwa kwa Jukwaa hilo kama ilivyoainishwa katika Mkutano wa Blantyre ni hatimaye kuwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC-Parliament*) kama ilivyo kwa kanda nyinginezo ambazo tayari zina Mabunge yao. Mfano wa Mabunge hayo ya Kanda ni *ECOWAS, EALA* na *AU*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Afrika (*PAP*) ni mojawapo ya Taasisi kumi za Umoja wa Afrika ambalo kati ya mambo yaliyojadiliwa katika kipindi cha mwaka 2013 ni masuala ya Amani na Usalama wa Bara la Afrika, Migogoro Barani Afrika pamoja na uwekezaji na unyakuzi wa ardhi wa Bara hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Bunge la Afrika linaendelea kushughulikia mapendekezo ya marekebisho ya Itifaki iliyounda Bunge hilo na mikataba mingine yenye Itifaki mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Afrika linaendelea kushughulikia mapendekezo mengine mahususi yanayohusu namna bora ya kudhibiti athari za tabia nchi na suala la ukimbizi na wakimbizi (*African Diaspora*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kikao cha kumi na moja cha Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
kushirikiana na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, iliwasilisha Bungeni Azimio la Kupongeza Tamko la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Azimio hilo ni jukumu la Kamati lililoainishwa katika Kifungu cha 7(2)(a) (ii) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Aidha, Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa Bunge lako Tukufu aliyoitoa tarehe 7 Novemba, 2013, ilibainisha msimamo wa Tanzania na kwamba Tanzania haitajitoa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati inaitaka Serikali kuzingatia kwa makini maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wakichangia Azimio lililowasilishwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mambo mbalimbali yaliyojitokeza, Kamati ina maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki yatekelezwe kwa ufanisi, Kamati inashauri:-

(i) Serikali iongeze kasi ya maandalizi ya Sera ya Taifa ya mtangamano na Mkakati wa Sera hiyo;

(ii) Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iimarishe mawasiliano na majadiliano baina yake na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, ili Sura ya Tanzania, kabla na baada ya kila Mkutano wa Bunge la Afrika Mashariki ionekane. Aidha, utaratibu huo uonekane katika Bajeti ya Wizara, Fungu 97;

(iii) Mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki uondolewe kwenye Bajeti ya Wizara ya Afrika Mashariki na kuwekewa utaratibu mwingine;

(iv) Kianzishwe kitengo cha utafiti chini ya Wizara hii kwa ajili ya kuainisha fursa katika mtangamano wa Afrika Mashariki;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

(v) Tanzania iendelee kusisitiza kuhusu utatuzi wa changamoto zilizopo katika utekelezaji wa Visa ya pamoja ya Utalii;

(vi) Tanzania iboreshe Miundombinu ya Bandari, Reli na Barabara na pia kuboresha huduma zinazotolewa na Bandari zetu; na

(vii) Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iratibu suluhisho na kero ndogo ndogo zilizopo Tanzania kuhusiana na mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza vyema majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Kamati inashauri:-

(i) Hali ya Balozi zetu kuhusu nyenzo za usafiri iboreshwe inavyopaswa kuwa.

(ii) Katika Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 Wizara ijipange kufanya ukarabati mkubwa wa majengo matatu ya Ubalozi wetu uliopo Stockholm – Sweden. Majengo hayo ni Jengo la Ofisi ya Ubalozi (*Chancery*) (Eneo la Nasby namba Alle 6 Taby), Jengo la Makazi ya Balozi (Residence) (Eneo la Vedettvagen Namba 35, Taby), Nyumba ya Afisa Ubalozi ambayo ina miaka sita bila kutumika. (Eneo la Masvagen, Namba 28, Taby).

(iii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ichukue hatua za haraka kujenga majengo iliyokusudia katika viwanja vyote ilivyopewa na nchi husika duniani.

(iv) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa iandae Mpango Mahususi utakaonesha mkakati wa kukarabati majengo yote yanayomilikiwa na Balozi zetu duniani.

(v) Kwa kuwa posho ya Utumishi nje ya nchi (*Foreign Services Allowance*) bado inawekwa katika Kasma

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
ya Matumizi Mengineyo (OC) na kwa kuwa fedha zinazotengwa kwa kasma hiyo ni kidogo, jambo linaloweza kusababisha fedha zote kutumika kwa masuala mengine, ni vizuri posho hiyo (*Foreign Services Allowances*) ikatengwa katika kifungu (*Item*) kingine kinachojitegemea.

(vi) Ili kuepuka aibu kwa Balozi zetu katika malipo ya huduma muhimu, Wizara iongeze juhudi itakayosaidia Balozi hizo kuwa na fedha za kutosha kwenye vifungu vya matumizi muhimu na ya lazima kama vile ankara za mawasiliano, ada za shule, mafuta ya magari na umeme.

(vii) Baada ya utaratibu wa mikutano ya Mabalizi kila mwaka tangu mwaka 2008, ni muhimu Wizara ikaandaa na kuhakikisha kuwa, mikutano hiyo inafanyika.

(viii) Kuna umuhimu mkubwa wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuliarifu Bunge lako Tukufu thamani halisi ya Jengo la *JN/ICC* katika maelezo hayo, Wizara ifafanue kiasi cha fedha kinachodaiwa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

(ix) Kamati inasisitiza na inashauri kuwa, utaratibu wa kutuma fedha za Balozi zetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa unapaswa kuboreshwa. Ili kupunguza urasimu usio wa lazima wakati wa kutuma fedha hizo, pamoja na kuzingatia misingi bora ya uwajibikaji kwa matumizi ya fedha, Kamati inaishauri Serikali kuwa, Hazina ipeleke fedha za Balozi zetu moja kwa moja bila kupitishia Wizarani, kama vile utaratibu unatuomika kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Diplomasia na Ushirikiano wa Kibunge ni jambo muhimu na linaweza kuwa na tija zaidi kwa Taifa kama suala hilo litaboreshwa kiutaratibu. Kamati inashauri kuwa:-

(i) Vyama vyote vya Kibunge viwekewe utaratibu maalumu utakaowawezesha Waheshimiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
Wabunge kuelewa kinachoendelea na kufuatilia mambo ya msingi.

(ii) Inapotokea Waheshimiwa Wabunge wametembelea Mabunge ya nchi nyingine, uwekwe utaratibu wa Wabunge hao kutoa Taarifa kwa namna itakayosaidia Bunge kubaini mambo ya kujifunza kutoka katika Taarifa hizo.

(iii) Kabla ya Wawakilishi wa Bunge letu kuondoka kwenda kuhudhuria Mikutano ya Vyama vya Kibunge, ni vyema wakutane na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa niaba ya Bunge letu ili kupeana changamoto zilizoko katika Balozi hizo.

(iv) Uwekwe utaratibu mzuri zaidi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kuhusiana kikazi na Bunge la Tanzania.

(v) Kutokana na Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye Vikao vya Bunge la Afrika hususan kuhusu migogoro ya ndani ya nchi za Afrika, Serikali yetu ijifunze kwa kuimarisha uwekezaji katika Sekta zinazoweza kuibua ajira kwa vijana.

(vi) Bunge liitake Serikali kuainisha Mikataba, Itifaki na Makubaliano ya Kimataifa yaliyosainiwa ambayo hayajaridhiwa na Bunge na kuyatolea maelezo kwa Bunge lako Tukufu kwa kueleza sababu za kutoridhia mikataba hiyo ili Bunge liweze kushauri ipasavyo.

(vii) Ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuelewa vizuri kinachoendelea kufanyika katika Vyama vya Kibunge ambavyo Bunge letu ni Mwanachama, utaratibu wa kutoa taarifa kwa Bunge unaweza kuboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kutegemea Taarifa ya Kamati hii, yenye mambo zaidi ya ushirikiano wa Kibunge, inawezekana kuamua kuwa katika kila mkutano

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]
mmojawapo wa Bunge, itengwe siku moja ya kujadili masuala ya Ushirikiano wa Kibunge. Kwa utaratibu huo, Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa itakiwe kutoa taarifa na maoni yake ya jumla na wawakilishi wa kila chama watakiwe kueleza shughuli zao za mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Edward Lowassa, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia mwezi Novemba, 2013. Tunaamini kuwa, fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuchukua nafasi hii kuitambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, kwa jinsi inavyosimamia heshima na hadhi ya Tanzania katika masuala ya uhusiano na ushirikiano wa Afrika Mashariki na Duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Ndugu Athumani Hussein, Ndugu Ramadhani Issa na Ndugu Nesta Kawamala, Makatibu wa Kamati hii, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati kwa kipindi chote na kufanikisha taarifa hii kwa wakati. Nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashillillah, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu, liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kuyakubali Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. S. NKAMIA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana, umeisoma vizuri sana na nina hakika *BBC* imepoteza mtangazaji mzuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wachangiaji saba, tutaanza na Mheshimiwa Masoud Salim na ajiandae Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Msabaha, Mheshimiwa Buyogera, Mheshimiwa Mwanjelwa na tutamalizia kipindi cha mchana na Mheshimiwa Kabati!

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia Taarifa za Kamati zetu mbili, yaani Kamati ya Ulinzi na ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nami niungane na wenzangu kutoa pole kwa Walimu, Wanafunzi na Uongozi wao wa Vyuo Vikuu viwili Zanzibar kwa ajali iliyotokea. Pia nawashukuru Wanafunzi na Walimu wa *UDOM* kwa ushirikiano ambao wameuonesha sambamba na kuwashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano ambao umeonekana wa hali ya juu pamoja na Serikali zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar, kwa kutoa ndege mbili za kuwasafirisha majerushi wote na wengine wote. Kutoa ndege mbili ni gharama lakini mmefanya wajibu wenu na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na nitakuwa naboresha kidogo tu kwenye Hotuba hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la Wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Wastaafu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

wa Jeshi la Polisi. Hali zao ni mbaya na inaonekana hata ile *pension* ambayo wanapata askari wa zamani waliostaafu ni ndogo sana na haikidhi hata maisha ya muda wa siku kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao ni askari ambao wamefanya kazi zamani, haikuwa bahati mbaya au haikuwa jambo la laana kufanya kazi mapema baada ya Uhuru au baada ya Muungano, lakini wamefanya kazi kubwa na nzuri na ya mfano wa kuigwa, lakini Wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Askari wa Polisi, pensheni yao ni ndogo sana. Mimi nadhani ieleweke kwamba, Maafisa wa Jeshi Wastaafu na wale wa *rank* nyingine wa miaka iliyopita, tofauti ya miaka minne au mitano tu, ukiambiwa tofauti zao za pensheni unaweza kulia, wanapitana sana kupita kiasi.

Ushauri wangu kwa Serikali, watu hawa tusiwadharau, tusiwabeze, tusiwanyanyase, tuandae mazingira mapya ya kuweza kuboresha pensheni zao. Mfumo wa pensheni wa Wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Mfumo wa pensheni kwa Askari wa Polisi wale wa zamani na wa sasa basi uandaliwe vizuri; vinginevyo, kumbe kufanya kazi zamani katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania ilikuwa ni laana kubwa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, tumesema mara nyingi tangu enzi ya Mzee wetu Malecela na ninampongeza sana, enzi ya Mheshimiwa Kusila, Mheshimiwa Masilingi pamoja na Mheshimiwa Lowassa na leo hii tukiwa na Mama Anna Margareth Abdallah. Hili naomba lifahamike vizuri zaidi na liboreshwe juu ya mfumo wa pensheni kwa Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Wastaafu wetu na Mapolisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni alama za *beacons*. Taarifa zimeeleza kwa wasomaji wote wawili ambao taarifa zao ni nzuri sana, nianze na ile ya Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, ameelezea suala zima la *beacons*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

Suala la *beacons* limekuwa likilalamikiwa muda mrefu na kwa kuwa suala hili lipo mipakani baina ya nchi na nchi na marafiki tunaopakana nao tunawaelewa. Sasa ukakasi huu na kigugumizi hiki kwa kuwa suala hili kama lilivyoelezwa ni mtambuka, Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini Wizara ya Ardhi, Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Mambo ya Nje ya Mheshimiwa Benard Membe, Wizara hizi tatu kwa pamoja na nchi husika ambazo tumepakana nazo; aliyepelekea mpaka kutoroshwa kwa *beacons* ni nani zaidi? Ni nchi zipi husika?

Naomba watakapofanya majumuisho watueleze hili na Serikali pia ni vyema ituambie hili. Nitoe mfano tu baina ya Tarime - Tanzania na Migori - Kenya, kuna Vijiji vya Kirongwe, Ikoma, Panyakoo, Ruchee, Kagoja na Nyamuhunda, zimeng'olewa zamani kwelikweli. Mheshimiwa Benard Membe, Waziri wa mambo ya Nje, miaka na miaka tunapiga kelele tangu enzi ya Mzee John Malecela, lakini hadi leo naona kuna kigugumizi. Ni nani aliyekwamisha; ni nchi gani? Mtuambie sasa!

Misenyi - Uganda kuna Vijiji vya Kakunyu, Bugango, Bubale, Mtukula, Minziro na Kashanze nako ni vilevile, majirani zetu ndiyo hao anajua Mheshimiwa Samuel Sitta, mambo yanavyokwenda na michakato tunayokwenda nayo. Mimi nafikiri na Tunduma hata *buffer zone* haijulikani, sawa utamaduni upo wa kuoana hata na Machifu lakini suala la mipaka ni kubwa na kila tukienda mbele naona kuna mambo yanaibuka ya majirani zetu. Naomba sana Serikali na wale wenzetu walitoa taarifa zao mbili, watuambie sasa ni mikakati gani ya Serikali kwa hali tunavyokwenda hivi sasa na majirani zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siku ya Mashujaa; mashujaa hawa tunawakumbuka kwa kazi nzuri walizopigania vita mbalimbali kama Kagera ambapo wale waliofariki walizikwa Kaboya na wale tuliowapeleka Msumbiji vilevile tulichimba mifupa kwa gharama kubwa tukaileta Naliendele Mtwara tukazika kwa mamilioni ya shilingi. Tunasahau wake zao wajane, wanatangatanga,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

wanahangaika na wanakufa kwa njaa. Watoto wa mashujaa wale vilevile hawakupata elimu kwa sababu wazazi wao walikufa kwenye vita. Je, kuwapeleka vitani ilikuwa ni laana?

Tunapiga kelele siku nyingi kwamba ni kwa nini wajane mmewaacha wanatangatanga muda mruu wanaombaomba, sisi tunasema tunawaenzi, tunamuenzi nani? Mifupa tumeshachimba na tumeshazika huku kwetu Naliendele Mtwara lakini je, wale wake zao, wajane na watoto wao kwa sababu hawakupata elimu na umaskini unazidi. Kumbe waliokwenda vitani bado hatujawaenzi, sisi tunawaenzi baada ya kuwaenzi tunakwenda kujipatia vitamuvitamu na kuku watamuwatamu lakini wajane je? Waziri nadhani uko makini sana, simuoni Waziri wa Ulinzi sijui yuko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili naomba sana tukae vizuri na Kiongozi wa Serikali naona yuko makini, wale Wanajeshi tuliwapeleka vitani wakafariki, wajane wale hali zao ni mbaya, watoto wao hawakupata elimu kwa sababu tuliwapeleka na ni mashujaa. Sasa tunasema tunawaenzi, tunawaenzi vipi wakati hali zao ni mbaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo lilikuwa ni jambo lingine. Kuboresha majengo yetu ya Ubalazi limesemwa, lakini nataka nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Jengo Namba 19, Uingereza, tumepewa *notice* kwamba, kama hatukuliendeleza watatunyang'anya. Tuelezwe hali ilivyo sasa; je, tuna mpango gani wa kulikabili hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahamiaji haramu limeelezwa na mimi niseme tu nawaomba Watendaji wa Vijiji vya mipakani vya Kigoma na Kagera na hasa Karagwe kwa Mheshimiwa Blandes, Watendaji ambao wana tabia mbaya baada ya kazi kubwa iliyofanywa na Serikali na Kamati zetu za Ulinzi wanapokea rushwa na kuwarudisha kinyemela wahamiaji haramu, nasema kwamba Serikali iwe makini sana na suala hili, watatuweka mahali pabaya sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

Watendaji wa Vijiji na Vitongoji wa Mikoa hii ni lazima wakae vizuri waweze kukubali kwamba kazi iliyofanywa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara kuchelewa ya baadhi ya Mabalazi wetu na watendaji wao ni jambo ambalo siyo zuri, wanaombaomba na baadhi ya wanafunzi mashuleni wanafukuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na mtoa taarifa, hili nalo alichukue na tulifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kwamba, ziara ya Mheshimiwa Xi Jinping tumefaidika na nini? Usafi ulikuwa mkubwa kweli na harakati zilikuwa ni kubwa, mliinamisha vichwa vyenu mkatia saini tu halafu magazeti yakaandika mafanikio makubwa. Rais Barack Obama mafaniko makubwa ni yapi baada ya usafi tuliouona, mtuambie leo hapa Watanzania wapate kusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie moja la mwisho, suala zima la miito ya moto ya uongo. Naomba sana wale wanaopiga simu wakawapigia watu wa Zimamoto, Zimamoto wakahangaika wakaenda katika maeneo na tukio halipo, tabia hii tuiache kwani hasara inakuwa ni kubwa mno kupita kiasi na wakati mwingine wanapigiwa simu wanasema simu hizi za miito ya moto inakuwa ni ya uongo. Naomba sana Watanzania tabia hii tukae vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji wa kesi; jamani hili suala limekuwa ni kubwa sana kwani kunakuwa na msongamano mkubwa sana magerezani, mtu anakaa miaka mitatu mpaka mitano kesi yake haiendi. Tatizo gari ni mbovu, hakuna mambo mengine mbalimbali na taarifa ya haki za binadamu zinaeleza kwamba Tanzania imechafuka kwa sababu ya msongamano wa mahabusu wanaofungwa magerezaji, lakini zaidi ni ucheleweshaji wa kesi. Rais amesema ni lazima kuwepo na adhabu mbadala lakini kunakuwa na kusuasua. Namwomba Mheshimiwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

mtoa hoja akija hapa atuambie hasa ukizingatia kwamba Tanzania sisi upo kwenye APRM. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Machali na ajiandae Mheshimiwa Chilolo!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye hoja za Kamati mbili.

Mchango wangu utajikita sana kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa kuwa ukiangalia kuna baadhi ya *issues* ambazo ni muhimu kama Taifa tukaziangalia kwa mapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niwapongeze Kamati zote mbili kwa taarifa zao, wame-*address issues* mbalimbali. Moja kwa moja nianze kwa kuwaomba Kamati za Ulinzi na Usalama ziharibu kufanya ziara kwenye Wilaya mbalimbali hapa nchini ili kujua hali za usalama kwenye Wilaya zetu ikoje. Inawezekana kweli wamekwenda katika baadhi ya maeneo lakini kwenye maeneo mengine ni imani yangu watakuwa bado hawajafika ndiyo maana tuna changamoto nyingi zinazotukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika Wilaya mbalimbali kuna Kamati ambazo tunaziita Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na kuna Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa. Naomba niseme kwamba, baadhi ya Kamati za Ulinzi na Usalama kwenye Wilaya zetu ndiyo chanzo cha vurugu na matatizo katika nchi yetu. Kwa sababu baadhi ya mambo ambayo wakati mwingine wanayaamua, haiingii akilini kabisa kwamba, kwa mtu mzima tena wengine wanajiita wasomi na mambo ambayo wanayafanya utajjuliza hivi huyu ni mtu mzima kweli ana akili ameamua hiki!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano katika hili kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Kasulu. Nilishafika mahali pengine nikasema mbele ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani akiwa amefanya ziara kwetu. Imefika mahali Wabunge wa Wilaya ya Kasulu hatuna imani na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kasulu inayoongozwa na Mkuu wa Wilaya, Bwana Danhi Makanga, kwa sababu vitu ambavyo vinafanywa havi-*make sense*.

Nitatoa mfano mmoja, tangu mwaka 2005 kumekuwa na *flow* kubwa ya mifugo ambayo inaingia katika Wilaya ya Kasulu Mkoa wa Kigoma. Mifugo hiyo inakula mazao ya watu, wakulima wanalalamika lakini Mkuu wa Wilaya amekuwa ni mtu wa kuwa-*favour* wafugaji sana na kuwapuuza wakulima. Kwa nyakati tofauti sisi kama Wabunge, baada ya Wananchi wetu kuja kutulalamikia tumekuwa tukienda wakati mwingine tunashauriana na *DC* huyu, lakini hatua hazichukuliwi. Imefika mahali kwa kuwa Mkuu wa Wilaya ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, mkulima anapokuwa pengine mazao yake yameliwa na mifugo, akienda kufungua shauri Polisi, Polisi wanakataa hata kufungua kesi.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani atakuwa shahidi kwa sababu alielezwa tarehe 23 Julai, 2013 wakati amefanya ziara katika Wilaya ya Kasulu na akazungumza na Wananchi wa Jimbo la Kasulu Mjini. Alielezwa mambo haya na watu walijitokeza wakapigwa, wakavunjwa mikono, wametokea mbele yake wakiwa na *POP*. Sasa najjuliza ni Kamati gani ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ambayo inaweza ikawa *biased* kwa kutoangalia kwamba pia kuna haki za wafugaji lakini pia kuna haki za wakulima? Hii *biasness* inatoka wapi? Naomba Serikali katika hili tujaribu kuangalia; vinginevyo, niseme kwamba, Serikali kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya ni vyombo ambavyo vinachochea vurugu miongoni mwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili katika hilo, kuna eneo moja ambalo Wananchi wa Wilaya ya Kasulu, Mkoa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

wa Kigoma, wamekuwa wanalima katika eneo moja ambalo Serikali wanasema kwamba ni eneo la Hifadhi ya Msitu wa Makele Kusini. Sisi kwetu tunajua ni eneo la Kagenda Nkanda wamekuwa wanalima. Leo hii ni zaidi ya miaka 30 Wananchi wale wamekuwa wanalima katika maeneo yale. Sasa swali linakuja; wakulima hawa wanaambiwa waondoke katika yale maeneo wanaambiwa ni maeneo ya hifadhi; hivi Serikali kupitia vyombo vyake *whether* ni kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwenye Idara ambazo zipo Wilayani kwenye Halmashauri zetu, walikuwa wapi kwa zaidi ya miaka 30 wasiwazuie hao watu kwamba waliingia kwenye Hifadhi?

Tujiulize pia mwaka 2004 Mwenyekiti wa Halmashauri wakati akiwasilisha Taarifa yake kwenye Kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama Desemba, 2012 ambapo Waheshimiwa Wabunge tulialikwa kwenye kikao hicho, akasema Charles Keenja, aliyekuwa Waziri wa Kilimo na Chakula wakati wa utawala wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alipofanya ziara Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kasulu, aliomba wamwoneshe mashamba ya mfano, Serikali ikampeleka kwenye eneo hilo akaona mashamba.

Mwenyekiti anaendelea kueleza kwamba, Waziri akashauri, baada ya kuona kuna mazao mengi, kuna mahindi yamestawi vizuri, kuna maharage, akasema kwa nini msiwahamasishe Wananchi wakaja hata maeneo mengine ambayo bado hayajawa mashamba wakalima tukapata chakula cha kutosha. Ni *challenge* ambayo aliweza kuitoa na Mwenyekiti akasema kama ni makosa yamekuwa ni makosa ya Serikali, lakini hata hivyo, tujiulize wanasema hii ni Hifadhi ya toka mwaka 1955, ukiangalia *population* ya mwaka 1955 ya Wilaya ya Kasuru na Mkoa wa Kigoma ni wazi kwamba, leo hii watu wameongezeka sana. Ongezeko la watu ni lazima liende sambamba na suala la uhitaji wa ardhi, haihitaji mpaka mtu pengine uwe na *PH.D*, uwe Profesa au ukae usome kwanza ujue watu wameongezeka wanahitaji ardhi kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao mbalimbali za kiuchumi hususan kilimo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo gani eneo hilo leo hii pengine Serikali ikasema ngoja isogeze mpaka ili Wananchi wale wapate haki kama ilivyo katika maeneo mengine. Serikali imefanya juzi walipopiga kelele kule nafikiri ni Ngorongoro, Wananchi wameachwa. Naomba uamuzi uliofanywa kule pia uende ukafanywe Kasulu; vinginevyo, Serikali niseme kwamba ni wachochezi wakubwa wa vurugu. Mbaya zaidi, Mkuu wa Wilaya aliahidi mwaka juzi wakati Mheshimiwa Ezekiel Maige akiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwenye kikao ambacho alikuwa anahitimisha ziara mwaka juzi mwezi Novemba baada ya kumaliza Bunge tulifanya ziara kule.

DC akaahidi akasema, ardhi katika Wilaya ya Kasulu na Mkoa wa Kigoma ipo ya kutosha, kwa hiyo, atatafuta mashamba mbadala ili Wananchi wale wakulima wasiende kulima kule. Naomba niseme, huyu Mkuu wa Wilaya, Bwana Danhi Makanga ni mwongo, mpaka leo hajafanya jambo lolote. Tumelalamika sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu tumemweleza na Waziri wa Ulinzi tumemweleza na hata TAMISEMI wana taarifa, lakini hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa. Kwa nini wanawadanganya Wananchi au ndiyo Utawala ambao mnatupatia CCM; mnawaahidi watu halafu hakuna kitu chochote ambacho mnafanya! Toka mwaka 2011, juzi Kamati ya Ulinzi na Usalama inawaelekeza watu waende kufyekewa mazao; vitu gani hivi kama siyo uchochezi wa vurugu?

Umewaahidi utawatafutia ardhi mbadala, hakuna ardhi yoyote toka mwaka 2011 mpaka leo. Kamati za Ulinzi na Usalama zinafanya vitu gani kama siyo wachochezi wa vurugu; na kuna sababu gani za kuwalinda Wakuu wa Wilaya kama Danhi Makanga na watu ambao wako chini yake? Watu wana mazao yao yanaharibiwa wanaenda kuripoti Polisi halafu Jeshi la Polisi linakataa kufungua mashauri; kwa nini?

Kamati za Ulinzi na Usalama zipo pale kwa ajili ya kuwagandamiza baadhi ya wakulima tu, hawa Wakuu wa Wilaya kazi zao ni nini? Inafika mahala mpaka wana-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM]

overlook wanakwenda kuingilia kazi nyingine wanapaswa waelewe kwamba, Wabunge ni Wawakilishi wa Wananchi. Lazima tuseme na ndiyo kazi yetu atakayekuuliza umetumwa na nani, nimetumwa na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo halijakaa vizuri, naiomba Serikali *i-take serious note* katika hili; vinginevyo, siku moja kama mtasikia kuna vurugu zimechochewa mjue chanzo ni Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa sababu jambo hili hawalichukui katika *broder perspective*, watu wanafikiria, watu wameongezeka, sasa tunafanyaje, Kamati ya Ulinzi na Usalama kazi yake ni kutumia hizi *cohesive apparatus*, Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo lakini ni imani yangu kwamba Serikali imeona umuhimu wa suala hili, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Chilolo, ajiandae na Mheshimiwa Lema!

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nichukue nafasi ya awali kabisa, niwapongeze Waheshimiwa waliowasilisha Taarifa za Kamati zote hizi mbili; Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Nkamia, wameni-*impress* sana sana. Nimeona kweli Wenyeviti wamewaandaa vijana, basi kama wapo wanaoandika Benki ya Viongozi chukueni majina hayo vijana wameshaiva Taarifa hizi wamewasilisha vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sitasita kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati, mama yangu Mheshimiwa Anna Abdallah, amefanya kazi nzuri, taarifa yake ni nzuri sana, imeandaliwa vizuri kabisa, ninaamini kama Serikali itaamua kuifanyia kazi, ufumbuji unaweza ukapatikana na nchi yetu ikaenda vizuri kabisa. Vilevile naipongeza Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Edward Lowassa, ni nzuri sana,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DIANA M. CHILOLO]

ninaamini Mawaziri wetu wasikivu, Mheshimiwa Membe yuko pale, akiichukua Taarifa akaifanyia kazi kama kawaida yake, mambo yatakuwa mazuri kabisa kabisa. *(Makofi)*

Baada ya pongezi hizi, naomba sasa na mimi niungane na Kamati au nitoe mawazo yangu ambayo ninaamini Mawaziri Vijana hawa watayafanyia kazi vizuri.

Nikianza na suala la madeni ya Wazabuni wetu kwenye Magereza, jamani Kamati imesema kuna madeni mengi ya wazabuni wetu, watakata tamaa watashindwa kusaidia Magereza yetu. Hawa watu wa Magereza, Wafungwa, lazima wale, wapate lishe nzuri, kama wazabuni wetu hawalipwi, Mwenyekiti hapa hajaandika tu ni shilingi ngapi naamini ni mabilioni mengi.

Mheshimiwa Dkt. Nchimbi, wewe ni mchapakazi, wewe ni mbunifu, wewe ni mchachalikaji, tatua hilo ili wafungwa wetu waendeleo kupata chakula, kwa sababu chakula ni wajibu lazima wale lishe inayotakiwa. Naomba kero hiyo isibakie tena kwenye masikio yetum ninaamini hiyo utaimaliza, nakushukuru sana Mheshimiwa Nchimbi kwa sababu wewe ni msikivu. *(Makofi)*

Naingia hoja nyingine; msongamano wa wafungwa na mahabusu. Ndugu yangu mimi mwenyewe na Kamati yangu ya UKIMWI tumefika kule, msongamano ni mkubwa lakini uwezo wa kupunguza msongamano upo. Kamati imekuainishia na wewe mwenyewe unafahamu na mimi nakuongezea. Mheshimiwa Nchimbi, kesi haziendi, Mahakimu wetu mmepeleka vijana wasomi wa Chuo Kikuu, hawana usafiri. Mahakama ya Mwanzo unampa Hakimu mmoja Mahakama nne, hana usafiri, atafanyaje kazi huyu! Ninaomba muwaangalie hawa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, wapeni usafiri ili waweze kufanya kazi, bado wana nguvu sana hawa vijana lakini hatujawawezesha. Ninakuomba sana Mheshimiwa Nchimbi uwasaidie vijana hawa waweze kufanya kazi, msongamano utapungua kama kesi zitaenda.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DIANA M. CHILOLO]

Kingine, hawa Majaji mnawatengea pesa ndogo za kuendesha kesi, wanapokuwa na pesa ndogo wanashindwa kuendesha kesi. Wakati huu ndiyo wa kuandaa bajeti, nakuomba unapoingia kwenye *Cabinet* nenda na wewe ukaibane Serikali yako ikuongeze pesa ili Majaji uwape fungu la kutosha kuendesha kesi, kesi zipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, hiyo Kamati ya *Parole* hivi mwaka huu imewatoa wangapi? Mheshimiwa Rais, nampongeza sana, amewatoa watu karibu 1,900 na zaidi, amefanya kazi nzuri. Kati ya hao wapo wanawake wanaonyonyesha na wajawazito, amewatoa Mheshimiwa Rais, mimi nampongeza sana na watu mbalimbali wenye matatizo mbalimbali. Kamati yetu ya *Parole* nayo ifanye kazi basi ya kupunguza wafungwa humo ndani ambao wana haki ya kusamehewa wasamehewe na kama tungekuwa tunapata taarifa au utakapopata muda ukituambia, Kamati hiyo kwa mwaka huu tu sitaki miaka mingi, imewatoa wangapi nao utakuwa umetusaidia sana. Hizi ni mbinu ambazo zinaweza zikasaidia kupunguza wafungwa na siyo hivyo tu, kifungo cha nje hata kesi ya kuku mtu anakaa humo ndani kufanya nini, kesi zingine ambazo siyo za lazima huwezi kukaa humo ndani wakae nje huko. Waende asubuhi wakafanye kazi warudi nyumbani au raia wawatazame huko watajibadilisha wenyewe tabia zao. Wataona majirani wanavyowaona, wanavyowatazama vibaya, watajibadilisha wenyewe tu. Nakuomba sana Mheshimiwa hili ulifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea, kingine ninapenda nizungumzie kuhusu Balozi zetu za nje. Balozi zetu za nje ndugu yangu Mheshimiwa Membe, kweli tunakokwenda hata ule ukarimu wa kusema jamani leo nimepata wageni tutapata *lunch* pamoja na wageni wametoka Tanzania kuna Wabunge wameingia au tutapata *dinner* haupo, kwa sababu hawana fedha, *OC* mnazowapelekea ni ndogo mno hata kupokea wageni *Airport* wanashindwa kuandaa hata basi la kupokea wageni kwa sababu fedha hawana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DIANA M. CHILOLO]

Mimi naomba sana Balozi zetu tuzitazame kwa jicho la huruma, tuwatengee fedha, majengo mengine kama Kamati ilivyosema, yamechakaa mno. Nilikwenda China, majengo yamepasuka, mtu anaweza kuchungulia akaona mpaka ndani. Wakarabatieni ofisi zao ndugu zangu ili waweze kufanya kazi kwa amani, wanashindwa kuja hata likizo hawana fedha, watumishi wachache hata kujigawa nani aende likizo nani abaki wanashindwa. Hivi matatizo haya mbona yanaweza yakasawazika jamani! Kuajiri wengine tunashindwa nini, tuwapelekeni na watu wengine wakafanye kazi huko, wasomi tunao wengi wenye uwezo. Mimi naomba sana, haya yapo chini ya uwezo wako, yafanyie kazi yapate ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu Magereza. Magereza zetu zinajitahidi sana kujitegemea, wanalima wenyewe, chakula wanajitafutia wenyewe, wana ufundi seremala, lakini Serikali mnashindwa kuwapelekea hata vifaa jamani, kama hamuwezi kuwapelekea bure basi wakopesheni, mkiwadhamini muwakopeshe. Nendeni Manyoni pale wanalima mahindi mahekali kwa mahekali, wanajilisha wenyewe, wana useremala, wanatengeneza vifaa vingi wanauza wanapata hela za kula wenyewe. Wapelekeeni vitendea kazi, kama hakuna vya bure muwadhamini wakopeshwe waweze kujitegemea vizuri zaidi na waweze kuzalisha zaidi. Bila kuwasaidia kwa kweli tunawanyima pato ambapo hakuna sababu ya kukosekana pato.

Nashukuru sana, naunga mkono hoja zote mbili, nategemea kupata majibu mazuri kabisa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Lema, ajiandae Mheshimiwa Buyogera!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa nasikiliza kwa makini sana Hotuba zote mbili na nilisikitika sana kwamba, ulinzi na usalama haupo kwenye vile vipaumbele sita.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Hotuba hii ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, unaona kuna mkanganyiko wa fikra. Taifa letu lipo kwenye wakati mgumu sana na hata kwanye maazimio yaliyosomwa kuhusu Bomu la Olasiti Kanisani, hilo limethibitisha, lakini chokochoko za udini na ukabila kimsingi zimeletwa na Wanasiasa, hapo nyuma hazikuwepo kabisa na kwamba zimetoka wapi; ni kwamba, zimeletwa na Wanasiasa pale wanapotafuta nafasi za utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tukio lilitokea Arusha na hata nilikuwa naongea na rafiki yangu hapa Mheshimiwa Msigwa, namwambia ninashangaa inawezekana vipi wakasema Waziri aliyeshindwa ku-*perform* kwenye Wizara ya Maji ama Kilimo ni mzigo, lakini Naibu Waziri aliyehudhuria kwenye kikao cha kueneza siasa za ukabila hatajwi kama mhalifu kabisa wa kwanza Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo *DVD* ya Naibu Waziri wa Ardhi, akiwa kwenye kikao cha ukabila wakati wa Kampeni za Udiwani Arusha Mjini na wakatoa maazimio ya kuwapa wageni sumu, kuwapiga mishale na kuwapiga mikuki na wasiuziwe mashamba, yaani wenyeji wa Mkoa wa Arusha wasiuze mashamba kwa wageni. Kikao hicho alisimamia alikuwepo Naibu Waziri wa Ardhi, taarifa hizo nilipeleka Kituo cha Polisi, nilipeleka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya, OCD John Mongela, nikamwambia jambo hilo akakiri amelisikia, ameliona na analifanyia kazi, lakini mpaka leo katika wale Mawaziri sita waliotajwa saba mizigo, Mheshimiwa Ole-Medeye siyo tu ni mzigo ni bomu ambalo likiendelea kuachwa hivi, kwamba, Naibu Waziri anakaa kwenye kikao cha ku-*insight tribalism* kwa sababu tu Chama chake kishinde Uchaguzi. Taifa hili litakwenda mahali pabaya sana, ndiyo sababu nasema wanaochochea Siasa ya Udini na Ukabila siyo Waislamu na Wakristo walioko Makanisani ni Wanasiasa wanaotafuta nafasi za kuongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipigwa bomu Soweto wakati wa kufunga kampeni zetu za Udiwani na kwa bahati

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

mbaya sana kwenye kitabu hiki hakuna jambo hilo limeandikwa hata moja. Chama chetu kimesema na mimi narudia kusema, tuna ushahidi wa watu waliorusha bomu katika Mkutano wetu wa kufunga pale Soweto. Hatusemi Serikali yote imefanya hivyo, lakini kuna watu ndani ya Serikali wanataka ku-*sabotage* Serikali. Vilevile kuna watu ndani ya Serikali wanafanya kazi karibu na shetani, kwa hiyo, wakipata ushawishi wa shetani wanaweza wakafanya vitendo ambavyo si vya kiungwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema tuna ushahidi na tukaomba Mheshimiwa Rais aunde Tume ya Kikatiba tupeleke ushahidi wetu kwake, jambo hili kwenye hiki kitabu hakuna na ushahidi huo wa *video* tunao, ambao ungeweza kuithibitishia Serikali na kusaidia watu wa Usalama waweze kubaini nani aliyefanya kile kitendo. Badala yake nini kimekuwa kikifanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikamatwa jambazi Nzega akapigwa sana, akaambiwa ataje yeye ndiye aliyerusha bomu la Olasiti na alipewa bomu na Mheshimiwa Mbunge Lema. Nilipigiwa simu na ndugu wa huyo jambazi aliyekamatwa Nzega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine huwa sisahau sala na dua kila ninapoamka, nafikiri hilo suala lilipita hewani kwa sababu nilimwomba Mungu. Wamekamatwa vijana wengi wanapigwa, hawapigwi kuulizwa chochote, wanapigwa kuulizwa kama waliona, kama kuna *video* au *CD*. Watu wamenyang'anywa simu zao, watu wamenyang'anywa camera zao kuonekana kama unajua nini kuhusu ama una picha gani kuhusu bomu la Soweto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yakiendelea, sisi ni binadamu, tunavyotaka kuuwawa kwenye bomu halafu inatokea watu wanasema tulijirushia bomu halafu tukakemea vipande vya mabomu! Sasa sijui ni kwa jina la Mwenyezi Mungu ama, visitufikie sisi tunaumia, ndugu zetu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

wanaona, rafiki zetu wanaona, wanachama wetu wanaona. Katika yote leo bomu ambalo limetajwa hapa ni bomu la Kanisani la Olasiti ambalo pia lilileta maafa makubwa, lakini bomu la Soweto halikutajwa hapa. Sisi tunasema, tuna ushahidi nani alitaka kutuua hatujasema ni Mwenyekiti, ni Spika ama ni nani, tunasema tuna ushahidi, Serikali iunde Tume tupeleke ushahidi wetu ukaonekane ni wa ukweli ama si wa ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nimekiona kwenye hili ni maandamano, hakuna maandamano rasmi. Nimeshangaa hiki kitabu kinasema sasa lazima kuwepo na utaratibu wa maandamano. Maandamano siyo tukio rasmi, ni tukio la ghafla kwa sababu yanasababishwa na *event* ambazo zinatokea ghafla. Sasa tukianza kuwa na maandamano rasmi maana yake tutakuwa na ratiba ya maandamano. Maandamano ni matukio yanayosababishwa na matukio kutokea.

Sasa hapa naona kama Serikali ina-*propose* kwamba iundwe sheria ya kuwatengenezea njia waandamanaji waandamane siku gani, saa ngapi na wapi; hayo siyo maandamano, hayo yatakuwa ni mazoezi ya kupiga vita kisukari. Maandamano ni tukio ambalo unaandamana kupeleka ujumbe na unapoandamana kupeleka ujumbe huchaguliwi njia, unachagua njia ambayo ujumbe utafika. Sasa kama mnataka tuanze kufanya mazoezi ya kuzuia sukari mwilini, hiki kitabu pale mlipo-*propose* hiyo itafaa. Niseme kwamba, hilo pia naunga mkono, lakini kwamba maandamano rasmi, huwa hakuna maandamano rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni maisha ya maaskari wetu, mishahara yao ni midogo sana na makazi yao ni mabovu sana. Maaskari wangu Arusha wanaishi kwenye nyumba ambazo tunaziita ni *hot pot*, wanaishi maisha magumu, mishahara migumu na hawa ndiyo wanapewa majukumu makubwa hasa kipindi hiki ambapo Dunia imevamiwa na Ugaidi, wanapewa majukumu makubwa, kazi kubwa ya kwenda kufanya utafiti kwenye

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. GODBLESS J. LEMA]

mazingira makubwa yanayohusisha watu wenye pesa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama leo ulinzi na usalama siyo kipaumbele katika vile vipaumbele vya nchi; unaweza vipi sasa ukazuia Ugaidi, ukazuia uhalifu mwingine wakati polisi wetu, askari wetu, wanaishi maisha magumu, maisha ya tabu, maisha ya ajabu? Mshahara wa polisi wa mwaka mzima huyu wa chini hauwezi kufikia mshahara wetu na posho yetu, yaani mshahara wangu na posho yangu ya miezi sita ni sawa sawa na mshahara na posho ya huyu polisi wa chini wa miaka 50. Kwa hiyo, maisha yao ni magumu na pia yanasababisha wao kushindwa kufanya *investigation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Ulinzi na Usalama, lazima pia tuangalie maisha ya polisi wetu wanaishi vipi. Polisi wa Tanzania wanaishi maisha magumu sana, wamekuwa ombaomba. Huko barabarani askari wa usalama barabarani wanakusimamisha wanapokuta huna makosa wanatafuta hata kosa la kuendesha gari mwenyewe kwa sababu gari linabeba abiria wanne. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Buyogera!

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati zote mbili, kwa ufafanuzi wao mzuri. Naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara hizi hasa Mheshimiwa Nchimbi na Naibu wake, kwa jinsi wanavyotupa ushirikiano katika kutatua mambo mbalimbali.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane na wenzangu kuongezea katika michango mizuri ya Kamati. Kwanza, nianze na Jeshi la Magereza. Tatizo la kutoa pesa kidogo za chakula kwa Wafungwa wetu ni tatizo baya sana na ambalo linakiuka haki za binadamu. Kutoa shilingi 500 kwa kila mfungwa badala ya kutoa shilingi elfu 3,500, hili Serikali lazima mliangalie kwa kina ni aibu. Mfungwa hajulikani atakuwa nani, kesho naweza nikawa hata mimi, kunipa mlo wa shilingi 500 kwa kutwa bado ni tatizo. Kwa hiyo, hili Serikali mliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Magereza, wiki iliyopita niliuliza swali la nyongeza hapa kwamba, ukiangalia Tanzania juzi tumesherehekea miaka 52 ya Uhuru, haiwezekani katika kushangilia uhuru wa kujitawala, bado kuna Magereza katika Wilaya zetu ambazo zimejengwa na Wakoloni, ikiwemo Magereza ya Wilaya ya Kasulu. Mheshimiwa Naibu Waziri, tulienda wote pale, Gereza lile limekuwa katikati ya Mji na bado ni Gereza la Mkoloni, Gereza ambalo halina miundombinu ya kisasa. Kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie ni namna gani hata kutafuta wahisani mbalimbali kuweza kuvunja hizi Magereza zote za Mkoloni, kwa sababu kuendelea kutumia Magereza ya Mkoloni wakati tunashangilia miaka 52 ya Uhuru haina maana yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa Jeshi la Polisi. Kamati imefafanua vizuri ni namna gani Jeshi la Polisi mnawapa Bajeti kidogo. Kitu kinachopelekea *OCDs* wetu kule wanapewa fedha za mafuta kidogo sana ikiwemo Polisi wa Wilaya ya Kasulu. Mheshimiwa Naibu Waziri, tulienda wote uliona kile kijiji kilichokuwa kimeanzishwa na Wakimbizi katikati kimekaa miaka kule. Siyo kwamba, Jeshi la Polisi hawakuwa wanahitaji kwenda kule, lakini akiangalia bajeti yake ya mafuta anawezaje kwenda kutafuta tu Wakimbizi wanaoishi porini wakati kuna matukio mengi ya ujambazi yanafanyika huko. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo tunayajua kabisa utawala wake, mazingira yake ni magumu, lazima tuongezee bajeti. Tuwe na nafasi ya Serikali kuangalia kutoa bajeti ya upendeleo kwa ajili ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA]

dharura kwenye Wilaya ambazo miundombinu yake ni mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niungane na kijana wangu Mheshimiwa Moses Machali katika yale aliyoyazungumza. Sitayarudia yote lakini naomba nithibitisha kwamba, alichokizungumza nipo pamoja nae, kwa sababu Wilaya ya Kasulu ina Wabunge wawili ambao ni mimi na Mheshimiwa Machali na tunafanya kazi kama timu moja. Kwa hiyo, aliyoyazungumza naungana naye, naomba Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kidogo, kunakuwa na lawama kubwa sana kwa Jeshi la Polisi mpaka nafika mahali namhurumia sana Mheshimiwa Waziri. Mimi ni mmojawapo ambaye ninamsumbua sana Mheshimiwa Waziri na ananiheshimu sana, lakini anashindwa kumaliza matatizo ya Wilaya ya Kasulu kutokana na kukosa Mkuu wa Wilaya mwenye uwezo wa kumsaidia kazi. Haiwezekani Wabunge tunamtaja Mkuu wa Wilaya kila siku. Tunarudia Waheshimiwa Mawaziri, mtakapokaa kwenye kikao chenu msaidieni Mheshimiwa Nchimbi. Haiwezekani kila siku tunalalamika Jeshi la Polisi Kasulu, Jeshi la Polisi Kasulu, lakini anayesababisha Jeshi la Polisi Kasulu lisifanye kazi ipasavyo ni Mkuu wa Wilaya Danhi Makanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini hapo nitakuwa nimeeleweka. Ninaomba niongezee kidogo kwenye Usalama wa Taifa. Usalama wa Taifa ni watu ambao wanaheshimika sana. Kwanza, zamani ilikuwa ni ngumu sana kumfahamu Usalama wa Taifa ni nani, kulingana na maadili jinsi walivyofundishwa. Leo hii kulingana na mfumo mbovu ambao hamuusimamii sawasawa, imefikia hatua kwa kuwa Usalama wa Taifa wa Wilaya ndiye Katibu wa Mkuu wa Wilaya, kwa hiyo, anapokea maelekezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya kupotosha na kukandamiza Wanasiasa hususani sisi Wapinzani. Kitu ambacho kinawaondolea heshima watu wa Ulinzi na Usalama. Mtu wa Ulinzi na Usalama wa Wilaya ni mtu muhimu sana, ni kimbilio la Mwananchi wa aina yoyote, lakini leo hii tumebaki tunawaogopa. Leo hii wengine

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA]

wanapoteza maadili maana mnaweza mkakutana nao hata baa akakwambia hivi unanitambua mimi? Mimi ndiyo Usalama wa Taifa; ebo ni maadili kweli hayo umefundishwa? Kwa hiyo, naomba hili nalo mliangalie kuwajengea heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie na Kamati ya Mambo ya nje. Ninalo moja tu kwa Mheshimiwa Membe. Mheshimiwa Membe, Jimbo langu limepakana na Burundi. Nikihutubia katika Kijiji cha Kitanga Warundi wanakuja kunisikiliza mimi. Ninaomba muiangalie mipaka ile, mnatupambanisha na watu wa Uhamiaji, Watanzania wanakamatwa, wananyanyaswa, Warundi wanaingia kienyeji, kwa sababu mpaka ule hauna kizuizi chochote. Serikali lazima mliangalie vizuri hili ili kuepusha ni namna gani Warundi wanavyoingia Kasulu. Mtu unapotoa ajira, Warundi na Watanzania kwa namna moja au nyingine, huwezi kuwatofautisha kwa sura.

Ukimwangualia Mrundi, ukimwangualia Muha wa Kasulu, tunafanana. Sasa mtu kama mimi wa kawaida ninaenda kutoa ajira shambani, siwezi kumjua huyu ni Mrundi, huyu ni Mtanzania, mimi nataka mtu wa kunifanyia kazi. Matokeo yake, unakuja kunitafuta Buyogera kwamba nimeweka Wakulima Warundi, mimi nawatambuaje? Sijasomea kutambua Mrundi ni nani wakati Mpaka ule Serikali imeuacha kienyeji. Mpaka wa Kasulu na Burundi pale ni Mto Malagarasi. Kule ndiyo kwenye chanzo cha Mto Malagarasi, Watanzania wanafua Mto Malagarasi, Warundi wanafua Mto Malagarasi. Kwa hiyo, hili nalo mliangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaomba nijali sana muda, sina sababu ya kuweka mbwembwe za kisiasa hapa, ni wakati wa kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Namwita Mheshimiwa Mwanjelwa, ajiandae Mheshimiwa Leticia Nyerere na Mheshimiwa Juma Nkamia!

MHE. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia siku hii ya leo. Ninaomba niungane na wenzangu ambao wamewapongeza Wenyeviti wa Kamati mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake nzuri sana ambayo aliitoa jana Qunu pale South Africa. Hotuba ambayo ilikuwa ni *exemplary* kabisa kwenye Mazishi ya Tata Nelson Mandela Madiba. Dunia nzima imetambua Tanzania ni nani katika Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika hususan Afrika ya Kusini. Niliona hata Mzee Kaunda pale akiimba tu wimbo na kuzungumzia habari ya Tanzania na Ukombozi wa Kusini mwa Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nizungumzie suala zima la *shuttle diplomacy*. Mimi ninatoka Mkoa wa Mbeya, nchi ya Malawi inapakana na Mbeya na sisi Wabunge wa Mbeya siyo wote Wajumbe wa Kamati ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. Katika suala la *shuttle diplomacy* tumesikia kwamba, akina Mzee wetu Chissano na wengine, wamekuwa wakizungumzia Mpaka wa Malawi. Jambo ni la Kitaifa. Kwa hiyo, ningepomba tuelezwe limefikia wapi na tupewe *status*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la *Conference Diplomacy*. Ninaipongeza sana Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, wanafanya vizuri na suala la *Conference Diplomacy* kama tunavyoelewa ni jambo zuri ambalo linaitangaza nchi na vivutio vyake na uchumi wa nchi pia unaongezeka. Sijasikia katika *Conference Diplomacy* hii mafanikio yake ni yapi maana *all of late* tumekuwa tukipata Viongozi mbalimbali wa Kimataifa kutoka nchi za nje, suala ambalo ni zuri na ndiyo *Conference Diplomacy* yenyewe, lakini hatujaelezwa mafanikio yake *out of that Conference Diplomacy*. Ningepomba Mheshimiwa Waziri Membe, atueleze mafanikio ya Tanzania *out of the Conference Diplomacy*. Hii ni nzuri kwa sababu pia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARY M. MWANJELWA]

inazungumzia diplomasia ya Kibunge kwa sababu hii ndiyo inayolainisha mambo na kuleta ushawishi katika masuala mbalimbali yaweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la Sera ya *Economy Diplomacy*. Hii ilianza mwaka 2004 kama nakumbuka vizuri. Nataka kujua Serikali yetu imeshapitia upya Sera hii na Mkakati wake, ambayo mimi ninajua ni kila baada ya miaka mitano. Sasa nataka Waziri Membe atueleze kama Serikali imeshapitia upya Sera hii ya *Economy Diplomacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sasa hivi Dunia inabadilika, uchumi unabadilika, siasa inabadilika, sielewi Serikali yetu ina mkakati gani wa kuita Mabalozzi kila mwaka kwa ajili ya *retreat* kufanya *review*. Kwenye hii Ripoti ya Kamati ukurasa wa 11 imesema, kutofanyika kwa Mikutano ya Mabalozzi licha ya umuhimu mkubwa wa mikutano ya mwaka ya Mabalozzi kwa ajili ya kutathmini na kuboresha mambo ya msingi, ni miaka saba sasa Wizara haijaratibu mikutano hiyo. Sababu hapa iliyotolewa hairidhishi inasema, athari hiyo ni kukosekana kwa tathmini muhimu, jambo linaloweza kukwaza ufanisi wa Balozi zetu na Wizara kwa ujumla. Hii siyo sababu.

Kwa maana hiyo mimi ninasema, Wizara ijitahidi sana kuita Mabalozzi wetu nchi za nje kwa ajili ya kufanya *retreat* na *review* kwa ajili ya kupeana miongozo mipya na mikakati, kwa sababu Balozi zetu nyingi nchi za nje zinatofautiana. Kwa mfano; unaweza ukakuta Balozi ama *staff* ambao wako kwenye *First World Countries* wanapata *income* sawa na wale ambao wako kwenye *Second World* au wako kwenye *LDCs*. Sasa hii si sawa au kwa mfano masuala ya kuwa na *effective communication*, kwa sababu *effective communication* ni yule *sender* na *recipient* kuweza kupata *feedback*. Sasa vitu kama hivyo Balozi zetu zitakapokuwa zinakaa chini ni rahisi kutafsiri, kutafakari na kuangalia ni jinsi gani ya kuweza kufanikisha.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARY M. MWANJELWA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, kwa kupewa tuzo na Sekta binafsi kwa kuwa hii ni njia mojawapo ya *economic diplomacy*, kwa sababu *no private sector no economy diplomacy*. Tunataka tujue *commercial attachés* zetu kule nchi za nje zinafanyaje kazi? *Are they so much proactive* au ni namna gani; *do they deliver?* Kama ndiyo hivyo basi wapewe *marbles* ili waweze ku-*achieve* hizo *goals* kwa sababu tunasikia tu *commercial attaché, commercial attaché*, hatujaona matunda kisawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Wanajeshi wetu kule DRC. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alikuja kuomba ridhaa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba, Wanajeshi wetu waende kule DRC na Bunge lako likaridhia. Basi ni vizuri tukapewa taarifa kamili kuliko kusubiri mpaka leo hii. Naomba niwapongeze wale Wanajeshi ambao wamekufa kwa ajili ya nchi yao kizalendo, lakini zile familia zao mpaka leo zinapata tabu. Mheshimiwa Waziri angeweza kutuambia wamekuwa na mikakati gani ya kuweza kuangalia zile familia ambazo waume zao walikufa kizalendo huko DRC?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabla sijakaa, Ubalozi wetu wa Israel bado ninajiuliza na huwa ninapata sana kigugumizi sijui kinatoka wapi na kwa nini tusiwe na *full-fledged Embassy* pale Tel Avive. Tatizo liko wapi? Sisi wengine kwa imani zetu lile ni Taifa Teule na ndiyo tunakokwenda kuhiji. Licha ya kwamba, Israel pia kuna mambo mengi sana ambayo sisi kama Watanzania tungeweza kujifunza kwa sababu nalo ni Taifa kubwa.

Baada ya kuzungumza haya, sitaki kugongewa kengele ya pili, naomba kuunga mkono hoja kwa Wizara zote na kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Leticia Nyerere, ajiandae Mheshimiwa Nkamia!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. LETICIA M. NYERERE: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote, naomba kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili akiwemo Mwenyekiti wa Kamati yangu ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Edward Lowassa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Mama Anna Abdallah.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la ugaidi (*Terrorism*). Suala hili limetikisa ulimwengu. Suala hili ni nyeti kiasi kwamba, nchi zote Duniani kote tunatakiwa tupigane kushiriki katika kukomesha ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukafikiri ugaidi unapotokea Marekani unawa-*affect* Wamarekani, tunaweza tukafikiri ugaidi unapotokea Kenya unawa-*affect* Wakenya, ni vita vya Dunia nzima, tunahitaji kupigana vita dhidi ya ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uweze kupigana vita kwa niaba ya nchi yako, unahitaji uzalendo. Ninasikitika kusema kwamba, Watanzania walio wengi sasa hivi hawana uzalendo. Uzalendo maana yake ni nini? Uzalendo maana yake ni kuheshimu Bendera ya Taifa lako. Uzalendo maana yake ni kupeleka mbele Taifa lako, yaani Taifa lako kwanza. Uzalendo maana yake ni kuheshimu Viongozi wako. Uzalendo maana yake ni kuheshimu Waasisi wa Taifa lako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo hili la watu kushindwa kuheshimu Viongozi wao, watu kutumia Waasisi wetu au majina ya Waasisi wetu kwa dhihaka; hii haikubaliki. Naomba ku-*declare interest*, mimi ni mkwe wa Baba wa Taifa Julius Kambarage Nyerere. Sioni kama ni busara au heshima kutumia jina la Baba wa Taifa kwa dhihaka na dhihaka zenyewe zinatokana na kutafuta umaarufu wa kisiasa. Ninaomba jambo hili likome mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ntoa mfano wa Marekani; George Washington ndiyo Baba wa Taifa wa Marekani.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LETICIA M. NYERERE]

Bahati nzuri nimeishi America, sijawahi hata siku moja kusikia jina la George Washington linatumika kwa dhihaka. George Washington ni Baba wa Taifa wa America anaheshimiwa. Hivyo, hata Watanzania kama hawana uelewa waelimishwe, kuna majina ambayo huwezi kuyatumia kwa dhihaka. Siyo Baba wa Taifa tu, hata Waasisi wengine, kuna Wazee wetu akina Mzee Mwinyi, kuna Mstaafu Rais Mkapa, huna ruhusa wala haki ya kutumia majina haya kwa dhihaka. Huo ni utaratibu tu wa kawaida, huhitaji kwenda shule kuelimishwa kuhusu hili na wala huhitaji kusoma *political science* kutambua hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha sisi Watanzania kwa kukosa uzalendo na kutokuelewa mipaka yetu, tunathubutu hata kulisema Taifa letu vibaya tunapokuwa nje ya nchi yetu. Jambo hili linatia aibu. Kuna watu wanafanya hivyo pengine hawana uelewa na kuna wanaofanya hivyo pengine kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito Serikali yetu ianze sasa kutumia juhudi za ziada kutoa elimu ya uraia kwa Watanzania wote ambao wanajiandaa kwenda nje kwa shughuli zao binafsi ama kwa shughuli za Kiserikali, waelewe mipaka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaniuma sana, ninaenda nje, nakutana na Mtanzania ameweka kikundi (kijiwe) pale anazungumza *negative about my country. This is not acceptable*. Tuwafundishe Watanzania mambo mengine tuliyoyafanyia mzaha, lakini hatuwezi kuleta mzaha kwenye Utaifa, hatuwezi kuleta mzaha kwenye Uzalendo na hatuwezi kuleta mzaha wa kudhihaki Viongozi wetu na kuruhusu majina ya Waasisi wetu yatumike vibaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawahi kuchangia kwa hisia kama leo. Kwa kweli haya mambo yanaudhi na sielewi tutatumia mbinu gani kuyaondoa. Kwa kuwa Serikali na Watanzania wote wananisikia, naomba walifanyie kazi jambo hili.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LETICIA M. NYERERE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Mambo ya Nje. Tuna Watanzania wanaoishi nje ya nchi, wameenda kule kwa sababu za kiuchumi, hawajaenda kule kwa sababu hawaipendi Tanzania. Mimi mwenyewe ni mfano, *I am a product of Diaspora*, lakini bado ni Mzalendo tena kuliko hata wale ambao waliishi maisha yao Tanzania. Tuelewe kuna watu wa aina yangu ambao wako nje ya nchi, wameenda kwa ajili ya sababu za kiuchumi, wapewe nafasi, wapewe uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe na Naibu wake, Mahadhi Maalim na vilevile nawapongeza Mawaziri wa Shirikisho la Afrika Mashariki; Mheshimiwa Samuel Sitta pamoja na Mheshimiwa Abdalla Saadalla, kwa juhudi zao za kuwasaidia Wananchi walioko nje ya nchi hii, kwa juhudi zao za kujaribu kupigania wanaoishi nje ili wapate uraia wa nchi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie jambo moja dogo sana kuhusu nidhamu. Watanzania tumekuwa mafundi sana wa kuiga mambo ya hovy hovy tu kutoka nje ya nchi, lakini tunashindwa kuiga mambo yenye faida, nidhamu. Ukienda Uingereza, mtoto au kijana akikuona mtu mzima umesimama kwenye treni, atasimama atakupisha kiti. Ukienda Marekani ukiwa Metro, kijana au mtu wa chini ya umri wako, akikuona umesimama anakupisha kiti. Sasa ingia kwenye madaladala yetu haya, unakuta wazee wanatangatanga wameshikilia vyuma wanaanguka hovy, wale watoto wadogo ndiyo wamekaa kwenye viti. Tena *they don't care, ana-chart. This is serious*. Tumeshindwa sisi kuwafundisha watoto wetu nidhamu tu ya kawaida kama hiyo? Wangapi wanaopisha watu wazima kwenye viti nchini Tanzania? Hakuna! Nimeingia kwenye mabasi, sioni. Mzee mtu mzima anasimama mpaka mwisho wa safari. Mtu kama mimi ambaye umri wangu ni mkubwa kuliko watu wengi tu ambao wako ndani ya basi, nasimama kumpisha yule mzee ni kwa sababu nimelelewa vizuri, nina maadili mema. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. LETICIA M. NYERERE]

Mheshimiwa Mwenyekiti na Watanzania wote kwa ujumla, wazazi, vijana ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Ahsante Mheshimiwa.

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Juma Nkamia!

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Taarifa hizi mbili za Kamati.

Kwanza, nawapongeza Wenyeviti wote wawili; Mama Abdallah na Mheshimiwa Lowassa na pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili na Manaibu wao; Mheshimiwa Membe na Baba Mkwe wangu Mzee Sitta, kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye Wizara hizo. Nitazungumzia mambo makubwa mawili tu, kwanza, nitajikita zaidi kwenye Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona watu wanachukua mamlaka mikononi mwao kwa sababu tu ama ni Wakuu wa Wilaya au ni Wakuu wa Mkoa, kufanya maamuzi ambayo wakati mwingine yanasikitisha sana. Nasema hili kwa sababu, nikupe mfano mmoja mdogo sana; kule Ndoamganga - Singida na kule Handa - Chemba, ni maeneo mawili ambayo tunapakana na wale watu. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Singida ambayo ilikuwa chini ya Mkuu wa Wilaya ya Singida, yule Mama Queen, alikwenda akachoma nyumba za Wananchi kule. Alikwenda kule Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye ndiyo Jimbo lake akawaambia msifanye hivyo, lakini bado

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JUMA S. NKAMIA]

akasema sisi tunatekeleza kazi ya Serikali. Kwa kweli ni dharau mbaya sana ile. Kama Mheshimiwa Nyalandu amekwenda kule, huyu ni Waziri anadharauliwa. Wananchi wanachomewa nyumba pale, Mkuu wa Wilaya kaamua, tena ana jina zuri kama la Malkia, anaitwa Queen Mlozi! Bado kwa kweli lazima hatua za haraka zichukuliwe dhidi ya watu kama hawa. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kijiji amekuja hapa Dodoma amekaa kwangu kwa siku 20, anaogopa ameambiwa Polisi wa Singida wanaenda kumchukua. Namshukuru Mheshimiwa Nyalandu, aliponiambia kwamba huyo Mwenyekiti aende tu, kama atakamatwa akamatwe. Jambo hilo lilitokea hata kule kwa Waziri Mkuu, Kamati ya Ulinzi na Usalama imeenda ikachoma Kijiji. Sasa kama kule kwa Bwana Mkubwa panachomwa, hivi huku kwetu sisi wadogo itakuwaje? Lazima tubadilike. Tatizo hili hili linatokea pia. Naomba Mheshimiwa Ole-Nangoro anisamehe sana, ni kaka yangu, lakini mimi ni Mbunge kama yeye. Tukiendeleza tabia hii ya kuwabagua kwamba hawa Warangi, hawa Wamasai, hawa Wagogo, itatufikisha mahali pabaya sana. Usalama wetu utapotea. Tusiwaone watu wa maana wakati tunaomba kura, lakini tukishapata kura tunataka kuhatarisha usalama wa Taifa hili kwa sababu ya *interest* ndogo ndogo. Inatokea migogoro mikubwa sana kule Kiteto, Chemba na Kongwa, lakini wanaosababisha migogoro hii na matatizo haya siyo Wananchi, ni baadhi ya sisi Viongozi. Wapo baadhi ya Viongozi ni wafanyabiashara ya migogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ifike wakati watu tuheshimiane, tufanye kazi hizi kwa manufaa ya watu. Tukianza kuhatarisha usalama wa watu wetu na Taifa letu kwa sababu ya *interest* tu za kutaka kupata jambo fulani, hatutafika mahala pazuri. Kwa hiyo, naomba tatizo hili la migogoro kule Kiteto, Chemba na Kongwa, Serikali mtusaidie. Kamati hii ya Ulinzi na Usalama, ningeomba siku moja hebu fanyeni utaratibu angalau mkatembelee maeneo haya. Hali siyo shwari hata kidogo. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JUMA S. NKAMIA]

La mwisho kwenye Kamati hii ya Ulinzi na Usalama ni suala la migogoro ya baadhi ya Magereza na Wanavijiji. Magereza ya Kigang'a kule Kondoa imenyang'anya ardhi ya Wanavijiji wa Kata ya Kingale. Sasa Wananchi wale wamekasirika, Magereza wamekasirika. Magereza wana bunduki, Wananchi wana mapanga na mishale. Ikiendelea hiyo hali, ardhi yao Wananchi wanayolima miaka yote wakanyang'anywa kwa sababu Magereza wanataka kue-*extend* eneo la kullishia ng'ombe, kutakuwa na mgogoro mkubwa hapo. Ningeomba mamlaka zinazohusika kwamba, jambo hili tutumie zaidi busara kuliko nguvu. Tutumie zaidi *dialogue*, itatusaidia zaidi kuondoa migogoro hii. Nimalizie kwa kusema kwamba, naomba wale wanaofanya biashara ya migogoro waache, tunawaumiza watu wengi kwa sababu ya *interest* za watu wachache. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie pia kwa kukupongeza wewe binafsi kwa jinsi ulivyosimamia leo na nimpongeze Mheshimiwa Kawawa, kwa jinsi alivyowasilisha Taarifa. Niwapongeze Wenyeviti wote na Mawaziri wote na Manaibu wao na mimi ni-*declare interest* kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, lakini kwa kweli tumepata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa Mawaziri hawa wawili; Mzee Sitta ni Baba Mkwe wangu mimi nina-*declare interest*, lakini pia na rafiki yangu Bernard Membe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Kakoso!

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nipate kutumia fursa pekee ya kuwapongeza Wenyeviti wote waliotoa mada zao hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza kimsingi limeachwa halipewi stahili zake. Gereza la Kalilankulukulu, mazingira wanayoishi Wanajeshi wa Jeshi la Magereza ni magumu mno.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOSHI S. KAKOSO]

Ninaomba sana Serikali ielekeze nguvu kuwasaidia Gereza lile ili liweze kupata stahili; hakuna maji, hakuna mifumo ya umeme na mbaya zaidi, hata chakula wanachokula wafungwa hakitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri husika, mazingira niliyoyakuta kwenye Gereza lile yalikuwa yanatisha, hata nguo za kuvaa wafungwa walikuwa hawana. Kwa jitihada za Waziri, ameweza kupeleka nguo baada ya kupeleka lalamiko; nampongeza sana. Ninaomba sana kwenye suala la Jeshi la Magereza, tuangalie umuhimu wa kuweka bajeti ya kutosha ili kuweza kuwasaidia Wananchi wanaofanya katika Magereza mbalimbali hapa nchini. Ni vyema tukiwasaidia, watakuwa na moyo wa kufanya kazi ambayo itawasaidia kuwapa moyo zaidi waweze kushughulika na ujenzi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linafanya kazi katika mazingira magumu sana. Nina Kituo cha Polisi Kalema, Kituo cha Polisi Mwese, Kituo cha Polisi Mishamo; wana mazingira magumu sana hata pale pale Mjini, bado Askari Polisi hawana hata nyumba za kulala. Ninaomba muwasaidie Askari Polisi mazingira mazuri sambamba na kuboresha mishahara yao waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na Operesheni zilizofanywa. Namwomba Mwenyekiti wa Kamati atembelee Mpanda, aone mazingira ambayo Wananchi wamefanyiwa kinyume na taratibu za Kiserikali hata utu wa binadamu. Kuna Kijiji cha Kabage kimechomwa kwa kisingizio kwamba, Wananchi wanaishi katika maeneo ambayo ni nje na makazi, wakati uhalali wao bado Serikali ilijenga na kuwapa mazingira na kuwapa hati halali ya kuishi kama kijiji. Kuna Kitongoji cha Mnyamazi ambacho kimechomwa, Serikali imeamua kutumia nguvu kuwatoa Wananchi ili waweze kuleta wawekezaji. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MOSHI S. KAKOSO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la hatari ambalo wanafanyiwa Wananchi katika nchi yao kama wakimbizi. Naiomba Serikali iliangalie hili na waweze kulifuatilia kwa kina ili wabaini ukweli uko wapi. Tukifanya hivi tutakuwa tumewasaidia Wananchi waweze kuishi katika nchi yao kwa amani na waipende Serikali yao. Vinginevyo, tutakuwa tunawaandalia mazingira ya kuichukia Serikali pasipo sababu muhimu, kwa sababu zinazosababishwa na Watendaji wa Serikali. Naomba hilo litiliwe mkazo ili liweze kuwasaidia Wananchi wa maeneo ambayo wanaonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Dkt. Nkya, dakika tano.

MHE. DKT. LUCY SAWERE NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote mbili na Mawaziri ambao wanahusika na hizi Wizara mbili ambazo tunazizungumzia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na mengi, ninachotaka kuzungumzia ni kuhusu Wananchi kuchukua sheria mkononi, kupiga Mapolisi na kuwahukumu Watanzania wengine mpaka kufikia kuwaua. Nilitarajia kwenye hii Ripoti ningeona hili limezungumzwa na kugusia chanzo ni nini. Mimi naiomba Serikali ione kwamba sasa hivi tupo kwenye *crisis* ya kutokuwa na uangalifu katika ku-*enforce* sheria. Wananchi hawataki kufuata sheria, wanachukua sheria mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa jana tu; kuna Diwani ameuliwa Mwanza, amepigwa na Wananchi. Sawa, kama alikosea wangemkamata wampele Polisi. Naomba niseme kwamba, wakati mwingine Wananchi wanachukua sheria mkononi kwa sababu uadilifu katika Vyombo vyetu vya Sheria na Ulinzi haupo. Mwananchi anakwambia mimi namuua mwizi kwa sababu nikimkamata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. LUCY SAWERE NKYA]

na kumpeleka Polisi, kesho yuko barabarani. Kulikoni Polisi wanakuwa na tabia ya namna hiyo? Hebu naomba Wizara zinazohusika sasa wachunguze waone kwa nini Polisi wanashindwa kufanya kazi ndani ya maadili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba pia wanaohusika kwenye mfumo wa sheria waangalie ni kwa nini wale ambao wanakuwa na haki zao wananyimwa wanapewa wenye pesa? Hilo ni tatizo kubwa tusilifumbie macho, tuliangalie tutafute suluhisho. Bila hivyo, nchi haitakuwa na amani, watu watakuwa wanachukua sheria mkononi na usalama wetu sisi wote utakuwa wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie hilo kwa sababu ni jambo linalohitaji kuchukuliwa hatua ya haraka; kulikoni Wananchi hawataki kutii sheria, hawataki kuwapeleka Wananchi wanaokosa wanapotakiwa; kilichokwenda vibaya ni kipi? Jeshi la Polisi lina matatizo gani? Mfumo wa sheria una matatizo gani? Wanauliza pia hata ukienda kwenye Magereza, wakipelekwa wanatokaje mle unawakuta barabarani, hatujui. Hilo liangaliwe kwa jicho la karibu na Kamati husika naomba mliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo naomba nizungumzie ni migogoro ya wakulima na wafugaji. Polisi wanashindwa kutusaidia Viongozi na Wananchi kwa sababu hawana usafiri. Nitoe mfano wa Morogoro Vijijini; kuna Polisi wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu sana. Polisi anakwenda na pikipiki au baiskeli kumkamata mhalifu halafu Polisi huyo aendeshe pikipiki na mhalifu wake amekaa nyuma yake. Kweli jamani hiyo inawezekana? Haiwezekani. Naomba hao Polisi wapate usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna gari limekaa kwenye mawe pale Ngerengere kwa muda wa miaka mitano. Ukienda Matombo, ukienda Kisaki, ukienda Mvuha; ni Wilaya nzima ambayo sasa hivi wakulima na wafugaji kila siku kuna ugomvi wanagombana. Polisi wanafika mahali wanaona wakupigie Mbunge; wewe Mbunge utakwenda kukamata watu? Naomba Jeshi la Polisi kwa sababu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. LUCY SAWERE NKYA]

halipati pesa na vitendea kazi ndiyo sababu wanashindwa kufanya kafi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DKT. LUCY SAWERE NKYA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, awamu yetu ya asubuhi inakwisha sasa hivi. Wachangiaji wetu saba walikwisha na tukapata bahati ya kuongeza wawili kutokana na nidhamu ya muda. Jioni tutakuwa na wachangiaji sita, tutaanza na Mheshimiwa Ritta Kabati. Wizara hizi nne za Ulinzi, Mambo ya Ndani, Afrika ya Mashariki na Nje; kila Waziri atapata dakika kumi.

Nasitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.58 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyoelekezwa na Katibu wetu, majadiliano yanaendelea. Namwona Mheshimiwa Ritta Kabati atuanzishie.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niwe mchangiaji wa mwanzo kabisa jioni hii ya leo.

Kwanza kabisa, nianze kuwapongeza Wenyeviti wote wawili waliowasilisha Ripoti zao hapa Bungeni tuweze kuzijadili. Vilevile nawapongeza Mawaziri wote ambao wapo katika Wizara ambazo Kamati zimetoa Ripoti zao.

Vilevile kabla sijaanza mchango wangu, nami nimuunge mkono Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RITTA E. KABATI]

kuipongeza Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Naipongeza Hotuba ya Mheshimiwa Rais, aliyokuja kutuletea hapa Bungeni katika Bunge lililopita ambalo lilizungumzia sana migogoro iliyoejitokeza katika Wizara ya Afrika Mashariki. Kwa kweli ningetamani nichangie katika Wizara zote, Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini niwaombe Mawaziri husika ile Hotuba imejitokeza. Sana sana kinachohitajika ni utendaji. Kwa hiyo, niwakumbushe kwamba, tunaomba sasa yale aliyoyazungumza Mheshimiwa Rais, hebu wayafikirie na kuanza kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu nichangie katika Wizara ya Mambo ya Ndani na nitaanza na Jeshi la Polisi. Nafikiri Kamati imeleta Ripoti nzuri sana ambayo inajitosheleza, imeongelea mambo mengi sana ambayo sisi tunahitaji kuboresha tu. Matatizo ambayo wameyasema kwenye ile Ripoti ni ambayo hata sisi wenyewe yapo katika maeneo yetu tunayoyaongoza na katika Mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lina changamoto nyingi sana kama ambavyo Kamati imesema. Kwanza kabisa, ukianza na makazi yao ni duni na nimeona kwenye Ripoti mara nyingi wamekuwa wakianza kujenga majengo ambayo yapo Dar es Salaam na Miji mikubwa wakati kwenye Miji yetu kama Iringa, Mbeya na kwingineko, bado kuna tatizo kubwa sana la makazi ya polisi. Sasa ninaomba wakati mwingine wawe wanaanza na makazi ambayo yapo katika Mikoa yetu ya Iringa.

Vilevile Jeshi la Polisi lina matatizo makubwa sana ya vifaa, vitendea kazi, na hasa nizungumzie kuhusu magari. Kutokana na changamoto nyingi sana ambazo kwanza kabisa miundombinu ya Mkoa wetu magari ni mabovu sana ambayo yapo katika Mkoa wetu wa Iringa. Kwa hiyo, naomba hili liangaliwe na utaona kutokana na bajeti duni ambayo wamekuwa wakiileta katika Mkoa wetu, basi wamekuwa na madeni makubwa sana ambayo wanadaiwa na hao wazabuni wanaotengeneza hayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RITTA E. KABATI]

magari. Jeshi la Polisi linapokuwa halifanyiki kazi kwa raha wanafanya kazi ambazo zipo chini ya kiwango. Ninaomba hili liangaliwe. Vilevile Jeshi hili mafuta kwao ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambasamba na hilo nizungumzie kuhusu Vituo vya Polisi. Mkoa wa Iringa una changamoto kubwa sana inayohusiana na Vituo vya Polisi. Hili tatizo Wananchi wengi sana wameguswa nalo wakaamua wajitahidi kujenga vituo. Kuna vituo ambavyo vimejengwa kwa nguvu ya Wananchi, naweza nikavitaja baadhi yake; kuna Kituo kimoja kipo Isimani kimejengwa kwa nguvu za Wananchi, Kituo kipo Ifunda kimejengwa kwa nguvu ya Wananchi. Idondi, nawashukuru sana TANAPA wameweza kujenga nyumba nzuri sana ambayo ni ya Mkuu wa Kituo. Vilevile kuna Udekwa hiki kipo Kilolo nacho wanajenga TANAPA. Mimi mwenyewe kama Mbunge nimeweza kujenga kituo kikubwa kizuri sana ambacho kipo katika Jimbo la Iringa Mjini. Hiki Kituo kipo Kihensa na kipo karibu na Chuo cha Tumaini, baada ya kuona wanafunzi wale wanapata shida sana, wanapata matatizo makubwa sana na karibu Kata nne pale kulikuwa hakuna kituo. Kwa hiyo, nikaona na sisi tusiwe wa kulalamika tuongeze nguvu katika Serikali yetu kutokana na ufinyu wa bajeti ambao upo nikajenga kituo kikubwa mpaka sasa karibu shilingi milioni 34 zimezitumia pale. *(Makofi)*

Nitawaomba Mawaziri husika na Mwenyekiti wa Kamati hii, siku moja wakati tunakifungua basi waje waone hata Wananchi wanaonisikiliza leo wajue kwamba, hizi posho tunazopewa tunagawana. Wasione kwamba tunapata posho nyingi pengine tunazitumia kwa mambo mengine ni pamoja na kujenga Vituo vya Polisi kama hivyo.

Ninachoomba Serikali iangalie hivi vituo vinavyojengwa kwa nguvu ya Wananchi vingi haijaisha. Sasa na wao wajitahidi basi kusaidia ku-*support* hivi vituo viishe ili viweze kufanya kazi na kuwapa moyo Wananchi ambao wamekuwa wakichangia hivi vituo waendeleo kuchangia vingine zaidi ambavyo havipo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RITTA E. KABATI]

La mwisho kabisa, katika mchango huu kwenye Polisi niseme kwamba, Wilaya ya Kilolo ni ya siku nyingi sana, mpaka leo kwenye Makao Mkuu hakuna Ofisi ya Wilaya ya Polisi, hali inayowasababishia Wananchi wa Kilolo kupata matatizo makubwa sana kutoka kwenye maeneo mbalimbali kufuata huduma ya Polisi kwenye Wilaya. Kwa hiyo, naomba hili liangaliwe. Najua Mbunge wake amekuwa akiongea mara nyingi na mimi kama Mbunge wa Mkoa nimekuwa nikiwasilisha mara nyingi, sasa ifike sehemu hata kama bajeti finyu, lakini hebu toeni kipaumbele kwa Kituo cha Polisi cha Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye Jeshi la Magereza. Nafikiri Majeshi yote tatizo lao ni ufinyu wa bajeti pamoja na Jeshi la Magereza. Jeshi hili pia lina tatizo la makazi, lakini tunashukuru kuna jengo moja lilijengwa pale japokuwa halijasaidia kwa kiasi kikubwa, lakini tunaomba waendeleo kuboreshewa makazi yao ili wafanye kazi vizuri. Mimi pia nilipata bahati ya kufanya ziara katika Gereza Kuu la Iringa, kwa sababu nilijua kwamba, hata wafungwa na mahabusu wana haki ya kusikilizwa na mimi kama Mbunge nilikwenda kufanya ziara pale ili nijue kuna kero gani ambazo ninaweza nikaziwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza sikupenda kulia pale mbele ya Magereza, lakini nilikuja kulia nyumbani na kupiga magoti na kusali sana kwa ajili ya watu wale wa Magereza, watu waliofungwa, watu ambao wapo mahabusu. Utakuta changamoto zao nyingi sana nyingine ni kama vile kuna uonevu mkubwa. Kwanza, kabla sijasema matatizo yao nimpongeze sana Mkuu wa Gereza lile, nililikuta Gereza safi sana japokuwa msongamano ni mkubwa sana kama walivyosema Kamati kwamba Magereza mengi yana msongamano hata hili la Iringa lina msongamano mkubwa sana.

Changamoto nyingi ni kwamba, upelelezi wa kesi unachukua muda mrefu. Ningeomba hili lifanyike ili watu watendewe haki, kwa sababu katika lile gereza nilipata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. RITTA E. KABATI]

bahati ya kusikiliza kero za wafungwa 20 na kero za mahabusu 20.

Tatizo lingine ni kwamba, Jaji katika Mkoa wetu ni mmoja na bajeti yake ni finyu. Kwa hiyo, utakuta kesi nyingi zinachukua muda mrefu sana. Naomba bajeti hizi za Wizara mbalimbali ziongezwe ili kuondoa msongamano.

Vilevile rufaa nyingi hazisikilizwi kwa wakati. Nafikiri tatizo ndiyo hilo ufinyu wa bajeti, lakini pia liangaliwe. Pia kuna upungufu mkubwa sana wa makarani na kusababisha nakala za hukumu kuchukua muda mrefu sana. Hii inaongeza sana msongamano wa wafungwa. Pia wafungwa walizungumzia sana tatizo la lugha. Lugha inayozungumzwa Mahakamani hawaitambui, wanajishtukia tu wamefungwa bila kupata utetezi. Kwa hiyo, hili jambo la lugha nafikiri lilizungumziwa sana katika ile Wizara nyingine. Naomba liangaliwe ili watendewe haki waweze kujitetea. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Ndiyo tatizo la dakika kumi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Ritta Kabati, kwa mchango wako na tunakupongeza sana kwa juhudi ulizofanya za kuweza kujenga Kituo cha Polisi Iringa Mjini si haba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rweikiza, tafadhali na atafuatiwa na Mheshimiwa Vincent Nyerere.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Nami niwapongeze Wenyeviti wa Kamati hizi mbili na Wajumbe wa Kamati zote hizo, kwa Taarifa nzuri walizotusomea leo asubuhi. Nitazungumzia zaidi upande wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JASSON S. RWEIKIZA]

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwepo na Operesheni mbalimbali mojawapo inaitwa ya Kuwaondoa Wahamiaji Haramu. Pale Bukoba walikuwepo wahamiaji wengi sana na wengi wameondolewa. Wahamiaji hawa walikuwa wanatokea nchi za Rwanda, Burundi na Uganda. Cha kushangaza ni kwamba, kwanza, Sheria zipo, mtu hawezi kuja kwenye nchi hii bila utaratibu, hana vibali vya kuishi lakini anaishi, anakaa, anajenga, anatafuta kazi kama ni kulima kama ni kuajiriwa, anapata kazi bila vibali vyovyote vile. Hilo ni tatizo kubwa na hiyo Operesheni ilianza baada ya Rais kutoa agizo. Sasa tunasubiri mpaka Rais wa nchi aseme ndiyo tufanye Operesheni kama hii. Mimi nasema kweli hii kidogo imetoka nje ya viwango, tusemba hadi Rais ahutubie aagize, ndiyo tufanye kazi ambayo ipo kwenye sheria, tuifanye mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nasema zoezi hili lilikuwa zuri, la kuondoa wahamiaji haramu, kama nilivyosema Sheria zipo zifuatwe. Hata sisi hapa hauwezi kwenda nchi yoyote ile ukakaa, ukapata ajira, ukajenga nyumba ukaishi kule bila utaratibu kufuatwa.

Sasa walivyoondolewa hawa wahamiaji haramu wa Bukoba ni jambo la kusikitisha, wengi sana wapo pale Uganda mpakani, wamepewa hifadhi na Serikali ya Uganda. Hatuwezi kuilaumu Serikali ya Uganda kwa sababu wameamua kuwapokea, wana hiari ya kuwaweka popote pale wanapotaka kuwawekea ndani ya Uganda, lakini wapo mpakani, kilomita kama nne baada ya kuvuka mpaka, ni sehemu ya pori, hakuna mashamba pale, wamewekwa kambi, wamejenga mahema na nyumba za plastiki; wapo wengi sana. Nimeangalia ile Kambi inaanzia kama hapa mpaka Ihumwa. Kambi, huku nyumba nyingi na upande huu nyumba nyingi na pale hakuna mashamba wanakwenda kuhemea nje ya Kambi, wanakwenda Kaskazini kule ndani ya Uganda, Mashariki na Magharibi ndani ya Uganda na Kusini Tanzania yenyewe walikotoka kuhemea chakula, wana majembe tu. Sasa hii nasema siyo salama hata kidogo kwa sisi Watanzania. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JASSON S. RWEIKIZA]

Hawa watu wameondoka siyo kwa furaha kwa kinyogo wameondolewa. Wameishi huku kwa miaka mingi, wameondoka wameacha mifugo yao, ng'ombe na mifugo mingine. Familia zao nyingine zimebaki huku, nyumba zimebaki huku, wameondoka kwa kinyogo. Wanaingia huru pale mpakani hakuna kizuizi, baada ya mpaka huku pembeni hakuna kizuizi, wanatembea kwa miguu wanaingia Tanzania tena kama kawaida. Sasa hatuwezi kuwa salama katika hali kama hii na ni wengi sana. Ni wengi sana lazima *study* zifanyike kuweka ulinzi imara pale wa kutosha kulinda hali ile isije ikaleta hatari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama nilivyosema hatuwezi kulaumu Uganda, lakini ikiwezekana zifanyike jitihada za kidiplomasia kuongea na Uganda kwamba, sawa hawa watu mmewahifadhi basi wawapeleke mbali kule juu kilomita 500 ndani ya Uganda huko siyo pale mpakani. Hili ni tatizo kubwa ambalo ninaona kwamba, baada ya muda mfupi watarudi mmoja mmoja usiku, jioni, watarudi tena. Hali itakuwa ni ile ile tuliyowaondoa, watakuwa wamerudi tena wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nikiwa bado nipo kwenye Wizara hiyo hiyo ya Mambo ya Ndani ni kuhusu wafungwa ambao Wabunge wengi wameongea kuhusu hali mbali ya bajeti. Kweli Magereza kuna matatizo, lakini siyo magereza peke yake, juzi nilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani pale Mwanza, akawa anasema mwaka jana tulipitisha Bajeti hapa shilingi 500 kwa kila mfungwa, chakula cha mfungwa. Waliomba shilingi 1,500 iliyopitishwa ni shilingi 500, ndogo sana, theluthi moja. Hiyo iliyopitishwa haikutoka Hazina kwenda kule Magereza iliyopitishwa. Bado wakawa na hali ngumu sana, kwa hiyo, chakula, mavazi, malazi, usafi na kadhalika ni hali ngumu mno.

Sasa mimi napendekeza kwamba, kwa sababu hali hii ya ufinyu wa bajeti siyo Magereza peke yake, Idara zote, Wizara zoe na Mikoa yote bajeti ni finyu. Kinachoombwa hakipitishwi, kinachopitishwa hakitoka. Ushauri wangu ni kwamba, magereza hawa ambao wana nguvu kazi, hawa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JASSON S. RWEIKIZA]

wafungwa ni nguvu kazi ya kutosha, wanafanya kazi nyingi sana kwenye Magereza, wana mashamba, wana Miradi mbalimbali inazalisha. Sasa wapanue wigo hawa wafungwa waende wakafanye kazi nje ya Gereza, waende mashambani, mashamba ya watu binafsi, mashamba ya makampuni, mashamba ya miwa kama kule Kilombero, Mtibwa, Bukoba kule Kagera Sugar waajiriwe, walipwe Magereza waitumie fedha hiyo. Wafungwa hawa wanakuwa wengi mno bila sababu kila mwenye kosa dogo jela miezi mitatu. Kosa dogo amepigana na mtu jela miezi sita, mimi nafikiri tunakosea mahakama, sheria zipo zinasema kuna vifungo vya nje. Mtu anafungwa kifungo cha nje hawi mzungo kwenye Magereza hana bajeti ya kumlisha, lakini amefungwa kifungo cha nje. Anafanya kazi za jamii akiwa nje ya Gereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni huo kwa sasa, kwa ufupi naomba Serikali isaidie kupunguza msongamano na matatizo ya bajeti katika Idara hii ya Magereza. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Jasson Rweikiza. Kama nilivyosema, Mheshimiwa Vincent Nyerere ndiye aliyefuata na atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni bora ukweli unaouma kuliko uongo unaofurahisha. Mimi ningeweza nikaanza na wewe, mimi, Mawaziri tukaenda tukakaa Gereza hata wiki moja tu, tukirudi hapa tukaongea lugha inayoeleweka.

Niliwahi kujibiwa na Serikali hapa kwamba, wafungwa wanakula milo mitatu na vitafunwa sijui na nini, Serikali hiyo hiyo leo wanatuambia wafungwa wanakula shilingi 500! Nashindwa kuelewa Serikali ilikuwa inadanganya siku zile au inadanganya sasa hivi? Shilingi 500 sehemu nyingine haitoshi kununua chupa moja ya maji leo anapewa mtu akale kwa milo mitatu haiwezekani. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VINCENT J. NYERERE]

Tukimchukua Waziri sasa hivi ukampa shilingi 500 ukamwambia akajilipie milo mitatu sijui kama inawezekana. Kama tunashindwa kukaa na wafungwa wafungulienu tuanze upya siyo ujinga. Wengi walioko Gerezani wengine siyo wahalifu. Wengine wamebambikwa kesi, kwa nchi iliyojaa rushwa kama Tanzania, wengine wamekosa fedha za kununua haki zao.

Wamekosa fedha ya kuhonga polisi, fedha ya kuweka Wakili au Mahakama wanaishia gerezani wengi siyo wahalifu. Ndiyo maana nasema pengine tukikaa wiki moja gerezani tukirudi hapa tutaongea lugha inayooleweka. Hali kule siyo nzuri wale watu wana shida.

Mimi huwa natembea sana Magerezani, niliwahi kukutana na mfungwa amehukumiwa miezi sita au faini sijui laki moja hana kwa sababu alipanda kwenye basi ambalo ndani yake lilikutwa lina mirungi na siti aliyokuwa amekaa ipo chini yake wakasema ni ya kwake lakini haikuwa yake, alifungwa. Kwa hiyo, wengi wanaokuwa kule tuwafikirie sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi, nadhani mwezi wa kumi alikuwa Gerezani pale alikwenda kuwatembelea wale wafungwa hali zao ni mbaya sana. Hasa mahabusu niliwahi kutembelea Gereza la pale Jimboni kwangu Musoma, kuna watu zaidi ya 50 wapo pale kwa kesi ya *murder* tofauti tofauti.

Sasa mimi Mbunge, sijawahi kusikia kuna watu 50 wamekufa, wengi wamebambikiwa na wapo wanaokwambia mimi nimebambikiwa kesi na askari fulani kwa sababu fulani wapo Gerezani. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VINCENT J. NYERERE]

Kwa hiyo, tunaposema tuwasaidie wafungwa, wengi sio wahalifu hasa mahabusu. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema ni vizuri tuwe tunaongea lugha ambayo inaeleweka kuliko kuwa tunadanganyana hapa. Sijui kwa nini huwa tunadanganya kwamba tuko shwari, hali ya usalama iko sawa! Unajua hizi *salute* ambazo Askari wanatupigia iko siku zitageuka kuwa makofi. Hakuna Askari Polisi hata mmoja asiyenung'unika. Tuliwapitishia fedha hapa Sh. 225,000/=, Serikali inakuja hapa na jibu rahisi tu kwamba fedha hizi hazipo sasa hivi, tuangalie bajeti ijayo. Mbona ziara za viongozi na wapambe wao hazisubiri bajeti ijayo?

Mimi huwa siwaelewi! Kama tulikubaliana hapa kwamba *ration* ya Askari iwe ni Sh. 225,000/= na kwenye Mikutano yenu ya siasa bahati nzuri Askari huwa wapo, Waziri wa Fedha na Wana-CCM wenzenu mnatamba uchumi wetu unapaa. Kama uchumi unapaa, kwa nini mnawanyima? Au mrudi mtuambie uchumi haupai, tuna matatizo. Kwa nini huwa mnawadanganya? Kama mnataka, siku moja piteni mumwulize Mama Maria Nyerere, yeye ana historia. Hivi Askari wakikosa adabu wakapindua huwa inakuwaje? Kwa sababu yeye yaliwahi kumkuta. Siwashauri wafanye hivyo, lakini mkae mnakumbuka kwamba hizo bunduki wanazobeba siyo gitaa. Hawana uwezo wa kusema kwa sababu hawaruhusiwi hata kuwa na Chama cha Wafanyakazi, lakini wananung'unika. Hali zao ni mbaya, halafu sisi kazi yetu huwa tunawatuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi, kimbilio la kwanza kwa kila mtu hapa huwa ni Polisi. Sasa hivi ukiwaita tu, njoo toa huyu wanakuja *speed*, wala hawahoji? Lakini ikifikia muda wa fedha tulizopitisha Bunge hili wapewe, hawapewi. Huwa ndiyo *nature* yao; unajua ukiwaambia Polisi nyuma geuka...

NAIBU SPIKA: Kwa Askari wa Bunge wanapata fedha zao. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. VINCENT J. NYERERE: Tatizo, ukiwaambia nyuma geuka hawaulizi kuna nini wanageuka, mbele tembea mpaka wapi hawaulizi, wanatembea; lakini inapofikia saa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VINCENT J. NYERERE]

ya fedha hazipo, sawa afande, wanakubali; lakini iko siku sijui itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja la ajabu sana, tumegeuza Jeshi la Polisi kama chanzo cha mapato cha Serikali. Anasimama *RPC* anasema mwaka huu faini za barabarani tumekusanya Shilingi milioni 200. Ajali zinaendelea. Hivi lengo ni kumaliza ajali au kukusanya fedha? Tukubaliane kama Jeshi la Polisi ni mojawapo ya chanzo cha mapato ya Serikali tuambiwe hapa tujue. Lakini kama Mkoa mmoja unaweza kukusanya faini za barabarani Shilingi milioni 200, kwa nini Polisi wasiwalipe hiyo *ration* kwa sababu ongezeko nadhani ni kama Shilingi bilioni tisa. Jamani tusiwadhulumu, nao wana shida. Aniambie Mbunge yeyote hapa ambaye ameingia hapa bila ya msaada wa Polisi, hayupo! Wote hapa wameingia hapa kwa msaada wa Polisi. Asimame aseme hapa, kwa sababu na Polisi wa Mkoa wake wanaona kwamba mimi sikuingia kwa msaada wa Polisi. Wote tumeingia hapa kwa msaada wa Polisi, awe wa Upinzani awe wa Chama cha Mapinduzi.

Kwa hiyo, ni vizuri sana kama tunataka kuwa salama, tuangalie. Sasa hivi fedha ambazo Polisi hawa wanakatwa mshahara na wananchi wengine wanakatwa mshahara wanalipa kodi zinawalinda Viongozi Wakuu wa nchi wakati wao maisha yao yako mashakani. Tukafikirie mara mbili kama kweli tunataka kufanya mambo *serious*. Polisi wana shida, Askari Magereza ndio usiseme.

Polisi hawana uwezo wala Askari Magereza ni tofauti na Madaktari ambaye anaweza kuwa na kliniki sehemu nyingine, Askari hawezi kuwa Askari halafu akafanya kazi ya ziada sehemu nyingine. Bora hata Walimu kidogo wanaweza kuwa wanafundisha *tuition*. Lakini Askari akiingia kwenye kazi ya lindo, ni hilo hilo na wanalinda mabilioni yetu Benki pale halafu wao nyumbani kwao hakuna hata sabuni. Kuna Askari Magereza wanaomba mpaka sabuni kwa wafungwa. Kwa hiyo, tufikirie sana. Tusiwafikirie tu wakati wa uchaguzi! Sasa hivi tunakwenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa ndio tutaanza kujipendekeza kwa Polisi. Tusifanye hivyo, ni dhambi!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VINCENT J. NYERERE]

Ndio maana nimeomba ikiwezekana wagome masaa mawili tu, mwone kama kuna mtu atakaa hapa.

Kwa hiyo, ni vizuri mnaposema uchumi unakua, utafsirike kwenye mifuko ya Askari pia. Wanapata taabu sana, fedha yao ni kidogo sana na hawana muda wa ziada wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na tabia wanasisia kuwayumbisha Askari. Sisi wenyewe tuliomba kwamba wahamiaji haramu wamekuwa wengi, tunahitaji operesheni. Hivi ni nani aliyewaambia operesheni ni sawa na doria? Operesheni ina vishindo vyake. Walivyogusa tu wapiga kura wenu, wengine Wenyeviti wa Serikali za Mitaa huko wa Chama chenu ambao ni wahamiaji haramu, tukarudi tena hapa; Polisi wameua, Polisi wabaya. Kwa hiyo, tunawayumbisha, tunawanyima muda wa kufanya kazi. Kama tumeamua, tumekubaliana hapa Bungeni operesheni ifanyike, ifanyike. Akikamatwa mtu wa Chama chako, wewe kauka tu kwa sababu tumeshakubaliana hapa. Tofauti na hapo, Polisi watafanya nini? Hapa na sisi wenyewe tumekubali operesheni ifanyike, halafu tunarudi hapa tena tunawalaumu Polisi. Kwani wakati tunakubaliana hapa mlikuwa hamjui? Kwa hiyo, ni vizuri tuwe na misimamo. Tunapoamua kitu kwenye Bunge kwa pamoja, hata kama tumeshindwa kwenye kura, vitu vikafanyike kama tulivyokubali. Siyo wakishaguswa watu wenu, mnarudi hapa tena mnawapiga Polisi mkwara, hawajui sasa wafanye nini; yaani hawajui washike amri ya nani. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. VINCENT J. NYERERE: Kengele ya kwanza hiyo.

NAIBU SPIKA: Wananiambia ya pili. Nakushukuru sana Mheshimiwa Vicent. Amewatetea sana Askari wetu, jambo ambalo ni zuri. Ila jambo moja hakufanya haku-*declare interest*, siku nyingine tutamwomba atueleze kidogo mahusiano yake na... (*Kicheko*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKA]

Sasa namwita Mheshimiwa Betty Machangu na Mheshimiwa Mariam Msabaha ajiandae.

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi ni-*declare interest* kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na naomba nitilie mkazo mambo machache. La kwanza, hasa niilenge Serikali lakini kupitia Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna majengo mengi nje ya nchi ambayo ni mazuri, yako kwenye maeneo muhimu. Kwa mfano, tuna jengo Washington, New York, kuna kiwanja kiko London, lakini popote haya majengo yalipo yanashindwa kurekebishwa na fedha ya mkopo, kwa sababu kuna Sheria ambayo ni ya Mikopo, Msaada na Dhamana ya mwaka 1974 ilirekebishwa 2004. Sheria hii ndiyo imekuwa changamoto ya Balozi kukopa kwa ajili ya kurekebisha majengo waliyonayo. Wako Mabalози wetu ambao ni wabunifu sana na ingekuwa inawezekana yaani hii sheria ingesharekebishwa, kuna majengo yake mengine yanayoweza kutoa dhamana akakopa akarekebisha jengo lingine zuri.

Kwa mfano, mahali kama pale Washington kulikuwa na jengo la ghorofa nne ambapo ingekuwa ni rahisi kuomba mkopo, yule Balozi angeweza kuomba mkopo akarekebisha lile jengo akapata fedha na akarudisha fedha za watu alizokopa Benki. Lakini inashindikana kwa sababu ya hii sheria. Kwa hiyo, ninachoomba, Serikali ilete Muswada turekebishe hii sheria kwa ajili ya kuwa na Kitengo cha *Debt Financing*. Kama itachukua *TBA*, au Serikali, Wizara ya Fedha au Mambo ya Nje, sisi hatujali. Tunachojali ni kwamba haya majengo yaliyoko nje ya nchi yatunzwe, yaletе *revenue* kwa ajili ya Taifa la Tanzania. Kwa hiyo, naomba sana tuangalie namna ya kurekebisha hii sheria kwa ajili Balozi zetu kuweza kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka nilitilie mkazo ni Kitengo cha Kuratibu Masuala ya Diplomasia ya Uchumi. Mabalози wetu wote wamesoma vizuri, wana elimu yao nzuri, wengine ni Wanauchumi, wana uwezo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. BETTY E. MACHANGU]

mkubwa kabisa wa kuleta hata *investors* wakafanya mambo ya kufaidisha Taifa hili. Kunahitajika Kitengo hiki kiwekwe, aidha kwenye Wizara ya Mambo ya Nje kwa ajili ya kuratibu hii Diplomasia ya uchumi, kuelekezana na hawa Mabalazi, kifanyike nini ili isaidie Taifa la Tanzania. Kwa hiyo, ningependa nisisitize hili, tunaomba sana hiki Kitengo kiwepo kiweze kuratibu haya masuala ya Kidiplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini linguine, wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye Balozi zetu; wewe unajua ukiwa Ulaya huna ndugu pale, hakuna mjomba wala shangazi. Siku huna fedha, ni kweli huna fedha. Sasa wafanyakazi waliopo kwenye Balozi zetu, fedha zikichelewa *you can imagine* namna gani wanateseka. Kwa hiyo, sisi Kamati tulikuwa tumeshauri kwamba fedha hizi Wizara ya Fedha ipeleke moja kwa moja kule Balozini. Si kule kuna *Accounting Officer? At-account for that money*, badala ya kuzitoa zipelekwe tena Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa halafu ziende kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Serikali iliangalie hili. Najua sababu gani walifanya hivyo, lakini kama kuna uwezekano wa kurekebisha kanuni au mpango wowote uliowekwa, ikawezekana kwamba wafanyakazi hawa wa Ubalozini wapelekewe fedha *direct*, mbona tunapeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri za Wilaya? Kwa hiyo, na huko tupeleke moja kwa moja kwa ajili ya kuwanusuru wafanyakazi ambao urasimu wa kupeleka fedha unawafanya wanapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda pia nisisitize kuhusu mikutano ya Mabalazi, ni muhimu kwa kweli kwa sababu Mabalazi wakija nyumbani wakakutana hata na Kamati za Bunge au na Wabunge, yako mambo mengi yanaweza kuibuliwa tukayajua, tukayasimamia, yapo mambo pengine kama Bunge tutahitaji kurekebisha kwa kupitisha Miswada ya Sheria, naomba tafadhali hebu Serikali iliangalie hili. Kwa miaka saba Mikutano hiyo haijakuwepo, sasa tunaomba kwa bajeti ijayo fedha iwepo ili Mikutano hii ya Mabalazi iweze kufanyika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. BETTY E. MACHANGU]

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Elimu bado. Watanzania wengi hawajui fursa zilizopo katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki, hawafahamu. Hata wale waliopo kwenye mipaka kwa mfano, Kilimanjaro, Arusha wengi pia hawafahamu, licha ambao wako Kusini au katikati ya Tanzania. Hii elimu imeshindikana kutolewa kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, ninachoomba, Serikali ilianganalie hili kipindi kijacho bajeti iweze kuongezeka ili elimu itolewe. Tunasikia mambo ya walio tayari waendele. Sasa hawa walio tayari waendele Waheshimiwa, maana yake ni kwamba na sisi tuamke, tufanye yale mambo ambayo yanatakiwa tuyafanye kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania waone hizi fursa wazichangamkie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuna sheria ambazo zinatakiwa zitungwe ambazo Wizara ya Afrika Mashariki inaandaa. Kwa mfano, mambo ya utafiti, Wizara itaandaa lakini itapeleka kwenye Wizara husika. Kwa mfano, itapeleka Utumishi ambao wanatakiwa wa-*domesticate* hizi sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi sheria haziwi hivyo! Hawafanyi! Zile *Sectoral Ministries* zinatakiwa zi-*domesticate* hizi sheria ili tuweze kushiriki vizuri kwenye *East Africa*. Wenzetu wa Kenya, Uganda wanafanya haraka haraka kila sheria inapopita, lakini sisi tunachelewesha. Naomba tulifanye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni Ofisi kwa ajili ya Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Tunalalamika kwamba Wabunge hawa hawaleti taarifa, hawa-*attend* vizuri, hawasemi ya Tanzania yanayotosha. Lakini haya mambo tunatakiwa na sisi tuwaambie wakiwepo kwenye ofisi fulani. Tulishaomba kwamba Bunge liwape ofisi, hata kama ni chumba kimoja chenye kompyuta mbili, lakini wapate ofisi. Kwenye hizo ofisi hata wananchi wanaotaka kuwaona ni rahisi kuwaona na kuwauliza mambo ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, naomba tafadhali Bunge ilianganalie hili, Wabunge wa Afrika Mashariki wapewe Ofisi kwa sababu nao wanaripoti kwenye Kamati yetu, na itakuwa ni rahisi kwa Wabunge

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. BETTY E. MACHANGU]

kuweza kuwasiliana nao na kuwauliza maswali, kupata taarifa zaidi za ushirikiano wa Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo, nashukuru sana, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Betty Machangu. Namwita Mheshimiwa Maryam Msabaha na kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge atakayefunga pazia ni Mheshimiwa *Capt.* Chilligati.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii nipate kuchangia hotuba ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mimi nitajikita sana katika mambo ya JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 14 wa hotuba ya Kamati, kuna hiki kipengele walichokusudia wakasema waongeze muda wa mafunzo ya JKT. Kuna vijana wanaenda makundi mawili katika JKT; kwa mujibu wa sheria na wale ambao wanajitolea. Lakini tuangalie makambi yetu yako vipi jamani. Bajeti ya Ulinzi na Usalama haitoshi! Bajeti yake ni ndogo sana! Wale vijana tunawapeleka makambini wanataka kula, bado miundombinu ya kule makambini siyo mizuri sana. Sasa tukisema tunaongeza miezi sita, watakula nini kule makambini? Wataishi vipi kule?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifanye *research* ya kutosha, iangalie makambi yetu, miundombinu siyo mizuri. Leo wakufunzi wa makambi nyumba zao zinavuja. Msione wanajeshi wamenyamaza, kuna vitu vingi sana, lakini haviwezi kuwekwa hadharani. Kwa hiyo, tuangalie ni namna gani tunaboresha kwanza makambi yetu ya JKT, tuangalie wanajeshi wetu wakufunzi wanaishi vipi, ndio tuseme tuongeze muda wa wanafunzi hawa wanaokwenda kwa mujibu wa sheria na wanaokwenda kwa kujitolea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine vijana wetu wakishakwenda kule kambini, wanataka ajira Serikalini. Tuangalie namna ya kujenga Vyuo vya *VETA* ndani ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARYAM SALUM MSABAHA]

makambi yetu. Vyuu ambavyo viko, havina tija, vinatakiwa viboreshwe. Leo hii kila kijana ukimwambia leo utaenda JKT anajua anakuwa Mwanajeshi, anajua anapata ajira Serikalini. Tuangalie namna gani ya kuwaboresha kwanza vijana wawe na ujasiri wa nchi yao kwanza, halafu wajiajiri wenyewe tusikazanie tu kuongeza muda. Kwa kweli hili napingana nalo na mimi najua mambo ya huko makambini, hali sio nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni wananchi walioko kwenye mipaka ya makambi, wanaozungukwa na maeneo ya Jeshi. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi upo hapa, hawa wananchi wanatakiwa wapewe somo la kutosha, kwa sababu wananchi hawa wanasogea maeneo ya Jeshi na kujenga majumba ya makazi. Jeshini kuna vitu vya hatari mle, vinapokuja kulipuka wananchi hawa wanaleta matatizo kwenye Serikali. Lakini wapewe elimu ya kutosha waogope kukaa karibu na maeneo ya Jeshi. Wengine wamekuwa wanaleta migogoro baina ya Wanajeshi na raia.

Kwanza hapo nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa sababu amefanya jitihada sana za kupima mipaka ya Jeshi na wananchi. Hili amefanya! Lakini hawa wananchi pia wapewe elimu ya kutosha kuhusu mipaka ya Jeshi. Wengine wamekuwa wanabishana. Mwanajeshi sio mtu wa kubishana naye! Lakini wengi wamekuwa wakibishana, wanavamia maeneo ya Jeshi na kujenga, baadaye wanaleta mgogoro kwenye Serikali. Kwa hiyo, wananchi ambao wanazunguka mipaka ya Jeshi wapewe elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu usalama wa nchi yetu jamani. Sasa hivi nashukuru mzee wangu wa Utawala Bora amekaa pale. Kwa kweli tumeona nyaraka za Serikali zinapoteapotea ovyo. Sisi sio useme kila mtu anaipenda Tanzania, tumezungukwa na maadui wangapi? Hebu tuangalie tu usalama wa nchi yetu na Kitengo cha Usalama tukiangalie vizuri, kina matatizo gani? Tukiboreshe na ambao sio waadilifu pia tuwaondoe kwenye Kitengo hiki. Hii inapelekea hata nyaraka zetu kuangukia mikononi mwa maadui waliotzunguka. Leo ukiangalia nyaraka za Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARYAM SALUM MSABAHA]

hata akina mama wauza maandazi wanazo. Maadui wakishapata nyaraka zile watajua uapungufu wa nchi yetu. Naomba mzee wangu umekaa hapo Mheshimiwa Waziri uangalie hili kwenye mambo ya usalama. Tuangalie mambo ya utawala bora na usalama. Usalama wa nchi hii kila mmoja awe mwaminifu kwa nchi yetu, tuangalie ni namna gani ya kulinda maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, leo hii vita ikiingia hapa au migogoro ikiingia ndani ya siasa na dini leo tutapelekana wapi? Hasa akina mama ndio tutapata taabu. Leo hii Askari wa Akiba tutachukuliwa, wengine sasa hivi tutashindwa, wengine hawajui na wengine wameshazeeke hata kushika bunduki wengine hawawezi. Sasa tuangalie ni namna gani tutadhibiti vitu vya Serikali. Mtu anayevujisha siri za Serikali, pia ipitishwe Sheria achukuliwe hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la Magereza. Hili suala limeongelewa sana, lakini kule ndani ya Magereza hasa kule Rumande, wale wenye kesi ndogo ndogo kama zile za kuku, nazi, kupora simu, tuangalie namna gani tuwafunge vifungo vya nje. Kwasababu unakuta kwa wenzetu kuna Sheria, wale ambao hawana makosa makubwa wanafungwa vifungo vya nje. Tukiangalia leo kama Tanzania, jiji la Dar es Salaam tunaongoza kwa uchafu, kwanini wale tusiwachukue wakafagia hata barabara zetu, wakasafisha mitaro wakaenda mahospitalini kule wakasafisha. Sisi tutapata wapi Bajeti ya kulisha watu wote wale Magerezani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Magerezani mle kunasambazwa Ukimwi, kuna vitendo vichafu ambavyo vinafanyika! Hili nimekuwa nikipigia kelele na nitazidi kulisemea! Tuwaondoe! Kuna watoto wadogo wanachanganyika na watu wazima mle Magerezani na Rumande huko. Hebu tuangalie ni namna gani ya kupunguza hawa wafungwa na hawa ambao wako Mahabusu au Rumande tuwafunge vifungo vya nje. Mtu akikamatwa na simu, akipora pesa, tuangalie tu wale wenye makosa madogo madogo tuwafunge vifungo vya nje. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARYAM SALUM MSABAHA]

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda haraka haraka, tuangalie na lingine kuhusu lishe ya Maaskari wetu. Askari ni mtu ambaye anapambana na majambazi; wanakaa usiku kucha wanalinda. Jamani tuangalie, hawana lishe ya kutosha. Lishe yao ni ya mgogoro. Tunavyosema Askari ni walinzi wa usalama, wanatulinda, tuwape lishe ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimeongea kwa uchungu kwa sababu kulikuwa na vitu ambavyo vilikuwa vinapatikana Jeshini leo havipo. Watu walikuwa wanakula vizuri kule Jeshini lakini vile vyakula kabisa siku hizi havipo. Sasa wewe unategemea nini *Yarabilaalamina?* Lazima Askari huyu kama hashibi, leo unategemea mwizi akija, jambazi mfano ametoka Rwanda ameshiba, amebeba risasi zake akishindana na Askari wetu, hana lishe ya kutosha kwa kweli m ajambazi hawa sisi tutawafanya nini? Si lazima watawapiga Maaskari wetu na kuwapokonya silaha? Tuangalie ni namna gani Maaskari wetu watapata lishe, na kuboresha maslahi yao. Kwasababu wakiboreshewa maslahi yao watakuwa katika *standard* ya kufanya kazi na watakuwa watifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusifanye mambo ya siasa kwenye Wizara nyeti kama hizi. Kitu kama kimepindapinda lazima tukiweke sawa. Vitu kama haviieleweki lazima tuviweke sawa. Lakini leo unakuta Maaskari wanachukua rushwa kesi haziendi; leo tumeshuhudia matukio wananchi wanachukua hatua mikononi, wanawapiga watu mpaka wanawauwa, kwasababu wanasema hata ukipeleka kesi Askari hatendi haki.

Kwa hiyo, sasa hivi tuangalie ni namna gani ya kuwaboresha Maaskari mishahara, posho zao, lishe ili waepukanike na rushwa ndogo ndogo. Kwa wenzetu kama hivyo Mawaziri wetu mnatembea mnakwenda nchi za wenzenu, mnajifunza; leo nenda Marekani, mtu akiwa kama Askari anapenda kazi yake na anafurahi, yaani ile kazi anaifurahia kwasababu anapewa vitendea kazi vyote. Lakini leo unamkuta mtu ana kirungu; kirungu kitafanya nini? Ana buti mbele inaomba mvua, unategemea atafanya nini?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MARYAM SALUM MSABAHA]

Sare za Maaskari ukiona hazipo katika *standard* ya kusema huyu ni Askari. Sisi tunataka tu tupigiwe saluti, kwa kweli hili tuliangalie kwa makini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Vituo vya Polisi na nyumba za Mapolisi. Tumekaa tunapiga kelele; kwa upande wa Zanzibar na Pemba ukiangalia vituo vingi vimechakaa. Tuviboreshe vituo hivi, makazi ya Mapolisi wapate huduma jamani zinazotakiwa. Tutawalaumu Polisi wetu, hawatendi kazi, wanakula rushwa, lakini na sisi tuangalie wanaishi mazingira gani. Mimi nakaa na Mapolisi, naona matatizo wanayoyapata, unakuta mtu chumba kaweka pazia, huku baba, huku familia ya watoto wanne ama watano. Mimi nakaa nao! Nakaa *Police Line* hapa Dodoma, naona mazingira ambayo wanaishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ya kwangu ndiyo hayo, naiomba Serikali, haya niliyoyasema myafanyie kazi. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maryam Msabaha tunakushukuru sana kwa mchango wako. Pia huko mbele safari na wewe tutakuomba u-*declare interest* katika kukaa na Askari kwa utaratibu upi?

Mheshimiwa Chiligati ndio mchangiaji wa mwisho kwa Waheshimiwa Wabunge. (*Kicheko*)

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja hii. Nimesimama kwa jambo moja tu, nalo ni kuwasilisha salamu za Askari wetu walio Darfur katika Bunge letu. Mimi ni mmoja wa Wanakamati tuliokwenda Darfur kuona jinsi vijana wetu wanavyofanya kazi kule na kuwatia moyo. Walifurahi sana kutembelewa na Waheshimiwa Wabunge tukifuatana na Waziri wa Ulinzi. Kama taarifa yetu ilivyosema, tuliwakuta hali zao ni njema kimwili, kiroho, kisaikolojia; wanajua kwanini wako kule na wanafanya kazi zao vizuri. Walitutuma kwamba tulete salamu zao, kazi

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI]

tuliyowatuma wanaifanya vizuri, tuwaombe kwa wako katika mazingira ya hatari, warudi salama. *(Makofi)*

Tukiwa kule tulizungumza vilevile na Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kule Darfur yaani *Head of Mission*, tulitaka kuona jinsi Askari wetu wanavyoendelea na anavyowaona, alituthibitishia kwamba Askari wa Tanzania ni moja ya vikosi ambavyo vinaonesha nidhamu nzuri, juhudi na weledi wa kiwango cha juu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Waheshimiwa Wabunge, nataka muwe na uhakika kwamba kazi ambayo tuliwatuma vijana kule wanaifanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme jambo moja kwamba hali tuliyoikuta ya amani, maana vijana hawa tumewatuma kulinda amani, bado hali ni tete kule Darfur. Kuna vikundi vitano vya waasi vinavyopigana na Serikali; yako mazungumzo ya kuleta amani yanafanyikia Doha Qatar; mpaka tunapokwenda mwezi Septemba katika vikundi vitano ambavyo vina silaha vinapigana na Serikali, kimoja tu ndicho kilikuwa kimetia saini kukubali kuacha mapigano. Vikundi vinne bado havijakubali na bado vinapigana. Mbaya zaidi, hivi karibuni imezuka tena tatizo lingine wao kwa wao tena wanapigana, yaani waasi kwa waasi wanapigana. Wanapigana kwasababu wananyang'anyana maeneo ya madini, maeneo ya kufuga nawizi wa mifugo. Kwa hiyo, tatizo limekuwa tete na tata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliishauri Serikali kwamba katika hali tuliyoikuta kule Darfur Serikali ijiandae kupeleka wanajeshi kwa miaka miwili, mitatu ijayo. Tatizo lile halitakwisha ndani ya mwaka mmoja au miaka miwili. Hayo ndiyo tuliyoyakuta kule. Lakini vijana wetu wanaendelea vizuri. Tuliwapa pole kwa lile tukio la Julai 13, ambapo wakati walikuwa wanasindikiza wale watoa huduma za jamii zile *convoy* zinapeleka dawa, chakula na mahitaji mbalimbali, wanasindikizwa na wale vijana wetu, sasa huko njiani ndio wakaviziwa, vijana wetu wakafariki saba. Kwa niaba yenu tuliwapa pole, wale majeruhi tulikuta wameshapona na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI]

wameanza kazi na walituhakikishia kwamba hatua zinachukuliwa ili kupunguza hayo maafa.

Tulikuta hayo maafa si kwa Watanzania tu, tulikuta vilevile na vikosi vya nchi nyingine. Pale kuna nchi nyingine zenye majeshi zinakaribia 30 vile vile na wenyewe majanga haya yanawapata. Tulikuta katika kipindi hicho karibu Askari wa nchi mbalimbali 151 vilevile walikuwa wamepoteza maisha. Kwa hiyo, katika operesheni kama hiyo, mambo haya yanatokea lakini hatua zinachukuliwa ili kupunguza hayo maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka niliseme tu hili kwamba vijana wetu wanaendelea vizuri na jambo la kufurahisha ni kwamba katika hizo nchi karibu 30 ambazo zina majeshi kule Darfur, Kiongozi Mkuu wa Majeshi yote hayo ya *UN* ni Mtanzania. Anaitwa Luteni Kanali Paul Mela, ndio anayeendesha majeshi yote ya Umoja wa Mataifa kule Sudan. Kwa hiyo, wakati mwingine Watanzania tunaona kama sisi wadogo, kama tunajidhalilisha, kumbe dunia inatuamini, inatupa majukumu makubwa na tunafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunajifunza nini kule Sudan? Jambo moja kubwa ambalo tulijifunza ni suala la kudumisha amani ndani ya nchi. Wale wenzetu amani imewaponyoka, tulikuta lile Jimbo la Darfur ukubwa wake ni kama nusu ya Tanzania. Tulikuta kuna wakimbizi, yaani Wasudani wenyewe ni wakimbizi ndani ya nchi yao zaidi ya 1,200,000. Kama idadi ya Mkoa mzima wa Singida, wote wanakaa kwenye Makambi, wote ni wakimbizi wa ndani. Nyumba zao walizokuwa wanaishi nzuri, wameziacha, wako kwenye vibanda vya nyasi kwa maelfu na maelfu; milioni moja na laki mbili kwasababu amani imewaponyoka.

Ningekuwa na uwezo ningewapeleka Watanzania wakaangalie madhara ya kupoteza amani ni yapi. Maana wakati mwingine lugha zetu zinaashiria kuvunja amani kwasababu madhara ya kuvunja amani hatujayaona. Sisi wenzenu tumeona. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI]

Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, sisi ndio viongozi, sisi ndio walinzi wa kwanza wa amani. Nawaomba wananchi wa Tanzania tuepuke kabisa hali itakayotufikisha tuwe kama wale tuliowaona Darfur, wakimbizi ndani ya nchi yao kwasababu wamevuruga amani. Mtu yeyote ambaye ana lugha ya kuashiria kuvunja amani tumpuuze, tumdharau. Chama chochote cha Siasa kinachoashiria kuvunja amani, kukipuuze, tukidharau. Tusifike mahali wenzetu wa kule Darfur walipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Serikali, ningepena kuona kwamba hivi vyombo vya Ulinzi na Salama ambavyo ndiyo mhimili wa amani na utulivu, basi tunapopanga bajeti viwe katika kipaumbele. Kwenye taarifa iliyosomwa leo asubuhi ya Mwenyekiti wa Kamati yetu, imeonesha dhahiri kwamba katika maeneo sita ya kipaumbele, eneo la amani na utulivu halimo. Limo kwenye mazungumzo, kwenye maneno, lakini katika mgao wa bajeti halimo. Matoke yake ni nini? Matokeo yake vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vinapata bajeti ndogo, bajeti ambayo haitoshelezi wakafanya kazi zao kwa ufanisi, inayofanya kazi yenyewe ya kulinda amani iwe dhalili. Tusifike huko! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili hatulisemi kwa mara kwanza. Wakati tunazungumzia ule mpango, wakati tunaweka vile vipaumbele, Mwenyekiti wa Kamati yetu Mheshimiwa Anna Abdalah alilisema. Kwa hiyo, Serikali msiseme kwamba mbona mnaleta mambo katikati hapa? Tulilisema tangu mapema wakati tunaweka vile vipaumbele, tukaishauri Serikali kwamba katika vipaumbele hivi, hili la kulinda amani, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na lenyewe liwemo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa mwezi Machi Serikali itakapoleta bajeti tutizame: Je, hili Azimio letu kwamba vyombo hivi vipate kipaumbele, limo? Polisi anapopewa sijui lita tano za mafuta apambane na majambazi kwa lita tano kwa siku, ni sawa? Tutazame mishahara ya hawa wanaolinda amani usiku na mchana, tunawatendea haki? Magari, mishahara yao, nyumba zao za kuishi, zana za kazi: Je,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI]

zinawaimarisha walinde amani sawa sawa? Sasa tukikuta Serikali halijaweka vizuri mambo haya, mimi nadhani tufanye kama tulivyofanya wakati ule tulipokataa ya bajeti ya maji mpaka wakaongeza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayasema haya kwasababu tukipoteza amani tutafanana kama Darfur! Hatutaki sisi tuwe kama Darfur! Kwa hiyo, kuwekeza katika vyombo vya ulinzi na usalama, kuwekeza katika suala la amani halina mbadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuleta salamu za Darfur na mafunzo ya Darfur ili yatuisadie sisi tutazame jinsi gani ya kulea vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa *Capt.* John Chiligati kwa hotuba yako nzuri. Naamini kabisa Watanzania na hasa Waheshimwa Wabunge watazingatia usia wako.

Sasa tunaingia upande wa Waheshimwa Mawaziri; namwomba Mheshimiwa Ole-Medeye aanze na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi atafuata.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia mjadala huu wa taarifa za Kamati za Ulinzi na Usalama pamoja na Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwapa pole sana wananchi wa Jimbo langu ambao wameathiriwa na mafuriko yaliookea kuanzia mapema mwezi huu na yanayoendelea hivi sasa. Natoa pole sana kwa familia ambayo ilipoteza ndugu aliyechukuliwa na maji eneo ya Lekamba. Nasema pole sana. Natoa pia pole na rambirambi zangu kwa ndugu wote waliopoteza ndugu zao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI]

katika ajali iliyotokea juzi, eneo la Longido ambapo tumepoteza jumla ya watu saba katika ajali ya Noah iliyogongana na Lori. Nawapa pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi na usalama wa Taifa letu kwa kweli siyo jambo la kufanyia mzaha. Ni jambo ambalo linahitaji Taifa kuwa pamoja, tuwe na mshikamano na jamii kuanzia chini hadi uongozi wa juu tuwe na sauti moja katika kutetea masilahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa nafasi hii nimpongeze sana Rais wetu na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, pamoja na wasaidizi wake wote kwa maana ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote na Watendaji pamoja na Viongozi Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, kwa maana Mkuu wa Majeshi, *JGP*, Mkurugenzi Mkuu wa Usalama, Kamishina *General* wa Magereza pamoja na Maafisa wote na Wapiganaji wetu kwa kuendelea kuhakikisha kwamba Taifa letu linaendelea kuwa na amani, hususan kwa ulinzi imara wanaouiweka katika mipaka yetu ya ardhini, baharini, pamoja na angani. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuwawezesha Askari wetu kuweza kufanya kazi hizo kwa kuwawezesha kwa hali na mali ili waweze kumudu kufanya kazi hizo bila matatizo. Napongeza sana vikosi vyetu vinavyoshiriki katika ulinzi wa amani katika Mataifa mbalimbali ambapo punde tu Mheshimiwa *Capt. John Chiligati* alipotupa taarifa juu ya vikosi vyetu vilivyoko kule Sudan kwa kazi nzuri wanayofanya. Nawapongeza sana Makamanda na wapiganaji wote walioko katika vikosi hivyo huko Congo, Darfur na nchi nyingine ulimwenguni. Tunawapongeza na tunawahikikidhia kwamba tuko pamoja katika kudumisha ulinzi na usalama wa nchi hizo waliodhaminiwa na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi na usalama wa Taifa letu, kumekuwa na vitendo ambavyo kidogo vinaashiria kutaka kuvuruga ulinzi na usalama wa Taifa letu. Wako wahamiaji haramu. Hawa tuawapitisha sisi, wanafika na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI]

wanakaa kwenye nyumba zetu, magari wanayosafiria ni ya kwetu. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba Sheria itazamwe upya ili kuona uwezekano wa kutaifisha magari na mali za wale wote ambao watabainika wameshiriki kuwasafirisha wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninashauri kwamba ili kuimarisha ulinzi kuanzia ngazi ya familia hadi ngazi ya juu Taifani zitungwe Sheria ndogo au kanuni ambazo zitawapa nguvu Mabalazi wetu wa Nyumba Kumi kwanza watambuliwe rasmi kisheria na wapewe nguvu Mabalazi, Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Mitaa ya kuweza kudhibiti wahamiaji hawa wawe na nguvu wakiweza kuwakamata na kuwakabidhi katika vyombo vya dola na kuwachukulia hatua wakazi wa maeneo hayo ambao watabainika kwamba wanashiriki kuwahifadhi wahamiaji haramu.

Pia Sheria iboreshwe ili kuhakikisha kwamba wageni wote wanaingia katika mazingira yetu wanatakiwa kujisajiji na kueleweka walikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika hali ya amani katika Jiji la Arusha. Naishukuru sana Serikali, Rais wetu, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote na Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wakati lilipolipuliwa katika Kanisa Katoliki Olasiti pale Arusha tarehe 5 Mei, sote tulishirikiana kwenda kuwafaraji wahusika, kuchukua hatua za kuwezesha wale majeruhi kutibiwa pamoja na kuhifadhi ndugu wa Marehemu. Nashukuru sana Serikali kwa mchango mkubwa ambao imetoa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali katika Jiji la Arusha hivi sasa inaanza kuimarika kidogo. Kuna maridhiano ambayo yamepatikana baina ya Madiwani wetu wa Vyama vyote na hivi sasa wanafanya kazi kwa ushirikiano na kwa hali ilivyo, Meya wetu hivi sasa anafanya kazi akiwa na uhakika kwamba hapati tena usumbufu. Kwa sababu wale waliokuwa wakichochea Madiwani wamkane Mstahiki Meya,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAAZI]

natumaini sasa hivi wamejitambua na hata wenyewe wameanza kushiriki katika vikao vyote na Halmashauri ya Jiji sasa inasonga mbele vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari zilizotokana na vurugu ambazo zimekuwa zikiendelea Jijini Arusha ni nyingi sana. Hali ya biashara siyo nzuri.

Vurugu zile za maandamano pamoja na Mikutano ile iliyokuwa inatisha wageni, kidogo imeathiri biashara. Kwa sababu hiyo, ningependa tu nishauri kwamba ni vizuri sasa wale ambao watarudia kufanya hivyo siku zijazo kwenda kuchochea vijana kufanya vurugu katika Jiji la Arusha, wachukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kupitia Bunge lako Tukufu, kumwomba Jaji Mkuu atusaidie kesi ambazo zimetokana na vurugu pale Arusha zisikilizwe na ziamuliwe kwa sababu bila kufanya hivyo, wahusika wataendelea kufanya fujo kwa sababu wanatambua kwamba hawana wa kuwagusa. Kwa hiyo, tungeomba kesi hizo zisikilizwe na maamuzi yafanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba nishukuru sana kwa fursa uliyonipa. Asubuhi ya leo nimesikia kuna mtu mmoja wa Waheshimiwa Wabunge akizungumza hapa, alirusha makombora ambayo sijui chanzo chake, lakini baadaye nitaomba unipe fursa niweze kuomba mwongozo juu ya hatua za kuchukua dhidi ya mwanamme anayemvizia mwenzake wakati hayupo au wakati ametazama upande wa pili, anampiga ngumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nakushukuru sana.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Ole-Medeye. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Nahodha, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu katika mjadala wa Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. Nitazungumzia mambo manne.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni kweli wanajeshi wastaafu wa miaka ya nyuma wanalipwa kiwango kidogo sana cha pensheni ukilinganisha na wanajeshi wanaostaafu katika miaka ya hivi karibuni. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imelibaini tatizo hilo. Kimsingi, jambo hili linatokana na utaratibu unaotumika katika kuwalipa wanajeshi wastaafu. Utaratibu unaotumika sasa ni kuangalia mshahara wa mwisho wa Askari mstaafu na muda wake aliolitumikia Jeshi. Sasa ukiangalia miaka ya nyuma, kiwango chao cha mshahara kilikuwa kidogo ukilinganisha na leo. Bila shaka ukitumia utaratibu huo Askari hao wataonekana wanapata malipo ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea kufanya mashauriano na Wizara ya Fedha. Tutapendekeza njia ambayo tunadhani itaweza kusaidia katika kuondokana na utaratibu huo. Kama Wizara yangu ingekuwa na uwezo wa moja kwa moja, basi nadhani tungefanya hivyo. Lakini jambo lenyewe la malipo, hili lina athari kwa Serikali nzima na bila shaka busara inatutuma tuwe na mawasiliano ya karibu na Wizara ya Fedha. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Masoud kwamba tunaendelea kulifanya kazi jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni kweli Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa muda mrefu linakabiliwa na uhaba wa nyuma za kuishi Askari. Lakini kwa bahati nzuri Wizara yangu hivi sasa imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za wanajeshi baada ya kupata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 85 kutoka *Exim Bank* ya China na Serikali ya Tanzania itachangia Dola milioni 15. Hivi sasa ninavyozungumza, ujenzi wa nyumba hizo umeanza katika Mkoa wa Dar es Salaam. Nyumba hizo sasa zinaendelea kujengwa katika Kambi ya Lugalo na Kigamboni. Tumeanza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA]

na Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna Askari wengi zaidi ambao wana matatizo makubwa ya nyumba.

Jambo la tatu ni malipo ya familia za wanajeshi ambao walipoteza maisha katika operesheni za kulinda amani zilizo chini ya Umoja wa Mataifa hasa Darfur na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechukua hatua zifuatazo: Kwanza, mnamo 20 Septemba, 2013 Umoja wa Mataifa umeanza kulipa Askari watatu ambao wamefariki dunia mwezi Agosti, kule Darfur Dola 70,000 kila mmoja kwa hawa Askari watatu waliofariki. Jambo la pili, Jeshi la Wananchi wa Tanzania mwezi Oktoba, 2013 limewasilisha nyaraka za Askari waliofariki dunia saba Darfur nchini Sudani; na hatua ya tatu, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limewasilisha nyaraka za Askari watatu waliofariki Jamhuri ya Kidemodrasia ya Kongo, Umoja wa Mataifa tarehe 27 Novemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malipo ya aina nne ambayo yanashughulikiwa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ya kwanza, hivi sasa Serikali imeshawalipa Askari wote 13 waliofariki dunia katika Operesheni hizi. Mishahara ya miezi sita tayari imeshalipwa kwa familia. Mafao ya kifo (*gratuity*) haya bado hayajalipwa lakini tayari yameshawalishwa Hazina kwa ajili ya kushughulikia malipo.

Malipo ya aina ya tatu hulipwa mke; moja ya sita ya mshahara wa marehemu ambayo nayo tumeshawalishwa Hazina. Malipo ya aina ya nne, hulipwa watoto kama Mwanajeshi aliyefariki ana watoto, basi moja ya nane ya mshahara wa Askari aliyepoteza mshahara yanalipwa kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu itaendelea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA]

kulifuatilia jambo hili ili familia za Marehemu ziweze kulipwa malipo na mafao yanayostahili haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne, nakubaliana sana na Mheshimiwa Maryam Msabaha kwamba Wizara yangu inapaswa kuwaelimisha wananchi juu ya hatari ya kujenga nyumba karibu na makambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Ni kweli ni hatari sana kwa sababu Jeshi la Wananchi wa Tanzania linahifadhi zana za kijeshi na baadhi ya zana hizi ni za milipuko na milipuko yake siyo ya masihara, ni milipuko ya hali ya juu sana. Naendelea kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa pamoja tuwaelimishe wananchi juu ya hatari ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ni hatari kufanya jambo hilo? Kwanza, tunahifadhi zana za hatari ambazo zinaweza kulipuka. Lakini pili, kama tunavyojua kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania ndilo ambalo linalengwa na maadui; na maadui wanapotaka kushambulia katika nchi *target* yao ya kwanza ni Kambi zinazotumiwa na Majeshi ya Ulinzi na Usalamal kwa maana hiyo basi, naendelea kuwakumbusha wananchi wetu kwamba wasidhani wako salama kujenga nyumba karibu na makambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Kwanza kwa sababu kunahifadhi milipuko ambayo ni hatari sana, lakini la pili ni lile kwamba sisi ndio *target* ya kwanza. Kwa maana hiyo basi, tunawasihi wananchi watumie busara na hekima na tutafanya kila linalowezezana juu ya kutimiza azma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa maoni na mapendekezo yao mazuri. Napenda kuwahakikishia kwamba Wizara yangu itafanya kila linalowezezana kuyafanyia kazi maoni na ushauri waliotoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa ushauri na maelekezo wanayotoa mara kwa mara pamoja na *paper* yao ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye baadhi ya hoja zilizotolewa na Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kuhusu kuwa na waambata wa Uhamiaji katika Balozi zetu katika nchi mbalimbali; tumefanya kikao na Waziri wa Mambo ya Nje - Mheshimiwa Bernard Membe, atalisemea jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusu matumizi ya *sticker* badala ya kutumia mihuri katika *visa* za kwa wageni mbalimbali wanaokuja nchini. Jambo hili linahusu Wizara tatu. Nafurahi kuliarifu Bunge lako kwamba pia tumekaa, tumezungumza na kwa sasa hivi maeneo yasiyotumia *sticker* ni machache tu ambayo ni ya Balozi za Heshima. Utaratibu wake ni Wizara ya Mambo ya Nje, inafanya mikataba na wale watu wa Mabalazi wa Heshima kurekebisha suala hilo. Kwa hiyo, tumekubaliana miezi mitatu maagizo ya Bunge yawe yametekelezwa na kila mahali itumike *sticker*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni dukuduku la Waheshimiwa Wabunge wengi kuhusu raia wengi kujichukulia sheria mikononi badala ya kufuata utaratibu wa sheria. Tulijaribu kuangalia kati ya mwaka 2007 mpaka leo, watu wangapi wameathirika kutokana na raia kuchukua sheria mkononi, ambao watu wana tabia ya kuwaita “watu wenye hasira kali”? Lakini hawa ni wavunja sheria, sio wenye hasira kali. Kati ya mwaka 2007 mpaka 2013 watu waliouawa kwa utaratibu huu wa kuvunja sheria ni 4,055. Watanzania 4,055

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

wameuawa na watu wanaoitwa eti wana hasira kali! Hii ni tabia mbaya, kuvunja sheria! Haikubaliki, na Serikali inailaani vikali na kuwataka watu waache tabia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la posho ya Askari kuongezwa kutoka Sh. 150,000/= mpaka Sh. 225,000/= katika Bunge lililopita, naomba kuweka rekodi sawasawa. Bunge hili halijawahi kupandisha posho hii. Lakini nilidhani pengine Waheshimiwa Wabunge walioongelea wanatumia utaratibu ambao wakati mwingine Wapiga kura wangu wa Songea wanapenda kuutumia. Wakitaka uwafanyie jambo lao, wanasema Mheshimiwa Mbunge ulituahidi. Nami nikiona linatekelezeka, nasema sawa, niliwaahidi, nitafanya. Lakini ni *style* tu ya kusema, "tunahitaji". Kwa hiyo, tumesikia na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushahidi wa bomu la Arusha, Waheshimiwa Wabunge walioongelea walisema wanao ushahidi na kwamba wanasubiri Tume. Hakuna Tume yoyote itakayoundwa. Vyombo vya Dola vimewekwa kwa mujibu wa sheria, uko utaratibu wa kutoa ushahidi, wafuate utaratibu huo.

Kwa kweli tunahitaji sana ushirikiano wao kuwapata wanaohusika. Nasi kama Serikali, tumeongeza hatua za kuchukua kuimarisha uwezo wa Jeshi letu kufanya upelelezi. Tulimshauri Mheshimiwa Rais tuanzishe *Division* mpya ya *Criminal Intelligence*. Mheshimiwa Rais ameridhia na mwezi huu amemteua Kamishna wa *Division* wa *Criminal Intelligence* na kuianzisha rasmi.

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, wakati sisi tunachukua hatua hizi kwa dhamira safi ya kuhakikisha nchi yetu inaimarisha utulivu, umoja na mshikamano wake, na wenyewe watupe ushirikiano badala ya kuendelea kukimbia na ushahidi kwenye *briefcase*, kila siku nina ushahidi, nina ushahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watu walioachiliwa kwa msamaha wa *parole*, kwa mwaka huu ni 173.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kidogo kuhusu suala la chakula cha wafungwa. Naomba niseme tena, na hili tulilisema sana kwenye Bajeti iliyopita na sasa tunalisema tena kwamba ni kweli kiwango cha chakula cha Sh. 500/= hakitoshi. Mheshimiwa Nyerere amejitahidi kulisemea sana, amesema angalau tukifungwa Mawaziri na Wabunge wote wiki moja tutajua maisha magumu yaliyoko kule.

Kwa kweli tuisubiri kufungwa. Tushirikiane tuone, hiki kiwango hakitoshi. Wafungwa wanaishi kwa shida na Askari wetu wanaishi kwa shida kwa sababu wanalazimika kukopa huku na huko kila siku. Deni limeshavuka zaidi ya Shilingi bilioni 25 kwa kutaka kuwalisha wafungwa vizuri. Hatuwezi kuendelea hivyo. Kwa hiyo, kama Serikali, tunaiona changamoto hii, na tuna hatua za kuchukua lakini vile vile Bunge lituunge mkono katika kulimaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kusisitiza umuhimu wa ulinzi na usalama kuingizwa katika vipaumbele vya Taifa. Kati ya vipaumbele sita, Waheshimiwa Wabunge mmesisitiza kwamba Ulinzi na Usalama uwe sehemu ya vipaumbele. Nakubaliana nanyi kwamba hii ni hoja ya msingi, na mtu yeyote mwenye akili timamu ataona hii ni hoja ya msingi. *(Makoff)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sitta ndio anamwakilisha Waziri Mkuu, kwa hiyo, nadhani atalisemea hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uraia wa nchi mbili, suala hili lilishafikia katika hatua nzuri. Tulishafika mahali tukaandaa sheria, tulihitaji tu maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yalikuwa katika hatua za mwisho, lakini tulidhani pengine litabebwa na mchakato mzima wa Katiba Mpya. Ni maoni ya Wizara yangu kwamba jambo la uraia wa nchi mbili sasa ni wakati muafaka kuwa nalo. Watanzania wengi wanaoishi nje ambao wamechukua uraia wa nchi nyingine, hawajauchukua kwa hiari,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

wametafuta maisha. Wanakuja Tanzania mara kwa mara, likizo zote wako hapa na wakati mwingine wakishamaliza hiyo kazi inayoitwa kutafuta maisha, wanaishi kwa shida katika nchi zao. Kwa hiyo, ni vizuri tukalionga hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kama litaonekana kwenye mchakato wa Katiba Mpya, basi itakuwa ni jambo zuri zaidi, lakini kama itashindikana, itabidi lije kwenye utaratibu wa sheria. Lakini kwa kuwa Wabunge mliopo hapa ni sehemu ya Bunge la Katiba Mpya, nitaomba pia mlitazame mkijua jambo hili lina maslahi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalotaka kulisemea leo ni kuhusu suala la uzalendo kwa nchi yetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Leticia; tuna tatizo kubwa sana la uzalendo kwa nchi yetu, tuna tatizo kubwa la mapenzi kwa nchi yetu.

Mifumo yote iliyopo katika nchi nia yake ni kutusaidia tufike mahali tuwe wamoja, tushirikiane tujenge nchi yetu. Akifanya jambo jema mtu wa *NCCCR*, *CHADEMA* au *CCM* kwa faida ya nchi yetu nisione taabu kumpongeza. Vyama vyote vinawakilisha nchi yetu kwa faida ya nchi yetu. Hatuko kwa maslahi binafsi. Tukifika mahali tukakubaliana kwamba hatuko kwa maslahi binafsi, hapo tutakuwa kweli tumetekeleza uzalendo kwa nchi yetu na tunaweza kujenga nchi yetu. Tujenge utamaduni wa kuaminiana, tupende kufanya kazi, kushirikiana ili tuweze kujenga Tanzania moja yenye mshikamano na yenye maendeleo kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kusema. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tunakushukuru sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, atafunga pazia Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa kuishukuru Kamati yako ya kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Kimataifa kwa taarifa yakinifu, lakini pia taarifa yenye ushauri mzuri ambayo wameitoa leo. Lakini pamoja na hiyo, naomba niwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia masuala mbalimbali yanayohusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa imegusa changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili Wizara yangu. Kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema, changamoto kubwa ambayo inaikabili Wizara ni ufinyu wa Bajeti. Ufinyu wa Bajeti umepelekea tushindwe kutekeleza kikamilifu malengo tuliyojiwekea. Lakini pamoja na upungufu wa Bajeti hiyo, Wizara imeweza kufanikisha majukumu yake hasa katika jitiada za kuleta wawekezaji nchini, jitiada za kutafuta masoko, jitihada za kuweka sawa masuala ya diplomasia ya kiuchumi na kuziendesha Balozi zake pamoja na matatizo hayo.

Ningependa kwa nafasi hii kupitia kwangu na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kupongeza Makampuni binafsi hasa Viongozi wa Makampuni binafsi kwa kutambua mchango wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, na kutupa tuzo kwakushirikiana nao kikamilifu pamoja matatizo yote haya kakaika masuala mazima ya kufikisha kwao masuala ya uwekezaji, biashara na diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujaribu kuziba pengo la fedha tunazozipata katika bajeti na kiasi kinachotakiwa, Wizara kama nilivyosema huko nyuma, tumenunua majengo mawili mjini *Washington* moja, *New York* jengo moja na tunategemea kukamilisha mipango ya ujenzi *London* pamoja na Nairobi nyumba za kupangisha. Lengo la Wizara ni kujaribu kupata pesa zitakazojaribu kuziba hili pengo la bajeti ya Serikali. Tunategemea baada ya miaka miwili mambo yanaweza kuwa mazuri sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nijibu sasa mambo muhimu ambayo yamejitokeza. Kwanza kabisa ni suala la mpaka kati yetu na Burundi; Tanzania na Kenya; na Tanzania na Uganda. Ningependa niseme kwamba mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu 2013, Wizara zinazohusika kati ya Tanzania na Burundi, yaani Wizara za Mambo ya Nchi za Nje na Wizara za Ardhi zinazoshughulikia mipaka zilikutana Mjini Dar es Salaam, na pale tukakubaliana mambo yafuatayo: kwamba mpaka wa Burundi na Tanzania ni kweli una matatizo ya *beacons* yaani mawe ya mpaka.

Kutokana na hali hiyo, wataalamu wetu mwezi Januari, wa pande zote mbili watakutana kufanya *demarcation*, yaani kuamua mpaka unakopita, na mwezi wa Tatu mwaka 2014, Marais wawili: Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, na Nkuruzinza wa Burundi watakutana pale Mpakani ili kuweka Jiwe la kwanza la *beacon* zoezi ambalo litafuatiliwa na kuweka mpaka kamili kati ya Tanzania na Burundi. Kwa hiyo, mwezi Machi tutakuwa na mpaka unaoeleweka kati ya Tanzania na Burundi. *(Makofi)*

Kwa upande wa Tanzania na Kanya, na upande wa Tanzania na Uganda, tunasubiri tu kupata pesa ambazo zimeobwa kutoka *Treasury* na mara zitakapopatikana mapema mwakani zoezi kama hili nililolisema lililofanyika kati ya Tanzania na Burundi na lenyewe litafanyika. Tunatambua kabisa umuhimu wa nchi yetu kuwa na mipaka inayoeleweka ili wajanja wanaopenda kunyofoa vipande vya ardhi, kutoka huko huko makwao ikome na kukoma mara moja tukiwa na sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lililoulizwa kuhusu gharama za ujenzi wa Kituo cha *Julius Nyerere Conversion Centre*. Ningependa niwaarifu kwamba gharama halisi zinaeleweka, ni Shilingi za Tanzania bilioni 46.2. Hizo ndizo gharama za ujenzi wa jengo la *Julius Nyerere Conversion Centre*. Tunachojaribu kukifanya sasa ambacho hakijakamilika, ni ku-*qualify* au kupata thamani ya *exemptions* ambazo tulizitoa kwa Wachina, maana nazo ni pesa. Katika

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[WAZIRI WA WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

hizi pesa, bilioni 46.2, bilioni 21.6 tumepewa za msaada bure, bure kabisa, bilioni hizo ishirini na moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizo bilioni karibu 27 ndizo zitakazolingia kwenye mkopo unaoitwa *Concessional Loan* na mkopo huu tumepata *grace period*, yaani kiwango cha kukaa bila kulipa cha miaka kumi. Lakini tutakapanza kulipa baada ya miaka kumi, tutakuwa pia tuna miaka kumi ya kuulipa mkopo huu. Tuna uhakika Watanzania wakati huo wataulipa, maana hata sisi sasa hivi tunaendelea kulipa madeni ya zamani tuliyoyarihi kutoka kwa akina Mzee Mwinyi. Kwa hiyo, nadhani Serikali zinazokuja nao watalipia deni hili.

Ningependa niseme jambo moja kwamba jengo hili limejengwa kwa kufuata Sheria za China Sheria na kanuni za Uingereza tulizozioea sisi ni hizi za kupata *BOQ*, yaani thamani ya kila kitu kinachojengwa, kinaorodheshwa na ndipo pesa zinatolewa. Wachina hawafanyi hivyo. Kwa majengo yate mnayoyaona hayo, iwe *National Stadium* au lile la kwetu, kunakuwa na *package* inawekwa pamoja, lakini ipo, na baadaye ile *package* inakwenda China, kule ndiyo wanapata wenyewe makandarasi wajenzi, wanawapa ile Tenda, wanawapa na *BOQ* yao, halafu baadaye ndiyo wanakuja kuzijengea nchi zilizofanya maombi. Ndicho kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spikak, lakini ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, tutashirikiana na Kamati ya Mambo ya Nje ili ikiwezekana, tutawaomba Wachina watuletee makabrasha yale na tuyatafsiri kwa Kiingereza na hata kwa Kiswahili baadaye ili tupate kitu kinacholingana na *BOQ* kwa ajili ya kufanyia kazi. Lakini kazi ile imekwenda vizuri, na wametujengea jengo lenye heshima kwa nchi yetu na vikao mbalimbali vya Kimataifa vitakuwa vinafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuelezea suala la Mikutano kutokufanyika kwa Mabalizi. Mwaka 2008 ndiyo tulifanya Mkutano wa mwisho, tulitegemea kufanya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

mwaka 2010. Kwa mujibu wa Sheria zetu tunatakiwa kufanya Mikutano kila baada ya miaka miwili. Sasa mwaka 2010, kwasababu ya Uchaguzi Mkuu hatukuweza kufanya, mwaka 2011 - 2012 hatukufanya kwasababu kulikuwa na mabadiliko makubwa ya Mabalozizi; ilibidi kuwarejesha Mabalozizi 17 nyumbani, na kuwateua Mabalozizi 24 wapya. Zoezi hili sasa limekamilika na kwakuwa sasa tuna Mabalozizi wasiopungua 41 wapya, ndiyo sasa tumeomba pesa za kuwa na Kikao. Tulishindwa kufanya vile mwaka 2012 kwasababu tungeitisha kikao, baada ya pale kuna wengine wangetuaga hapo hapo kwamba mimi nimestaafu, narudi nyumbani kwangu. Sasa kumbe kusingekuwa na faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazingatia ushauri huo, lakini tutakuwa na Mkutano wa Mabalozizi hivi mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nimalizie kwa jambo la kisera tu kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kuruhusu Majeshi yetu yaende *DRC* kuifanya kazi ya Kihistoria, na kipigo walichokipata M23 kimepelekea siku ya tarehe 12/12/2013, juzi, kuwa na makubaliano yaliyowekwa saina Nairobi, yakijumuisha Uganda, *DRC* pamoja na M23 waliobaki. Sasa wakikubali kuacha vita, hatutegemei kusikia vita imezuka tena kule *DRC*. Imekwisha vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, napenda kuwashukuru Watanzania kwa tabia walioionesha kumuenzi vizuri sana Baba wa Taifa wa *South Africa*, Mzee wetu Nelson Mandela. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kama mlivyoona, ametoa hotuba ya kiistoria kwa niaba ya Vyama vya Ukombozi Barani Afrika.

Hotuba ile imetukumbusha siyo tu tulikotoka, lakini heshima ya nchi hii inazingatia kwamba uhuru wetu pekee hautoshi; uhuru wetu unakamilika pale tunapojitoa mhanga kuzisaidia nchi nyingine zinazotuzunguka kupata uhuru. Afrika ya Kusini imepata historia kupitia Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete jana inayoonesha njia ya uhuru wao toka ilipotokea Tanganyika mpaka walivyopata uhuru wa Afrika Kusini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, lakini napenda kuwashukuru Watanzania kwa mshikamano wa kumuenzi Baba wa Taifa wa Afrika Kusini, Mzee Nelson Mandela ambaye sasa hayuko katika dunia hii, yuko kwenye dunia ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie hapo, nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kama nilivyosema, atakayemaliza ni Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Samuel Sitta.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii ya Wizara yangu na kuweza kutoa majibu na maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kutoa taarifa kwamba kwa mujibu wa utaratibu niliouweka wa kuujenga uzoefu, nilimwandaa Mheshimiwa Naibu Waziri wangu aweze kuyatoa majibu hayo, kwasababu nadhani kazi hizi lazima tuwe tunasaidia kujijenga. Kama mimi walivyonijenga waliopita, nami namjenga yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa ridhaa yako, naomba Naibu Waziri aweze kutoa majibu ya Wizara. Mimi nina imani naye asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afrika Mashariki, ruksa.

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Natoa shukurani zangu zote kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuniadini, nitajitahidi kuchangia kwenye mada hizi zilizopo hapa juu kiasi itakavyoyumkinika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nipongeze Kamati zote hizi mbili kwa weledi na umahiri mkubwa sana wa jinsi walivyochambua mada hizi zinazohusu Wizara zetu na kuzileta mbele ya Bunge lako Tukufu. Lakini vilevile kwa maelezo mazuri ambayo yameelezwa na Waheshimiwa Wabunge ambayo yanatuhitaji sisi angalau tuyajibu kwa uchache wake na kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, yalileta utata mwingi sana hapa nyuma na nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania kwa kuthamini kwamba wao ndio waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, walisimama kidete hawakutetereka, na mwisho wake wakaja wakamuunga mkono Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupitisha Azimio katika Bunge hili juu ya msimamo thabiti wa Tanzania ndani ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambazo tumehisi kama Wizara tuzichangie kwa ajili ya manufaa na kuleta weledi kwa Watanzania, wajiamini na waishi kifua mbele kwamba yanayojiri katika Afrika Mashariki ni maamuzi yao na maamuzi ya nchi na maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwanzo ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la kuwa na *visa* moja ya utalii. Suala hili ni zito sana, lilijitokeza katika uhiari wa utatu, tukaonekana kama vile tumetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, tunatoa kauli kwamba *Visa* ya pamoja ya Utalii Tanzania hatujaipinga. Sisi tunaitaka, lakini tunalolieza ni kwamba, lazima mchakato maalum upite ili nasi tuwe tunatembea na kujiamini na wale ambao wanatumia *Visa* hiyo iwe ni watu ambao tunawaamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo matano ambayo Tanzania tunasema lazima yatimizwe. Jambo la kwanza, kuwe na mtandao thabiti ndani ya Balozi zote za nchi tano za nje na ndani ya nchi ambapo kutakuwa na uelewa wa nani kachukua wapi?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]

Jambo la pili, mbali ya kuwa na mtandao wa Balozi zetu za nchi tano za nje ya nchi, kuwe na mitandao mipakani ambayo sisi Tanzania tutakuwa tunajua mtu fulani kaingia wapi, na katika nchi zote tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, miuondombinu hii kwa hivi sasa haipo na sisi tunasisitiza lazima iwepo ili na sisi tujunge. Lakini kama hilo halitoshi, kunatakiwa kuwe na usimamizi maalum wa fomu na utendaji ili tujue anayekubalika mahali fulani, basi na sisi tunamkubali na anayekataliwa katika nchi fulani na sisi tunamkataa. Lakini kama halijafanyika hilo, sisi tunaona bado hatujawa tayari kuungana na wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine la tatu ni utoaji wa *Visa*. Tuna magaidi wengi sana ambao wengine wanaweza kupitia katika nchi nyingine kwa siri. Anaweza akatokea gaidi, akachukua *Visa*, ya kuingia Afrika Mashariki, China lakini akaenda kufanya hujuma katika nchi nyingine, kwa mfano, Alshababu. Tunataka lazima tuwe na mtandao wa kuweza kuwajua hawa, tunataka mtandao wa Balozi zetu, tujue nani anaingia na mwisho ugawanaji na ukokotoaji wa fedha za mgao wa hizi *Visa*. Haya yote bado hayajakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania, tunasema kwamba hatujakataa *Visa* ya pamoja, lakini tutaongana na wenzetu pindi haya yatakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa vizuri tu lijulikane, ni lile ambalo lilikuwa linafanana sana na hili, juu ya Umoja wa Himaya Moja ya Forodha. Nalo hili ni jambo ambalo lilikuwa linajadiliwa ndani ya Afrika Mashariki, ndani ya mfumo wa sasa hivi wa Afrika Mashariki na siyo ule wa utatu. Lakini tunashukuru sana kutokana na busara ambazo Watendaji wetu wamezitumia, Baraza la Mawaziri na mwisho *Summit*, Maraisi wamelikubali. Kwa hiyo, sasa hivi Himaya Moja ya Forodha ya Afrika Mashariki imekubalika na nchi tano zote na Maraisi wetu wamepitisha suala hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wameshapendekeza kwamba tuanze mchakato mwezi Januari, na huu mchakato unaanza. Mchakato wa kwanza ni kupitia Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ambayo tayari ipo itapitishwa tena. Mchakato wa pili, ni wanajumuiya kutazama mfumo mmoja kuweka *bond*; Mchakato wa tatu, ni kufuata taratibu za namna gani mizigo itatoka Dar es Salaam kwenda katika nchi nyingine au Bandari zetu zozote nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo mambo makubwa ambayo yalikuwa kidogo na hitilafu ningependa Watanzania waweze kunielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tulikuwa tunahisi na Mheshimiwa Betty amelizungumza vizuri sana hapa, ni jinsi ya uwianishaji wa Sheria ambazo zimetengenezwa katika Afrika Mashariki lakini ziwe *Domesticated* katika Sheria zetu za Tanzania. Napenda kutoa taarifa kwamba Wizara yetu imeshapitia Sheria nyingi za Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na hivi sasa tumezipeleka katika Wizara husika za Kisekta jambo linalobidi sasa Waheshimiwa Wabunge zitakapoletwa katika kalenda za Wizara za kisekta za *Registration Calendar*, basi nazo mzipitishwe ili tuwe tunakwenda sambamba na mabadiliko ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni kubwa kidogo lililojitokeza hapa, lakini pia Watanzania na Bunge lako mweze kulifahamu, ni suala la vipindi vya kuweka Bunge Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi, Baraza la Mawaziri limeshakubaliana vikao vyake vyote asilimia 50 vitakaa Arusha na hilo halina mbadala na asilimia 50 ndiyo vitakuwa vikizunguka kwa kuwa na *spirit* moja ya *exposure* ya kujitokeza sura yetu ya Afrika Mashariki nje ya nchi nne zilizobaki. Lakini vilevile Bunge letu la Jumuiya ya Afrika Mashariki, najua wakati mmekaa Wabunge hapa kulikuwa na matatizo mawili matatu yamejitokeza kule watu kutoka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI]

nje na kuingia ndani, vilevile limepitisha azimio la kwamba vikao viwili cha *Audit and Account* kimoja na kingine cha Bajeti, lakini na kikao kingine kimoja chochote kile kitakuja katika mfumo wa mzunguko.

Kwa hiyo, jumla Tanzania kutakuwa na vikao vitatu. Hili ni jambo ambalo limepitishwa na Umoja na Azimio ndani ya Bunge. Halikuweza kufanyika kwa kipindi hiki kwa sababu tu kwamba utaratibu wa kikazi wa mwaka mzima, kalenda imeshapitishwa na vilevile *Financing Bill* na *Appropotion Bill* ilishafanyika. Lakini tunaahidi kwamba tutalisimamia suala hili kwa vyovyote vile mpaka kijulikane kimoja na tuna imani kwamba utaratibu huu utafuatwa kwa ni utaratibu wa Azimio la Bunge la Afrika Mashariki, na Wabunge wetu wako imara kweli kweli kwa hili. Nawapongeza na huko waliko wajue kwamba Bunge lao linawapongeza kwa kusimamia suala hili na maslahi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya malimbikizo ya watendaji, posho ni kweli lipo. Lakini ningependa kutoa taarifa tu kwamba kwa kiasi kikubwa sana Hazina imetusaidia na tumeshapunguza karibu Shilingi milioni mia moja hivi na utaratibu huu kulingana na uhalisia wa fedha zitakapopatikana, Wizara yetu tutajitahidi kupunguza madeni haya bila ya kuathiri yale mambo ya kipaumbele ya Wizara yetu. Lakini tunaamini kwamba Wizara ya Fedha, Hazina na wahusika wengine watatusaidia kulipa malipo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kutokana na umuhimu wa Wizara yetu na ukuaji wa kasi ya Afrika ya Mashariki...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii lakini yako mengi ya kueleza. Nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afrika Mashariki, ahsante sana Waheshimiwa Mawaziri wote mliochangia.

Sasa namwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kwa niaba yake Mheshimiwa Vita Kawawa. Karibu sana Mheshimiwa Kawawa, naomba isizidi dakika thelathini.

MHE. VITA R. M. KAWAWA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia au kufunga mjadala huu kwa upande wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, naomba tuwashukuru Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi. Lakini pia naomba niwashukuru Mawaziri wote waliotoa ufafanuzi wa utekelezaji wa mambo mbalimbali ambayo yanashughulikiwa au yanatekelezwa yaliyokuwa yanatolewa hoja na Waheshimiwa Wabunge na Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge na ushauri, imeboresha mapendekezo ya Kamati. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Serikali ipo hapa, imesikia. Pia Kamati inaishauri Serikali iyafanyie kazi yale yote ambayo yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge na mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi michango yao imezungumzia hasa kutopewa kipaumbele mbele kwa Sekta hii ya Ulinzi na Usalama kibajeti. Ni kweli walichozungumza Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kutoweka kipaumbele hiki katika bajeti ni jambo ambalo linahatarisha amani ya nchi yetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. M. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI
YA ULINZI NA USALAMA (MHE. EDWARD N. LOWASSA)]

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli wachangiaji hao wamezungumza vizuri sana na wengi wao waliochangia katika eneo hili ni Mheshimiwa Lema, amechangia vizuri sana leo kwenye eneo hili, amevitetea vyombo vya ulinzi na usalama; Mheshimiwa Buyogera, Mheshimiwa Chilolo, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Dkt. Nkya, Mheshimiwa Vincent Nyerere na mwisho alizungumza vizuri sana Mheshimiwa *Senator* Chilligati. Kwa hiyo tunawashukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge hawa wamezungumzia madhara ambayo yanaweza yakajitokeza hasa kwenye bajeti kuhusiana na vitendea kazi, upungufu wa magari au uchakavu wa magari, mafuta yasiyotosha kama Kamati ilivyokuwa inazungumza, hali duni za Askari wetu na kutopatikana kwa fedha za chakula kwa wakati kwa Wazabuni wanaohudumia wafungwa walio Magerezani. Hii ndiyo *concern* kubwa kwa Kamati kwamba bajeti ijayo iwe jambo la msingi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Wabunge mkituunga mkono wakati ule wa bajeti ili eneo hili liongezewe bajeti na Serikali na liwe kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia Operesheni Tokomeza na Kipunga, na kuna baadhi ya wachangiaji wamekosoa. Naomba tu nieleze kwamba zipo operesheni mbili hapa; iliyosimamishwa kwa muda ni Tokomeza Ujangili, lakini Operesheni Kipunga ile ya kuondoa wahamiaji haramu, bado inaendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mheshimiwa Mzee Wasira anasema juzi ametoka Ngara, wakati anapita na gari akakuta watu wanakimbia milimani, akauliza kwanini wale wanakimbia? Akaambiwa wale wanakimbia kimbunga. Halafu akauliza, mbona kimbunga chenyewe sikioni, kiko wapi? Akaambiwa wale ni wahamiaji haramu, wanakimbia Operesheni Kimbunga. Kwa hiyo, operesheni hii inaendelea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. M. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI

YA ULINZI NA USALAMA (MHE. EDWARD N. LOWASSA)

na Kamati inasema operesheni hii iendelee kuwahamisha hawa wahamiaji haramu. (*Makofi*)

Pia kuna watu wamezungumzia dosari mbalimbali zilizojitokeza katika operesheni hizi mbili, nadhani wamezungumzia sana ile ya ujangili; Mheshimiwa Machali, Buyogera, Nkamia na Rweikiza wamekosa, wametoa dosari mbalimbali zilizojitokeza. Kamati inasema, hizo dosari zifanyiwe kazi, lakini tukumbuke hata Bunge letu nalo pia limeunda Kamati Teule kuchunguza mambo haya. Hivyo, naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge pia kwamba dosari hizi zinafanyiwa kazi na zitakaporekebisha Kamati inasema kazi iendelee kama kawaida lakini kwa uangalifu. (*Makofi*)

Pia tukumbuke katika maeneo haya Bunge letu Tukufu tuliruhusu Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Lembeli, wafanyie kazi dosari mbalimbali zilizojitokeza, naamini wanatuwakilisha vyema, wanaifanya kazi hiyo vizuri, lakini pia kuna Kamati teule ambayo imeundwa na Prof. Msolla kushughulikia malalamiko, nayo inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo kwa ujumla, naomba nirudie kwa watu mmoja mmoja ambao walitoa maoni yao.

Mheshimiwa Masoud yeye alizungumzia kuhusu Maaskari waliomaliza kazi zamani kwamba ameiomba Serikali itazame vizuri mfumo wa *pension* wa majeshi, usipishane sana kwa ngazi za wale watumishi waliostaafu wa jeshi. Kamati inasema, ni kweli na imekuwa ikishauri jambo hili lifanyiwe kazi kwa majeshi yote na itaendelea kuishauri Serikali ili iendelee kuboresha eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Machali naye alizungumza amezungumza mengi, lakini kama tulivyosema, aliyoyazungumza Mheshimiwa Machali ni moja ambalo ni illosema kwa ujumla hapa, Serikali inayafanyia kazi na Bunge pia linayafanyia kazi. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. VITA R. M. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI
YA ULINZI NA USALAMA (MHE. EDWARD N. LOWASSA)]

Mkuu pia alishakwenda katika Jimbo lake na hapa Serikali ilishasema kwamba ilisitisha yale aliyokuwa analalamikia Mheshimiwa Machali. Lakini ameomba Kamati yetu ifanye ziara katika Wilaya yake.

Naomba nimkumbushe kwamba kabla Kamati hizi mbili hazijatenganishwa, tulifanya ziara na tulienda katika Jimbo lake Wilaya ya Kasulu na tulikutana na Kamati ya Ulinzi na tulikutana na wananchi, lakini tatizo hili lilikuwa bado, kwa hiyo, hatukupewa tatizo hili. Ila kwa kuwa amelisema katika Bunge lako Tukufu, naamini na Serikali kama nilivyosema inalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chilolo, alizungumzia kutokulipwa kwa Wazabuni wanaotoa huduma za chakula walipwe, Serikali iangalie utaratibu wa kuwalipa ili wafungwa wapate huduma nzuri inavyostahili.

Ni kweli jambo hili na Kamati inaisisitiza kweli Serikali iangalie bajeti zinazotengwa kwa kuwahudumia hawa wafungwa kupitia Wazabuni walipwe fedha zao. Lakini kimsingi, Wazabuni hawa ni wale wafanyabiashara wa kati na wa chini ndio wanaotoa huduma hizi katika Magereza zetu. Sasa wanapocheleweshewa kulipwa malipo yao, maana yake tunawadidimiza kabisa kiuchumi na wafanyabiashara wa kati ndiyo wanao-*stimulate* uchumi wa nchi hii kwa sababu wako wengi. Sasa wao wanakopa, wanaweka dhamana nyumba zao, sasa tunaposhindwa sisi Serikali kuwalipa kwa wakati Bunge limepitisha bajeti yao, tunadidimiza uchumi wa wananchi hawa.

Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali ihakikishe inalipa madeni ya wazabuni hawa kama ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Masoud walizungumzia ucheleweshaji wa mafao ya Wanajeshi wastaafu. Kamati imelichukua hili tunawashukuru. Hata Umoja wa Wanajeshi wastaafu wametuandikia barua inayosema hivyo nasi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. M. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI

YA ULINZI NA USALAMA (MHE. EDWARD N. LOWASSA)

tumeshawasilisha kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili walifanyie kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandishi pia Mheshimiwa Christowaja naye amelalamika sana kuhusu tabia inayojitokeza sasa hivi ya utumiaji mbaya wa silaha ndogo za moto kwa wananchi wenye silaha hizo kuwaua wapenzi wao na watu wasiokuwa na hatia. (Makofi)

Tunamshukuru sana Mheshimiwa Christowaja kwa kuliona hili na kulisema kwa maandishi. Lakini Kamati inalaani vitendo hivi na inaishauri Jeshi letu la Polisi kupitia upya na wale wote wenye silaha ndogo, hizi *pisto*/kuhakiki kwa maana ya kuangalia kwamba kwa madhumuni yale waliyopewa kwa wakati ule na mwenendo wa sasa mtu alionao: Je, anapaswa kuendelea kuwa na silaha hiyo au hapana? Kwa hiyo, Kamati inashauri sana Serikali ifanye kazi hii ya kuhakiki. (Makofi)

Pia tunamshukuru Mheshimiwa Christowaja kwa michango yake mingine yote, Kamati imepokea na itaipeleka Serikalini ili waifanyie kazi.

Mheshimiwa Leticia Nyerere, tunakushukuru sana kwa kusema kwa ukali na uchungu kwa wale wote wanaodhihaki au kutumia majina ya viongozi wetu wakubwa waliotangulia, siyo vyema. Kamati inalaani na kukemea tabia hii sana. Sio ustaarabu na utamaduni wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mengine alizungumza Mheshimiwa Lema kuhusu chokochoko za udini na ukabila zinazoletwa na wanasiasa wanaotaka madaraka. Kamati inawashauri wanasiasa wote, kwa kweli tusifuuate au tusishawishi wananchi kupitia udini na ukabila. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mifano mingi ya nchi ambazo zimesambaratika kabisa kwa sababu ya udini. Leo hii Iraq chanzo chake kikubwa cha kusambaratika ni kwa sababu ya dini moja lakini Ushia na Usuni, lakini leo wamesambaratika kabisa. Kwa hiyo, Kamati inashauri

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. VITA R. M. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI
YA ULINZI NA USALAMA (MHE. EDWARD N. LOWASSA)]

wanasiasa wote tuangalie kabisa katika ushawishi wetu
tusitumie udini wala ukabila. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Lema alilalamika kuhusu suala la
kupigwa bomu katika Mikutano ya kwamba halikutamkwa
katika taarifa yetu. Naomba tu nimkumbushe kwamba katika
taarifa yetu ukurasa wa 12 (c) tumesema: "Vitendo vya
uhalifu dhidi ya watu wasio na hatia" na tumezungumza
kuhusu "ulipuaji wa mabomu." Kwa hiyo, ulipuaji wa mabomu
huu, unahusiana na Mkutano huo pia.

Vile vile Mheshimiwa Lema alizungumzia kuhusu
maandamano na akasema hakuna maandamano rasmi.
Mimi naomba niwashauri Waheshimiwa Wabunge, kwamba
tunapozungumza suala la maandamano kutokuwa rasmi,
maana yake ni kwamba hayajafuata sheria. Maandamano
yoyote ya binadamu, lazima ni rasmi kwa sababu watu
wanakaa, wanapanga na kwenda kuandamana. Hayo ni
maandamano rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria na
Katiba ya nchi yetu na sheria zake ni kwamba kuna utaratibu
wa maandamano.

Sasa yaliyopendekezwa na Kamati, tunaomba Bunge
lako likubali kwamba maoni ya Kamati kwamba Serikali ipitie
upya sheria zake ili hatimaye iandae Muswada wa sheria
utakaoweka utaratibu mahususi wa watu kuandamana,
utakaozingatia siku, muda, mahali, njia ya kupita ili
kuwawezesha wananchi watumie haki zao kuandamana bila
kuingilia haki za watu wengine au uhuru wa watu wengine.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Bunge lako
Tukufu lituunge mkono kwenye hili. Hata wenzetu Marekani
walioendelea leo kidemokrasia, ukiomba maandamano
unaambiwa utapita njia fulani, na utaenda sehemu fulani
na pale utasimama, utasema yako mpaka umalize na kwa
muda fulani; ukimaliza unaondoka. Lakini siyo kila mahali
wakati watu wanaendelea na shughuli zao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. M. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI
YA ULINZI NA USALAMA (MHE. EDWARD N. LOWASSA)]

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nilipata bahati mara mbili kwenda *New York* kuhudhuria Mkutano wa Umoja wa Mataifa. Pale kwenye Mkutano huo, Marais wanakuja dunia nzima na Marekani na watu wa dunia nzima; watu wanaandamana, lakini shughuli zinaendelea kama kawaida. Wanapewa nafasi yao mahali pa kufanyia maandamano yao bila kuharibu shughuli za watu wengine. Lakini tukiachia hivi, tutaharibu uchumi wa wananchi wetu waliokuwepo barabarani. Ndiyo maana Kamati inapendekeza kwamba suala hili lazima litengenezewe sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maandamano lazima yaratiwiwe. Sisi unajua ni wakulima, sisi kwetu hakuna ng'ombe; ng'ombe ndiyo tumeanza kuwaona sasa hivi. Nilikuwa natoka Dar es Salaam nakuja Dodoma, kufika katikati nikaona kuna mtu mmoja Mmasai kasimama kashika fimbo juu hivi halafu kundi la ng'ombe limesimama. Sasa mimi nikapita taratibu halafu nikasema kwanini? Amefanyaje yule? Tulipopita nikamwambia dereva wangu hebu simama nione. Akashusha ile fimbo chini *chap*, ng'ombe wale wote wakaanza kuvuka barabara. Kwa hiyo, maandamano yote yanaratibiwa! Hata ya ng'ombe yanaratibiwa. Hakuna maandamano yasiyoratibiwa. Itakuwa ya binadamu! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pia Kamati ililaumiwa kwamba imeandika tu habari ya bomu la *Olasit*. Kamati ilizungumzia bomu la *Olasit* kwa sababu ililetwa kwenye Bunge hapa na Kamati kama Azimio kulaani kitendo cha bomu lile. Ndiyo maana tumeleta taarifa hiyo hapa. Kwa hiyo, sisi tunaiomba Serikali, kama kuna maeneo mengine isisitize kama ilivyosisitiza leo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alivyoshauri kwamba kama mtu anao ushahidi aupeleke Serikalini ili Serikali iweze kuchukua hatua zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wengine wengi walichangia jioni hii naomba niwashukuru sana kuhusu msongamano wa Gerezani, akina Mheshimiwa Rweikiza, pia Mheshimiwa Nyerere, Mheshimiwa Maryam Msabaha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. VITA R. M. KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI
YA ULINZI NA USALAMA (MHE. EDWARD N. LOWASSA)]

amezungumza vizuri sana, tunamkushukuru sana na naamini Serikali imesikia na itayafanyia kazi haya yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wote mliyoyachangia na Kamati imeyachukua na itayasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mama Anna Abdallah kwa kunilea vizuri katika Kamati ile; pia Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ile kwa kuniadini mimi kuja kuwasilisha, kuandaa pamoja na kuwasilisha Taarifa ya Kamati na kufanya majumuisho leo mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Kamati yangu, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsante sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama
iliridhiwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Tunawashukuru sana Kamati ya Ulinzi na Usalama. Sisi wote kama Wabunge tunafahamu kabisa kwamba Kamati ya Ulinzi na Usalama inashughulika na mambo ambayo ni nyeti na tete, mambo mazito, siyo yote wanayoweza kuyaleta hapa, lakini kwa niaba yetu wanayafanyia kazi vizuri kabisa na kwa uaminifu mkubwa na wanatunza siri kwa kiwango kikubwa sana. Basi na Kamati nyingine tuige kidogo utaratibu huo. *(Makofi)*

Nichukue fursa hii kwa niaba ya Bunge niwatakie kila la heri Waheshimiwa Mawaziri na Wizara zote zile ambazo zinahusika na Kamati hii ya Ulinzi na Usalama na kuwatakia kila la heri katika kazi zao kwa mwaka unaokuja. Ni matumaini yangu kwamba tutakapokutana mwaka 2014, wakati wa Taarifa za Kamati, basi kutakuwa na mabadiliko kwa kutilia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKA]

maanani kwamba maoni na mapendekezo ambayo yametolewa yatakuwa yamefanyiwa kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo, sasa naomba nimwite Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Tafadhali unaweza kuendelea, una nusu saa. *(Makofi)*

MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU WA MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA :

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kunipa mimi nafasi hii leo ili kuweza kufanya majumuisho na michango mbalimbali ya Wajumbe, Wabunge, na Waheshimiwa Mawaziri wa Idara ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati yetu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa wiki hii ana dharura, ilikuwa yeye mwenyewe aje kufanya majumuisho haya, lakini kutokana na dharura, imebidi sisi tuweze kuongoza jahazi hili. *(Makofi)*

Nachukua nafasi hii kumshukuru vile vile Mheshimiwa Juma Nkamia. Kwa kweli Mheshimiwa Nkamia amesoma vizuri, *professionally* na nilisema naona hata *BBC* wanajuta kwa nini wamemwachia aondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Mawaziri wote; Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Manaibu wake na Katibu Mkuu wake. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Afrika ya Mashariki; Naibu Wake, Makatibu wake na Watendaji wao. Kwa kweli ni Wizara mbili zinazofanya kazi kubwa sana na zinahitaji pongezi kubwa sana, zinaitetea nchi yetu sifa kubwa sana za Kimataifa na katika *Regional areas*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana hatua ya Serikali na hasa tulivyomsikia Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa leo, akizungumza kuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

masuala ya *demarcation* wameyawekea kipaumbele, na siyo tu mipaka kati ya Tanzania na Burundi, inatakiwa mipaka yetu yote ambayo tumezungukwa na nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuitwi Tanzania, kwa sababu ya watu au bendera, au kwa sababu tu ni Wajumbe wa Umoja wa Mataifa; tunaitwa Tanzania kwa sababu ya *Territorial Demarcations* ambazo ndiyo zinatambua uhalali wa nchi yetu katika dunia. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hilo na kwa kupokea ushauri wa Kamati ambacho ni kilio chetu cha miaka mingi sana kuhusu mipaka ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wabunge wote kwa michango yao mizuri na ushauri ambao wameutoa. Niwahakikishie tu kwamba michango hii na ushauri huu, utatumika kuisaidia Kamati kuweza kuisimamia na kushirikiana na Serikali katika kuleta mustakabli wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia sasa hivi kwa juu juu kabla sijaanza kuwa *-identify* Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kwa maeneo mahsusi. Kulikuwa na suala la mipaka ya nchi yetu na majirani, ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, na Wabunge wengine. Kama nilivyosema, tunaishukuru Serikali, imeishaanza kufanya kazi na tutashirikiana nao vizuri sana.

Mheshimwia Naibu Spika, Mheshimiwa Betty Machangu alizungumza kwa ujumla suala la Mabalazi na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwajelwa. Hali ya Mabalazi wetu bado siyo nzuri. Hii inatokana na ufinyu mdogo ambao Wizara inapewa, nasi Kamati bado tunajitahidi kuisaidia Wizara ipewe Bajeti ya kutosha ili iweze kutoa heshima ya Mabalazi katika nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna viwanja. Ukienda Zambia, tunazo nyumba kama tisa; ukienda katika nchi nyingi sana tunavyo viwanja, lakini viwanja hivi karibu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

tutanyang' anywa kutokana na ufinyu wa Bajeti. Tunaomba tukitoka hapa leo, baada ya Taarifa hii kupokelewa, Watu wa Bajeti, na *Budget Committee* na Serikali waweke kipaumbele kuhakikisha viwanja hivi vinajengwa ili badala ya kulipa kodi, nyumba hizi ziweze ku-*generate funds* na iipunguzie mzigo Serikali kulipa kodi. Serikali inatumia pesa nyingi sana, takriban kwa mwaka siyo chini ya Shilingi bilioni 13, wastani kwa malipo ya kodi kwa Mabalozzi yote nchini katika dunia.

Kwa hiyo, uko umuhimu wa Wizara na Serikali kupokea ushauri. Nimeona nikushukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje; juzi nilikuwa Malaysia, nikaona Balozi alipewa waraka kutoka ofisini kwako ili aanze ku-*scout* kutafuta maeneo ambayo kama kutakuwa na *Financial Institutions*, kuweza kudhamini na tuwe na nyumba zetu katika nchi kama ile. Lakini vile vile siyo vibaya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ukajaribu kutazama ile mifuko yetu ya ndani, ambayo vile vile itaweza ku-*empower* Balozi zetu tukaweza kujenga Balozi zetu. Tukaweza kupata *revenue* na badala ya pesa hizi kulipwa Mabenki ya nje, zikalipwa *institutions* za ndani kwetu wenyewe, na tukajikuta ni *win win situation* ya Serikali na Mifuko hii.

Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, umeyazungumza sana mambo ya diplomasia ya uchumi. *More can be done*. Mambo mengi mmefanya, lakini mengi yanaweza yakafanywa kwa kushirikiana vizuri na Kamati. Bado tumeona kuna udhaifu wa wataalam au mnawakabidhi kazi za diplomasia za uchumi, kuwa bado *skills* zao, *negociation skills*, uelewa hata wa mali ambayo Tanzania inayo, kwao bado inakuwa ni ngumu kuelewa. Sitaki kutaja, kuna baadhi ya Mabalozzi, ukiuliza *deposit ya gas* Tanzania ni kiasi gani hawajui. Kwa hiyo, sasa hii inaweza kuwa ni taabu kuweza kuuza gesi na kadhalika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, mnfanya kazi nzuri, lakini kama nilivyoshauri, kitengo cha Diplomasia ya Uchumi ndani ya Wizara ni muhimu sana, kiweze ku-*compound* maeneo yote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

ya *natural resources* ili sasa nchi za nje waweze kutujua.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki. Namshukuru sana kwa msimamo wake kukubaliana na Kamati kwenye suala la *Economic Partnership Agreement – (EPA)*. Hii ni *burning issue* kubwa sana nchini mwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua. Mimi na wewe tuna bahati ya kuhudhuria kikao cha *ACP*, wewe ukituongoza ukiwa Mkuu wa *delegation* ya Tanzania. Tunapambana kweli kweli na wenzetu wa *European Union* kuhusu suala la *export taxes*. Wao wanataka ku-*impose 86% ya tax liberalization* kwa maana sisi tusipate chochote tunapo-*export* mali ghafi zetu. Hii tumewaambia, *over our dead body*, hiyo hiyo haitawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi ku-*compete* na Ulaya katika masuala ya kibiashara kutokana na *compliance* na sheria ambazo wao wamejiwekea. Nyama ya Tanzania ni nzuri kuliwa na Wazungu kutoka Ulaya wakiwa hapa kwetu. Lakini nyama ya Tanzania hairuhusiwi kupelekwa kwao kwa sababu ya kushindwa *comply*. Kwa hiyo, kuna *double standard* namna gani tunapambana katika mjadala huu wa *EPA*. Lakini jambo muhimu vile vile, tujaribu sasa kutafuta *regional markets*. Tu-*trade within ourselves!* Siyo lazima tutafute masoko ya nje. Tunao uwezo wa ku-*trade* ndani ya *regional* yetu na tukapata mapato makubwa sana ya kusaidia nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii vile vile iliweza kujadili mambo ya *International Conference of Great Lakes Region (ICGLR)* na hili eneo ni *burning issue* kwenye suala la usalama katika *Great Lakes Region*. Naipongeza sana Serikali. Naipongeza Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa namna wanavyofanya kazi katika *Great Lakes Region*, kuweka *stability*. Tumepeleka Majeshi *DRC*, siyo kuonesha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

nguvu. Tumepeleka majeshi *DRC; peace in DRC is peace* in Tanzania. Ndiyo sababu kubwa kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais na Wizara hii, kwa kuweza kuja na hoja kama hii na Kamati kuweza kukubali. Kwa kweli ni jambo muhimu sana. Kukiwa na amani kwa majirani zetu na sisi tutakuwa na amani. Tanzania imekuwa ni kisiwa cha amani, sisi tutakimbilia wapi wakati machafuko yanakuja hapa kwetu? Kwa hiyo, nilikuwa naomba tuweze kuendelea na moyo huo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo la Bajeti ya Afrika ya Mashiriki. Hiki ni chombo muhimu sana. Mradi tumekubali kujiunga na *East African Community*, lazima tukubali kui-*fund* kui-*fund* Wizara hii. (*Makofi*)

Wizara kwa mfano inapewa Shilling bilioni 15 katika Bajeti yake; cha kushangaza, Shilingi bilioni zaidi ya 12 zinakwenda kama *fee* na Shilingi bilioni tatu ndizo zinatumiwa kuweza ku-*run* Wizara hii. Haiwezekani kabisa! Hizi pesa zinakatwa na watu wadogo wadogo tu katika Wizara ya Fedha, Hazina. Lazima waambiwe! Sasa tuna *Budget Committee*, lazima sasa *Committee* hii i-*instruct* Serikali wakati Bajeti ya Wizara zetu zimepangwa, lazima kusiwe na makato. *Revenues* zipo, mkishirikiana na Serikali na Kamati ya Bajeti mtajikuta mnaongeza asilimia 50 ya hicho tunachokusanya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, michango ya Afrika ya Mashariki isiingizwe katika Wizara, ipelekwe moja kwa moja na Hazina, na Wizara waweze kupata fedha zao. Hii inaashiria kwamba hata Wizara haiwezi kuwa na Kitengo cha *Market Intelligence*. Bila kitengo cha *Market Intelligence* tuta-*compete* vipi na wenzetu? Tutajuaje wenzetu wanafanya nini? Lazima tuwe na Kitengo ambacho kitakuwa na *relevant data, strategy* za kusaidia Serikali iweze kupambana kiuchumia na kuhakikisha kuwa nchi yetu inakwenda mbele. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wamezungumzia suala la upelekaji wa fedha kazi Balozi zetu. Bado uko udhaifu kwa Ofisi za Balozi zetu kupata fedha *on time*. Utakuta sasa hivi *foreign service staff* wanateseka sana, fedha zinachelewa kwenda, wakati mwingine zinakwenda kwa awamu mbazo haziwezi kukidhi matumizi yao. Lakini nashukuru kwamba baada ya Kamati kupiga kelele ziko dalili zilizoanza kuonekana kwamba sasa hivi Wizara inapeleka fedha kwa *quarter* nne na inaonesha imani fulani kuwa sasa hivi Wizara imeanza kutekeleza magizo ya Kamati na Mabalazi wetu wanaanza sasa kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo utakuta tunapeleka wafanyakazi Ubalazi, hawa wanakuwa na mahitaji ya kukaa na familia zao, wana mahitaji kwa watoto wao kusoma na wana mahitaji ya *utilities*. Wakati mwingine hata *component* ya *utilities* inakuwa haipo katika kuwasaidia. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee kutafakari suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Serikali imejitahidi kupitia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tumepata magari kwenye Ubalazi magari mapya. Japo hayatoshi, lakini haba na haba hujaza kibaba. Hongera sana Waziri kwa kujitahidi, na ukipata misaada mingine jitahidi kuwasaidia Mabalazi wetu na wao wawe na heshima. *(Makoff)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi hatuwezi kuyasema hapa. Siyo vizuri kuyasema hapa tukaanza kujivua nguo, wakati kidogo tunayo matatizo lakini Serikali inajitahidi, na Wizara tunajitahidi, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mikutano ya Mabalazi ni muhimu sana. Toka mwaka 2008 mpaka leo hii Mabalazi hawajakutana. Yamezungumzwa hapa. Mimi nilikwenda mwenyewe kwenye Kamati ya Bajeti, na nikawaombea Shilingi bilioni moja. Kamati ya Bajeti iliahidi watatoa hizi pesa. Sasa sijui kama Serikali ndiyo bado hawajatoa, au ni kitu gani kinachogomba.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

Mheshimiwa Naibu Spika, upo umuhimu kwa Mabalazi hawa kukutana nyumbani ku-*share experience*, kuona upungufu, *challenges* ambazo wanazona huko waliko, mifano ya kuona nchi nyingine zinavyoendelea, ili na sisi tuige, tuweze nasi kuendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi nafikiri uko umuhimu kikao hiki kifanywe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara za Viongozi mbalimbali wanaokuja Tanzania, baadhi ya Wabunge wamechangia, kwa kweli nchi yetu ina sifa kubwa sana. Kwenye medani ya Kimataifa lazima tuseme *we are proud of our country*. Nchi yetu iko juu na inaheshimika. Ni mambo madogo madogo tu yetu wenyewe na hasa kwenye Media zetu. Wakati mwingine tena ni mfano mdogo.

Tazameni Marekani, Marais wakishapita, mambo yao yanakwisha. Hayazungumzwi mambo ya nyuma! Hapa gazeti likitaka kuuza, lazima waanze kuzungumza maneno ambayo siyo ya kweli, mradi tu kupata pesa kutokana na mauzo ya magazeti na ku-*dirty* na ku-*tarnish image* ya nchi. Naomba vyombo vya Habari, Wabunge tuibebe nchi yetu tuweke heshima ya nchi yetu kama tunavyoheshimiwa katika nchi za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uzalendo wa nchi, namshukuru sana Mheshimiwa Leticia Nyerere. Amezungumza *point* ya kizalendo, *point* ya maana, ameonesha uzalendo wake, ameonesha utu wake wa kuipenda nchi yake. *This is what should be done*. Nasi wote tuige mfano wa Mheshimiwa Leticia Nyerere. Mheshimiwa Leticia Nyerere, hakuleta masuala ya vyama. Ameweka mbele zaidi uzalendo wa nchi ndani ya Bunge na hiyo ndiyo njia ya kwenda nayo. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Leticia Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utamaduni, heshima kwa viongozi wetu; bado kuna watu wanaoanza mazuri waliyofanya viongozi wetu. Kitu kikubwa, tuachane kabisa kuwabeza viongozi wetu na tukumbuke mema waliyoyafanya. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitakwenda kwa wachangiaji mmoja mmoja. Tumeanza na Mheshimiwa Mwanjelwa, yeye amempongeza Mheshimiwa Rais kwa *speech* yake ya Afrika ya Kusini, nami nakubaliana naye *and I am adding my own words* kwa kusema *President Kikwete you have made us proud*. Kwa kweli. Alichokifanya Mheshimiwa Rais Kikwete, *and President Kikwete was at his best* jana tarehe 15 Disemba, 2013. Amefanya mambo mpaka Marais wa zamani waliokwenda pale kwenye mazishi ya Hayati Tata Madiba, walitoa machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Kikwete, amewakumbusha waliyosahau, amewaleza wasiyojua, mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Bara la Afrika, damu ya Watanzania iliyomwagika katika kuzibeba, na Mwalimu Baba wa Taifa alisema mwaka 1962, hakuna sababu ya kusherehekea uhuru wa Tanganyika wakati nchi nyingine za Afrika ziko kwenye mikono ya ukoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jana Mheshimiwa Rais Kikwete amewakumbusha waliyosahau na amewaambiwa wasiojua ni kitu gani Tanzania imefanya. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais, ume-*inspire* watu. Ume-*touch peoples heart*. Kwa hiyo, ndivyo namna ya Kiongozi wetu anavyofanya na sisi tufuate nyayo zake. Tuache kujikamulia ndimu wenyewe kwa wenyewe humu ndani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hati aliyopewa Mheshimiwa Mandela, hakupewa peke yake. Alipewa Samora Machel, Sam Nujoma, walipewa wakombozi wote; alipewa mpaka na Robert Mugabe, na wote walikuja ku-*train* hapa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui ulikuwa na umri gani wakati SWAPO walipokuwa Kongwa. Sijui kama unakumbuka! Kwa sababu mimi najua historia ya nchi hii ilivyo. Nami nilishiriki katika vita vya Uganda na vita vya Msumbiji kukomboa wenzetu. Kwa hiyo, nasema *I am proud of what I did for my country*. Nasi vile vile wote tujielekeze huko. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

Mheshimiwa Naibu Spika, hati za kusafiria alipewa mpaka Maryam Makeba kama mtamkumbuka. Hati za kusafiria alipewa mpaka Doroth Masuka, kama mtakumbuka. Maryam Makeba akaenda Guinea na kuolewa na Stoka Michael ambaye alikuwa ni Mwana harakati pamoja na Anjela Davis miaka ya 1970 kwa wale ambao mnaweza mnakumbuka. Kwa hiyo, nchi hii inayo historia kubwa sana katika harakati za ukombozi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda sasa kwa Mheshimiwa Leticia Nyerere. Nimezungumza mwanzo, umesema namna nchi yetu inavyo-*hold credit* katika Nyanja ya Kimataifa. Ni kweli kabisa. Umezungumzia dharau za kubeza viongozi. Kwa kweli tubadilike. Media ibadilike, Waheshimiwa Wabunge tubadilike, wananchi tubadilike, tuwe na hamu ya nchi yetu. Ziko changamoto! Hakuna nchi isiyokuwa na changamoto! Serkali ikubali vile vile changamoto hizi lazima zimalizwe. Haiwezekani changamoto zinaendelea tu, zinaendelea tu! Changamoto, zimalizwe wananchi na wao wa-*enjoy* nchi yao. Lakini kutokana na uongozi wa huu wa Mheshimiwa Rais Kikwete na Chama hiki, tufafika huko na *you will see, we will be on the top of the mountain*. *(Makofi)*

Vile vile Mheshimiwa Mbunge namshukuru, amezungumzia uraia wa nchi mbili. Nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kalizungumzia vizuri tu, kuwa suala la uraia wa nchi mbili uko katika hatua nzuri. Ni kweli, ni muhimu kuwa na kitu kama hicho. Tusiwe na *a blind nationalists*; unajua mtu mwingine anakataa, sitaki, sitaki; tuache mambo hayo. Tunao Watanzania wanaoweza ku-*contribute* katika *diaspora*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda Ethiopia, nawe ulikuwepo. *Diaspora* ya Ethiopia ina-*contribute* nchini mwao *five billion US Dollars* kwa mwaka. Hata sisi, wa kwetu wangepata nafasi wangeweza ku-*stimulate* uchumi nchini kwetu. Wako kule kwa sababu wanatafuta, hawataki kujenga kule, wanataka kujenga nyumbani. Kwa hiyo, nafikiri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

mchakato huu uendelee na tutazame namna gani unaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na mchango wa Mheshimiwa Khatibu Said Haji. Yeye alichangia kwa maandishi na alizungumzia vilevile uraia wa nchi mbili. Kwa hiyo, nafikiri majibu ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje pamoja na Serikali hili wataendelea kulitazama.

Vile vile ali-*point* hoja nyingine kwa suala la kwenda kuomba *Visa* kwenye baadhi ya nchi, unalipa Dola 200 lakini *Visa* yako inakataliwa na hurudishiwi pesa. Hili kwenye Kamati tumelizungumza sana, lakini nitaomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje ajaribu kulitazama kwa ku-*refund* pesa ambazo *Visa* hazitoki. Isije ikawa ni mradi, kwa sababu *Visa* nyingi hazitolewi lakini sasa pesa zinakusanywa na Watanzania wanaumia.

Mheshimiwa Betty Mchangu alizungumzia majengo na nilishazungumza mwanzo, nakushukuru sana Mheshimiwa Betty; pia kazungumzia diplomasia ya uchumi; ni kweli. Serikali inajitahidi sasa kuweka wataalamu kwenye Balozi zetu. Tusi-*concentrate* sana kwenye masuala ya siasa. Siasa sasa hivi kwenye masuala ya uchumi yamewekwa ni *second factor*. Sasa hivi *primary factor* ni diplomasia ya uchumi. Tuiuze nchi yetu vizuri ili wananchi wetu waweze ku-*benefit*.

Pia Mheshimiwa Betty Machangu alizungumzia jambo lingine la *disbursement* ya *fund* ambalo nimesema kweli lipo tatizo, lakini sasa hivi wanajaribu kulifanyia kazi. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje wanalishughulikia.

Jambo lingine ambalo Mheshimiwa Leticia Nyerere alilizungumzia ni suala la *terrorism*. Jamani masuala ya ugaidi ni masuala mazito sana. Usione jirani yako kaingiliwa sisi tukakaa. *Threat* kwetu ipo na ripoti za kiintelijensia zinasema, kwenye makambi ya *training* ya *terrorist* wanakutwa watu wanasema Kiswahili, wanasoma magazeti ya Kiswahili na wanasikiliza redio za Kiswahili. Kwa hiyo, ni lazima miongoni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]

mwetu wetu wapo watu wanapata mafunzo. Kwa hiyo, ni lazima tuwe *very careful*. Vyombo vinavyohusika lazima tuwe makini navyo. Ma-*terrorist* wanaingia maeneo wanatafuta *object of it*, wakishaanza kuona hamko pamoja, wataingia kwenye kikundi kimoja kutafuta *sympathy* ili waweze kufanikisha mambo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kikao chetu cha *ICGLR* tulikuwa tunazungumzia suala la *security* ya *Central African Republic*. Sasa hivi nchi zinaungana kujaribu kupeleka majeshi *Central African Republic* ku-*erode threats* za *terrorists*. Sasa hivi tayari kuna ugomvi kati ya Waislamu na Wakristo. Siyo jambo zuri. Lina-*trickle down* kwenye maeneo mengine, linaifanya *lake road region* haina *security*, inakuwa na *instability* ya *security* na hili ni jambo la hatari sana kwetu na kwa nchi ambazo tumezungukwa nazo. Lazima nchi yetu iwe *virtual, strong*, tuwe na *courage* na *wisdom* kwenye kutekeleza mambo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maeneno hayo, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Spika mwenyewe kwa kutupa fursa hii ya kuweza ku-*present* Kamati hii na nikushukuru wewe, niwashukuru Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya, nimshukuru Katibu wa Bunge, Makatibu wa Kamati; Ndugu Hussein Ramadhani na Ndugu Nesta.

Nitoe pongezi za rasmi kabisa kumshukuru Mheshimiwa Lowassa - Mwenyekiti wa Kamati yetu na Wajumbe wa Kamati yetu kwa kazi nzuri tuliyofanya kwa kuendelea kushirikiana na Wizara na Serikali. Sisi tupo tayari kufanya kazi vizuri na Wizara na ninafikiri Mheshimiwa Membe analijua hili. Mheshimiwa Membe mara nyingi nafikiri tukizungumza maneno makali, hatuzungumzi kwa ubaya, bali tunazungumza ili tukusaidie wewe uende mbele na huko mbele hujui kutakuwa na nini Mungu kakuwekea. Kwa hiyo, nilitaka tu kusema hivyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[MHE. MUSSA Z. AZZAN - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI
YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA]*

wa Kimataifa pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu Mbunge wa Ilala na Makamu Mwenyekiti wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na pia Mwenyekiti wetu wa Bunge, amehitimisha hoja yake kwa umahiri mkubwa sana. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Alichokiweka mbele yetu ni kwamba sasa Waheshimiwa Wabunge mkubali kupokea Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na mapendekezo na maoni ambayo wametuletea mbele yetu katika taarifa yao.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na
Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Utekelezaji wa Shughuli
zake kwa mwaka 2013 iliridhiwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Wote wameafiki taarifa hiyo na mapendekezo hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nawashukuru sana Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kazi nzuri na ambayo wamekuwa wakifanya na vilevile Wizara ambazo zinawajibika kwenye Kamati hiyo ambazo ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Wizara ya Ushirikiano wa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKA]

Afrika Mashariki, kwa kazi kubwa na ya heshima ambayo wamekuwa wakitupatia. Ni matumaini yetu kwamba mwakani mengi yaliyozungumzwa hapa yatakuwa yamefanywa kazi vizuri na hayatajirudia sana.

Niwashukuru sana kwa *compliment* ambayo mmeitoa kwa Mheshimiwa Rais kwa hotuba aliyotoa jana kule Afrika Kusini kwenye mazishi ya Mzee Madiba, kwa kweli ilitugusa wengi sana. Sisi wengine watu wa Kongwa tunakumbuka. Eeh, maana kuna kawaida ya kusahau historia. Shughuli yote ile ilianza Kongwa.

Baada ya *OUA* kukubaliana kwamba sasa ukombozi wa Kusini mwa Afrika, hawa jamaa lazima twende kwa lugha yao wanayoielewa, yaani lugha ya bunduki; baada ya kukubaliana *OUA* kule, kambi la kwanza kuanzishwa lilianzishwa Kongwa. Nikiwa mdogo, nakumbuka Rais wa Algeria alifika na ndege yake Kongwa, na mwaka 1967 hivi alikuja Rais Gamal Abdel Nasser na kutua na ndege yake pale. Unajua hizi historia zinapoteapotea hivi! (*Kicheko*)

Rais wa kwanza wa Msumbiji - Samora Machel, ameishi Kongwa; Rais wa Pili wa Msumbiji Mzee Chissano ameishi Kongwa na Rais huyu aliyepo hivi sasa wa Msumbiji ameishi Kongwa. Wangapi mnajua? Karibuni Kongwa! Rais wa kwanza wa Namibia Sam Nujoma ameishi Kongwa na Rais wa sasa wa Namibia ameishi Kongwa. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ni historia kubwa ya ukombozi wa Afrika. Rais wetu jana alitukumbusha mbali sana katika mambo haya. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje mnachokosea ni kwamba mnapokwenda huko hamumchukui Mbunge wa Kongwa hata siku moja. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ratiba yetu imekwenda vizuri mpaka dakika ya mwisho. Mheshimiwa Medeye!

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nimesimama kuomba mwingozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoja na kanuni ya 64(1)(f) na (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi wakati Godbless Lema akichangia mjadala wa Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alitamka maneno ya kuudhi na kukera sana ambayo yamenijeruhi mimi, familia yangu na wapenda amani wote Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godbless Lema alisema kwamba tunasema kwamba kuna Mawaziri mzigo lakini Ole-Medeye ni bomu.

Aliendelea kusema kwamba Mheshimiwa Ole-Medeye alishiriki Mkutano wa Viongozi wa Kimila uliofanyika Arusha na ambao ulitoa azimio kwamba katika chaguzi wasichaguliwe wachaga. Aliendelea kusema kwamba Ole-Medeye ana upendeleo katika ugawaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako juu ya hatua zitakazochukuliwa dhidi ya Mheshimiwa Lema kwa upotoshaji mkubwa alioufanya kupotosha Umma wa Watanzania na ulimwengu kwa ujumla kwamba sasa yeye anapoona kwamba anaelekea bondeni kisiasa anageuza mambo haya kuyaleta kwamba ni Ole-Medeye. Alisema kwamba ana *video* inayoonesha kwamba mimi nilishiriki Mkutano huo na kwamba kauli hiyo nilishiriki kuitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *video* hiyo iletwe Mezani kwako ili tuiangalie na tujue hiyo kauli niliitolea wapi? Naomba pia Mheshimiwa Lema aeleze bomu hilo lillilotegwa linaloitwa Ole-Medeye lina uzito gani na linalipuka lini. Awasilishe pia hilo Mezani kwako. (*Kicheko/Makofi*)

Naomba pia aeleze na alete ushahidi juu ya namna ambavyo mimi napendelea katika utekelezaji wa majukumu yangu. Hili limewaumiza watu wengi sana ambao wamepitia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMA NA MAENDELEO YA MAKAZI]

mikononi mwangu kupata haki zao wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Naomba alete ushahidi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru Mheshimiwa Ole-Medeye, Naibu Waziri lakini kabla sijasema chochote kuhusu mwongozo huo, bahati nzuri Mheshimiwa Lema yupo, umemsikia Mheshimiwa Mbunge mwenzako, sasa nakupa fursa kama una cha kusema.

MHE. GOGBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Ole-Medeye sio tu ni bomu la Taifa, lakini ni athari kubwa kwa Taifa. Nina ushahidi wa *DVD* na nitaukabidhi mbele ya Kamati ya Bunge ama mbele ya Bunge ikitakiwa, Mkutano ambao alihudhuria na Mikutano mingi ambayo amekuwa aki-*initiate* na Mkutano wa kwanza ambao ulifanyika kwenye Ukumbi wa Mkorea Arusha ambao nilitoa taarifa kwa Mkuu wa Usalama wa Taifa wa Mkoa wa Arusha wa siasa za ukabila ambao Mheshimiwa Ole-Medeye pamoja na kuoa mchaga, lakini amekuwa ni mtu akifanya siasa za ukabila sana.

DVD hiyo ninayo na iko kwenye *Youtube* na kama tungekuwa na muda, leo kabla ya chakula changu cha jioni ningeweza kuleta. Lakini ni mtu hatari. Kama tunaweza tukamsulubu Mheshimiwa Maghembe na Mheshimiwa Mathayo na kumwacha Mheshimiwa Ole-Medeye kuwa Naibu Waziri wa Ardhi kwa ushahidi nilionao ni hatari kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi huo ninao na nipeni tu taarifa niulete wapi.

NAIBU SPIKA: Waziri wa Maji - Mheshimiwa Maghembe.

MHE. PROF. JUMANNE ABDALLAH MAGHEMBE – WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Lema akinitaja. Ananitaja kwa sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. *This is completely unacceptable! He must apologise.*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi imemtaja....

WAJUMBE: Aaaaah!

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilinde!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi na mimi nathitibisha kwamba kati ya Mawaziri mizigo ambao wametajwa na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi na Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi ni pamoja na Mheshimiwa Maghembe. Sasa hili nilikuwa namsaidia kwamba yeye kama ni mzigo lipo bomu zaidi. Kwa hiyo, namuunganisha na watu wengine.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kanuni zetu zinakataza kwa kiwango kikubwa sana Wabunge kusemana katika mwanga huu uliofanyika leo hapa ndani ya Bunge. Sasa kwa sababu Mheshimiwa Ole-Medeye amelalamika na Mheshimiwa Waziri Maghembe naye vilevile amelalamika hapa na Mheshimiwa Lema anasema ana ushahidi wa mambo haya anayoyasema, basi taratibu zetu zinatutaka tulipeleke jambo hili kwenye Kamati ya Brigedia Ngwilizi inayoangalia masuala yetu ya Maadili ya Wabunge.

Kwa jinsi hiyo, suala hili nalipeleka huko. Kamati hii itawaita Wabunge husika, italitazama, na itamshauri Mheshimiwa Spika ipasavyo na baada ya hapo basi tutaona namna ya kuendelea na jambo hilo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU SPIKA]

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, kazi zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika. Kwa jinsi hiyo, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 1.33 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 17 Desemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)